ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria wa Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya shilingi bilioni 658,526,528,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30/6/2014, na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani ripoti ya ukaguzi wa hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za SMZ kwa mwaka 2011/12 na Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za SMZ kwa mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kwa niaba ya Kamati niwasilishe Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika kuhusu Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za SMZ kwa mwaka 2011/12, na Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za SMZ kwa mwaka 2011/12. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Marina Joel Thomas: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kwanza asubuhi hii ya leo na napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti na kwa kazi nzuri ambayo ameifanya pamoja na watendaji wake kwa ujumla. Mimi Mhe. Spika, nitachangia katika maeneo matatu, eneo la kwanza mfuko wa barabara, eneo la pili *E- Government* na eneo la tatu ni Idara ya Mhasibu Mkuu, nitaanzia na mfuko wa barabara Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mfuko wa barabara una jukumu la kusimamia matengenezo ya barabara mbali mbali hapa nchini, na barabara zetu Mhe. Spika, zinahitaji matengenezo kwa sababu ziko nyingi ambazo zimeharibika. Na katika kikao kilichopita na huu mfuko wa barabara walitueleza kuwa kuna changamoto karibu tatu mpaka nne; na moja ya changamoto walizotueleza ya kwanza ni chanzo kimoja cha mapato, ya pili uanzishwaji wa wakala wa barabara, na tatu ni uchakavu wa vifaa na upungufu wa wahandisi wazoefu na wenye ujuzi.

Mhe. Spika, hapa nilikuwa na ushauri kumuomba Mhe. Waziri, wafanye jitihada za makusudi kuanzisha wakala wa barabara, kwa sababu ukianzishwa wakala wa barabara suala la uchakavu wa vifaa, upungufu wa wakandarasi, ukosefu wa chanzo cha mapato haya yote yatarekebishika kutokana na kuwa na wakala, kwa sababu wakala atakuwa na uwezo mkubwa, atakuwa na vifaa vya kutosha kwa hiyo atafanya kazi zake kwa vizuri. Kwa hiyo naiomba tu Wizara kupitia Serikali kuanzisha wakala wa mfuko wa barabara.

Jengine Mhe. Spika, nitakwenda katika suala zima la *E- Government. E - Government* kwanza nataka nipongeze Wizara kwa hatua kubwa iliyopiga na ya kihistoria ya Zanzibar kutoka kwenye analojia kwenda dijitali. Pia naipongeza Serikali kwa dhati kabisa kwa kukubali mradi huu wa *E - Government*. Serikali imefanya jambo jema na inapaswa kupongezwa na wananchi. Hapa nilikuwa nawashauri Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, hichi kitengo ni kipya, na kitengo kikiwa kipya kinapata changamoto mbali mbali, kwa hiyo ushauri wangu tuiachie Serikali ifanye kazi zake angalau ioneshe utekelezaji wake kwa asilimia angalau 50 na sio kuunda kamati teule,

kwa hiyo tuiachie Serikali ifanye kazi kwa sababu huu ni mradi mpya, na kitu kikiwa kipya tunajua kama kinakumbana na changamoto mbali mbali.

Nitakwenda katika Ofisi ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Idara hii ina kazi ya kusimamia matumizi, mapato mbali mbali ya Serikali na ni hasa nitaangalia katika suala zima la wakaguzi.

Mhe. Spika, Wakaguzi wanakuwa na kazi ngumu, kwa sababu wanaweza kwenda kukagua na wakakuta mambo mbali mbali na pengine mambo mengine yanafanyika kwa kutokana na hamasa za watu. Lakini wakaguzi hawa wakiboroshewa maslahi yao labda wakipatiwa mafunzo ya mara kwa mara, kwa sababu wakipatiwa mafunzo ya mara kwa mara wakaguzi hawa wataweza kuwasaidia katika kuwajengea uwezo wao wenyewe kufanya kazi zao kwa uadilifu kabisa. Kwa sababu sasa hivi kuna mabadiliko mengi tu, kuna mabodi mbali mbali yanaundwa, kuna taasisi mbali mbali zinaundwa na wakaguzi wanatakiwa wakazifanyie kazi kabisa. Kwa hiyo wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ili waendane na mabadiliko ambayo yanajitokeza.

Mhe. Spika, naona mchango wangu ndio huo tu sina mchango mkubwa leo. Baada ya kusema hayo naunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kuwepo leo katika kukhitimisha bajeti hii. Mhe. Spika, juzi ulisema kama husifiwi bora mtu mwenyewe ajisifu kwa namna ya Baraza lilivyokwenda. Mhe. Spika, huna haja ya kutaka kujisifu au kusifiwa, historia imeshakusifu, historia imeshakuandika, kwa hivyo nataka tu na mimi nithibitishe ikae kwenye *hansard* kama historia imeshakuandika na imethibitika.

Mhe. Spika, Baraza hili tarehe 14/01/1980 kama Baraza ndio liliasisiwa rasmi na Rais wa Zanzibar Mhe. Aboud Jumbe, alizindua Baraza hili na Mhe. Jumbe, alisema hivi. Hii hapa ni hotuba ya Mhe. Aboud Jumbe; Rais wa Zanzibar, ya ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi, Jumanne tarehe 15/01/1980 kichwa cha habari ni Ngome ya Wananchi.

"Baraza lako tukufu katika bajeti ya mwaka huu, kikao hichi kimethibitisha kwa vitendo kama Baraza hili ni ngome ya wananchi na ni sauti ya wananchi"

Mhe. Spika, hayo yalisemwa mwaka 1980 lakini kikao cha safari hii cha bajeti na leo tunakhitimisha kimethibitisha rasmi kwa vitendo sio kwa maneno kama hili Baraza ambalo wewe unaliongoza ni ngome ya wananchi na ni sauti ya wananchi. Naomba kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe na Wajumbe wote wa Baraza hili kuthibitisha hilo kwa vitendo.

Mhe. Spika, jana ndugu yangu Omar Ali Shehe nataka nimpongeze sana, alisema wakati umefika sasa hivi tuko miaka 50 tunaadhimisha kesho kutwa Mapinduzi yetu. Iko haja ya kujitathmini na kujipima. Mimi nakubaliana na yeye moja kwa moja, na Mhe. Spika, ningekuomba katika matayarisho haya kama kuna Kamati imeundwa ya maadhimisho haya basi Wajumbe wako hakikisha watiwe kwenye kamati hizo ili waweze kuchangia kutoa maoni yao ili jambo hili lifanikishwe, kama halipo basi sisi wenyewe Barazani na sisi ndio ngome tutengeneze kitu chetu tuweze kuja na kitu maalumu kuadhimisha siku hiyo.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri Omar Yussuf. Mhe. Omar Yussuf ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, ni Mwenyekiti wa kamati ya kununua meli, ni Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia Uwanja wa Ndege. Sasa ametwambia ana matumaini 2015 meli yetu itatembea itafika Zanzibar. Tulipouza meli yetu ya M.V Mapinduzi kwa dola 4,010 tuliweka dhamana kianzio cha kununua meli, kwa hivyo wazo la meli lilitokana na awamu ya sita kuiuza meli ya M.V Mapinduzi na fedha zile zipo, moja inaanza ikifika milioni, awamu ya saba imekuja kutekeleza ununuzi wa meli ambayo ilikuwa kilio cha muda mrefu. Nachukua nafasi hii kumpongeza ndugu Omar Yussuf na Kamati yake kwa juhudi aliyoifanya na *inshaallah* Mwenyezi Mungu na yeye atakaa kwenye historia.

Mhe. Spika, kuhusu Uwanja wa ndege. Uwanja wa Ndege fedha zake zilitafutwa na awamu ya sita. Awamu ya saba ilifanya utekelezaji wa mikataba. Mhe. Spika, niruhusu nisome tabia zetu za Serikali yetu hii ya Mapinduzi.

Tarehe 11/08/2010, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Amani Abeid Karume aliliaga Baraza hili rasmi na kufungwa Baraza tarehe hiyo 11/08/2010, naomba nimnukuu.

"Mhe. Spika, nchi yetu inaendelea na utaratibu tuliojiwekea wa utekelezaji wa demokrasia kwa kupokezana uongozi wa nchi kwa njia ya uchaguzi. Awamu ya sita Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliingia madarakani Novemba 1 mwaka 2000 kufuatia uchaguzi mkuu uliofanyika. Muda wa Kikatiba na Kisheria wa awamu hiyo panapomalizika uchaguzi mkuu utafanyika tarehe 31/08/2010".

Mhe. Spika, sisi tuna utaratibu wa kupeana kibendera. Mzee Karume yeye alipindua, lakini mbio za vibendera baada ya kuuawa alikabidhiwa Mhe. Aboud Jumbe, yeye alipeperusha bendera na yeye akamkabidhi bendera Mhe. Ali Hassan Mwinyi. Ali Hassan Mwinyi bendera akaipeperusha akamkabidhi Mhe. Idrisa Abdulwakil, na yeye vile vile akaipeperusha bendera

akamkabidhi Dkt. Salmin Amour (Komandoo), na yeye vile vile akampa bendera Dkt. Amani Abeid Karume, na yeye vile vile akamkabidhi bendera Dkt. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Spika, bendera hii tangu imetembezwa inatembezwa na Chama cha Afro Shirazi na Chama cha Mapinduzi, na bendera hii itaendelea miaka mingi ijayo itapeperushwa na Chama cha Mapinduzi. Ndani ya Baraza lako tukufu wako wagombea waliogombea mwaka 2010 tunaye Mhe. Haroun Ali Suleiman alitamani bendera aipeperushe kupitia Chama chetu, tunaye Mhe. Ali Juma Shamuhuna alitamani bendera aipeperushe, tunaye Mhe. Shamsi Vuai, hawa wametoka ndani ya Baraza hili. Pia tunaye ndugu Mohammed Aboud, alitoka ndani ya Bunge wote hawa Chama chetu kiliwapa idhini lakini hatimaye bendera akakabidhiwa Dkt. Ali Mohammed Shein kuiongoza Serikali hii ya awamu ya saba yenye mfumo wa umoja wa kitaifa.

Dkt. Shein ni muungwana kawachukua wote alioshindana nao. Nawaomba wote wale wampe mashirikiano na sisi Baraza tumpe mashirikiano.

Mhe. Spika, sasa niliona nitoe kidogo hiyo dibaji ya historia, kwa sababu mtu anasema haya mambo tuliyakuta sio utaratibu sawa, Serikali inabeba majukumu kwa sababu hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, yote tuliyopeleka mbele; ya nyuma na ya mbele ni yetu, kwa hiyo tuna wajibu wa kutekeleza wajibu wetu huo.

Mhe.Spika, tarehe 9/8/2010, Baraza lako tukufu chini ya uongozi wako liliweka historia kubwa sana, lilipitisha marekebisho ya kumi ya katiba. Katiba ambayo ilizaa Serikali ya Mapinduzi yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, naomba uniruhusu kwa heshima na taadhima kwa kuweka sawa *records* na *history* Mhe. Spika, ulisema hivi.

"Wajumbe naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo hii tarehe 9/8/2010 kukutana katika kikao chetu cha mwisho kwa ajili ya marekebisho ya Katiba katika ukumbi huu mpya.

Mhe. Spika, niruhusu niwataje mashahidi ambao historia itawakumbuka milele kwa kuwa wao ndio waanzilishi wa Baraza hili jipya, pamoja na kupitisha katiba ili *hansard* zikae sawa siku za mbele niruhusu niwataje.

1. Mhe. Pandu Ameir Kificho
2. Mhe. Kamal Basha Pandu
3. Mhe. Ali Mzee Ali
4. Mhe. Thuwaiba Edington Kissasi

5. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha
6. Mhe.Ali Juma Shamuhuna
7. Mhe.Abubakar Khamis Bakary
8. Mhe. Haji Omar Kheri
9. Mhe. Haji Faki Shaali
10. Mhe.Mwinyihaji Makame
11. Mhe.Ramadhan Abdalla Shaaban
12. Mhe. Suleiman Othman Nyanga
13. Mhe. Hamza Hassan Juma
14. Mhe. Machano Othman Said
15. Mhe. Adam John Mwakanjuki
16. Mhe. Samia Suluhu Hassan
17. Mhe. Burhan Haji Saadat
18. Mhe. Asha Abdalla Juma
19. Mhe. Haroun Ali Suleiman
20. Mhe. Sultan Mohammed Mugheir
21. Mhe. Mansoor Yussuf Himidi
22. Mhe. Zainab Omar Mohammed
23. Mhe. Iddi Pandu Hassan
24. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo
25. Mhe. Mzee Ali Ussi
26. Mhe. Khatib Suleiman Bakari
27. Mhe. Khamis Jabir Makame
28. Mhe. Shawana Bukheti Hassan
29. Mhe. Tafana Makame Mzee
30. Mhe. Zahra Haji Hamad
31. Mhe.Zakia Omar Juma
32. Mhe. Said Ali Mbarouk
33. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
34. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk
35. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
36. Mhe. Hamad Masoud Hamad
37. Mhe. Omar Ali Shehe
38. Mhe. Rashid Seif Suleiman
39. Mhe. Moh'd Ali Salim
40. Mhe. Asaa Othman Hamad
41. Mhe. Aziza Nabahan
42. Mhe. Najma Khalfan
43. Mhe. Nurdin Mohammed Nurdin
44. Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis
45. Mhe. Abass Juma Mhunzi
46. Mhe. Ali Abdalla Ali
47. Mhe. Ali Denge Makame

48. Mhe. Ali Haji Ali
49. Mhe. Ali Mohammed Bakari
50. Mhe. Ali Suleiman Ali
51. Mhe. Ame Ussi Juma
52. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
53. Mhe. Thobias Makungula
54. Mhe. Asha Bakari Makame
55. Mhe. Asha Moh'd Hilali
56. Mhe. Ashura Abeid Fereji
57. Mhe. Hindi Hamad Khamis
58. Mhe. Dadi Faki Dadi
59. Mhe. Fatma Abdalla Fereji
60. Mhe. Haji Mkema Haji
61. Mhe. Hasnuu Mohammed Hija
62. Mhe. Hija Hassan Hija
63. Mhe. Meja Khamis Juma Khamis Tindwa
64. Mhe. Juma Duni Haji
65. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
66. Mhe. Mkongwe Nassor
67. Mhe. Mohammed Kombo Mtanga
68. Mhe. Mustafa Mohammed Ibrahim
69. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
70. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
71. Mhe. Omar Ali Jadi
72. Mhe. Pembe Juma Khamis
73. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu
74. Mhe.Raya Suleiman Hamad
75. Mhe. Suleiman Khelef
76. Mhe. Salim Suleiman Ferouz
77. Mhe. Salim Abdalla Hamad
78. Mhe. Salmin Awadh Salmin
79. Mhe.Subeit Khamis Faki
80. Mhe. Suleiman Hemed Khamis na
81. Nd. Ibrahim Mzee Ibrahim (Katibu wa Baraza).

Mhe. Spika, hawa ndio mashahidi walioipitisha Katiba hii na sisi tutaingia tena tutafanya kazi.

Mhe. Spika, nataka nimpongeze Mhe. Waziri, kwenye hotuba yake kwenye *People's Bank*. Benki ya Watu wa Zanzibar lazima nimpongeze Mhe. Waziri, yeye alikuwa Mjumbe wa kuifufua. Tulipoingia madarakani mwaka 2000 benki ilikuwa hali yake ni mbaya sana. Ikaundwa Kamati na yeye ni mmoja, walikuwa hata *licence* hawa. Madeni ya Baraza unayajua Mhe. Spika, ilikuwa

hayajalipwa, mafao yalikuwa hayajalipwa, hali ilikuwa mbaya sana. Lakini ndugu Omar na wenzake wakaja na mawazo na Kiongozi Dkt. Amani Karume, benki ile leo ni benki moja katika benki kubwa katika Tanzania, na sisi ni wafanyabiashara wakubwa wa benki hii. Hivyo nataka nichukue nafasi hii Mhe. Spika, nimpongeze Meneja Mkuu wa Benki pamoja na Waziri kwa kuweza benki kuifanya hivi.

Mhe. Spika, katika kitabu kuna sehemu hii ya mitaji ya umma. Mitaji ya umma ndani yake kuna mashirika. Mhe. Spika, Makamu wa Pili wa Rais, alilihutubia sana Baraza hapa akaahidi kuwa Serikali hii itasimamia kuondosha ubadhirifu, wizi na maovu. Sasa Wizara hii inasimamia mashirika yafuatayo, *People's Bank of Zanzibar*, Bima na ZSSF na taasisi nyengine. Lakini haya mashirika mengine ndani ya Baraza hili Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa msemaji mkubwa sana kuitaka Mamlaka ya uwanja wa ndege iwe mamlaka. Baraza lako tukufu hili awamu hii ya saba sheria ikapitishwa tukatengeneza mamlaka ya uwanja wa ndege. Tumesikia mengi Mhe. Spika, kuhusu mamlaka hii.

Mhe. Spika, nashauri haya mashirika ya Serikali yote ikiwa Bandari, ikiwa Meli yasimamiwe na mitaji ya umma, na Waziri asimamie kama hakuna sheria sheria tutengeneze wawe ndio wasimamizi wa mashirika haya, kwa sababu mashirika haya yana matatizo.

Leo kwa miaka yote ya nyuma kwa mara ya mwanzo Shirika la ZSTC limeweza kulipa mafao yake. Nampongeza sana Mhe. Nassor Mazrui kwa juhudi zake, ilikuwa hawalipi, sasa Mhe. Spika, nilikuwa naomba hilo.

Lakini Mhe. Spika, niruhusu nimnukuu Mhe. Aboud Jumbe, kwa hotuba yake aliyoitoa mwaka 1983 kidogo tu anasema:-

"Mapato yetu na matumizi yetu havilingani, matumizi yetu ni makubwa zaidi kuliko mapato yetu"

Naomba Mhe. Waziri na Baraza hili tukufu la serikali tuyazingatie maneno haya ya Mhe. Aboud Jumbe kuwa mapato yetu na matumizi yetu havilingani, matumizi yetu ni makubwa zaidi kuliko mapato. Sasa Mhe. Spika, tumekwenda muda mrefu sasa hivi *Alhamdulillah*, katiba hii tumeipitisha, tumepata utulivu ndani ya nchi na amani kidogo. Lakini sasa kuanzia Baraza hili tukiondoka Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukiwa sote wananchi na serikali sasa tufunge mkaja tunyanyue uchumi wa watu wetu, bila ya kunyanyua uchumi wa watu wetu itakuwa matatizo. Sasa tukaze buti.

Mzee Karume alipomaliza muda wake alipouwawa akafa aliacha *25 million pounds* katika *reserve* ya benki yetu London, kwa wale watu wa mitandao hii Benki inaitwa *Moscow Narodny, Bank of London*. Benki hii ilianzishwa mwaka 1915 London, benki hii leo 2012/2013 inaitwa *EURO Finance Postal Bank* aliacha katika *reserve 25 million pounds* Mzee Karume kwa miaka saba hajakopa, hajakopeshwa.

Leo nichukue nafasi hii watu ambao wamerithi shilingi milioni tano, watu ambao dola ambayo tuishukuru na ni wenzetu wa kweli ni Uchina. Wachina walimpa Mzee Karume mkopo shilingi milioni mia moja basi, pesa zile Mzee Karume hazijaliwa zilitengeneza Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha Sukari, Uwanja wa Amani na Majumba ya Upenja ya Machina.

Lakini kwa kukaza ukanda aliweza kutengeneza TV ya Rangi, alitengeneza majumba mengi, barabara kutokana na bila ya mkopo na yeyote anayebisha a-c*hallenge* aseme baada ya Mchina. Lakini Mhe. Spika, nini funzo lake, funzo lake ubadhirifu na uchafu, wizi ulikuwa *controlled***,** sasa wakati umefika Ndugu Omar Yussuf kazi yako kubwa kuongeza mapato. Sasa tushirikiane pamoja tupunguke huku ili wananchi wetu wapate kuweza kuleta amani tuliyoikuta. Wazungu wanasema, *"An hungry man is always angry"*. "Mtu mwenye njaa kila siku anahamaki". Sasa wakati umefika tuondoshe ubadhirifu, tuondoshe uchafu tuwe safi.

Mhe. Spika, tunamaliza hili Baraza kuanzia kesho kutwa tutakabiliwa na mambo mengi huko mbele, tutakabiliwa na rasimu ya pili sio kazi ndogo, tutakabiliwa na Bunge la Katiba si kazi ndogo, tutakabiliwa na *referendum*. Kwa hivyo, miezi mitano tunayokwenda tutapambana na dharuba kubwa sana, lakini *Inshaallah* kwa utukufu wa siku ya leo *sabaa wa ishiriin Lailatulkadir* jana tumeiona na Mhe. Spika, jana nilikuona kwenye nuru nafikiri dua zako za usiku jana zilikubaliwa, Mwenyezi Mungu atatujaalia tuvuke kwa salama usalimini.

Mhe. Spika, hapa watu wengi sana hutoa historia, tumezungumza mambo mawili katika bajeti hii Benki Kuu pamoja na Mitaji ya Umma. Juzi watu hapa watu walituhesabia, Zanzibar Mheshimiwa ni nchi ambayo tulipindua, tulipindua nini? Udhalimu, uonevu, dhulma tukaleta utu na ubinadamu wa Muafrika na Wazanzibari, lakini watu wengi hawakusema kuwa Wachina ni watu wa mwanzo kututambua na kutuunga mkono. Ni kweli Wachina ni watu wa mwanzo, lakini ili tuweke hizi rekodi sawa Mheshimiwa nchi ambazo zilitutambua mwanzo mwanzo baada tu ya Mapinduzi na kufungua balozi hapa Zanzibar ni Ubalozi wa Urusi, China, Israel, GDR na Ghana. Hizi ni nchi ambazo zilifungua ubalozi wakati kabla hatujaungana, na nchi nyingi zilitutambua.

Sasa kabla sisi hatujatambuliwa kabla ya Mapinduzi Zanzibar ilijiunga na Umoja wa Mataifa. Mhe. Spika, hizi ni historia naomba unistahamilie ili tuweke *hansard* na vijana wajue. Mimi nina barua mbali mbali, katika kikao cha Umoja wa Mataifa cha *Session* ya 92 *Revolution* anasema, *"Having received the recommendation of Security Council of December 1961, that Tanganyika should be admitted to the membership of United Nation, having considered application for membership of Tanganyika decided***.**

Sasa Tanganyika wenzetu tulioungana nao waliingia *UN application* yao tarehe 14 Disemba 1961, lakini Zanzibar sisi tuliingia kukubaliwa tarehe 21 Disemba mwaka 1963. Sasa baadae tukapindua tukaendelea. Sasa Mheshimiwa niliona nitoe historia hii tujue. Zanzibar sisi tulipofanya Muungano wa nchi mbili ikazaliwa *United Republic of Tanzania* baadaye tukaungana leo ni miaka 49 nafikiri tumepiga hatua. Yako mambo mengi tumefanya kama tulivyoanza Baraza la Wawakilishi mwaka 1980 tulifanya tulipokuwa nyuma mwaka 1964, lakini Mhe. Spika, nithubutu kutamka Baraza la Wawakilishi la mwanzo kabisa leo tunao Wajumbe; Mjumbe wa mwanzo aliyeingia katika Baraza la mwanzo mwaka 1979 ni ndugu yetu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kaingia kupitia JUWATA, Baraza la mwaka 1980 ameingia Bi Zainab Omar kuteuliwa, leo *Alhamdulilah* tunao nyinyi hazina tuitumie. Mhe. Ramadhan Abdalla, Mhe. Zainab Omar tusaidieni nyinyi ndio waasisi.

Sasa Mhe. Spika, hizi historia ninazozizungumza lazima tuelewane. Jana palikuwa na mazungumzo ya Benki Kuu kuwa imesema haiwezi kuhudumia chumi mbili. Mheshimiwa haya mambo ya mabenki na mambo gani sijui sisi tulianzisha benki yetu *People's Bank*, paliundwa tume maalum ya kuanzisha *People's Bank* na *People's Bank* ikawa *Central Bank,* mwaka 2003 hapa tukaifanya kuwa *Commercial Bank.* Yako mambo Mheshimiwa tunao uwezo wa kuyafanya, tumefanya mabadiliko ya kumi ya Katiba, tumeweka bendera, tunapiga wimbo wa taifa. Yako mambo yako ndani ya mikono yetu kama Zanzibar, jambo la uchumi ni jambo letu tujitahidi tunyanyue hali za wananchi wetu ili tupate kwenda kwa salama na amani, tunaweza, Baraza hili linaweza na serikali inaweza.

Narudia tena, hali ya uchumi wakati umefika sasa nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati hii kwa hotuba yake Mheshimiwa jana hujaisikia lakini utaiona, alifafanua kila kitu na nampa pongezi sana Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mnadhimu wa Chama chetu cha Mapinduzi kwa ufafanuzi bila ya kujali itikadi na bila ya kujali chochote. Sasa Mheshimiwa nimeona leo hii tuweke historia sawa, tushikamane na *AG* alisema, tumeweza kushikamana kwenye suala la mafuta, suala la Katiba na mengine, sasa Baraza hili lishikamane na wewe Mhe. Spika ndiye kiongozi wetu, tuijenge

nchi yetu, tukiondoka humu ndani sisi historia nayo itutaje kama tulivyowataja waliopita.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumze ni kwamba tuna mambo yetu nasema hivi, la mwisho nataka tuelewane. Mapinduzi yalifanywa na Chama cha Afro Shirazi, sasa tuna wimbo ambao tulikuwa tunaimba. "Mama yetu Afro Shirazi, Baba yetu Mapinduzi, Msimamo wetu Muungano, Siasa yetu Ujamaa, Wakoloni wababaishaji fikra, Mabeberu mabwannyenye, wapinga maendeleo Mabepari zii, Tanzania moto moto, Mapinduzi Daima".

Hii ndio *slogan* naiomba tuifufue, tuiendeleze, na ile meli itapokuja tulipoiuza na Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alikuwepo kule Baraza la Mapinduzi, na wengine tukasema hii meli ikiuzwa ikija nyengine tuite 'Mapinduzi Daima' natoa wazo meli ile iitwe "Mapinduzi Daima".

Sasa dakika tano ni nyingi nachukua fursa hii Mhe. Spika, kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu hili kwa kushikamana, kwa kushikana na kuendeleza hili Baraza lenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Na wewe mwenyewe Mhe. Spika, nakupongeza sana kwa kutuongoza, na mimi nachukua fursa hii kwa kuwa nafunga dimba leo nijipongeze mimi mwenyewe nafsi yangu kwa kuwa nihai na mzima na historia nilivyokumbuka.

Mheshimiwa wengine wamesema mia kwa mia lakini mimi naunga mkono mia mbili kwa mia mbili na Wajumbe wote nakuombeni tuunge mkono. Mhe. Spika, nakushukuru nawatakia Wajumbe Ramadhan njema na Eid Mubarak. Ahsante sana nashukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana, Mhe. Ali Mzee Ali ametukumbusha mengi sana na ukitaka kuendelea ni vizuri ukakumbuka umetoka wapi, uko wapi na unakusudia kwenda wapi; ndicho alichokuwa anatwambia Mhe. Ali Mzee kwa kifupi sana. Basi baada ya shukurani hizo kwa Mhe. Ali Mzee sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza kabisa nataka nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe, lakini la pili nataka nitoe shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuchangia kwa ufasaha kabisa bajeti sio tu ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, bali bajeti za wizara zote kuanzia ile ya Serikali. Nataka niwapongeze sana.

Lakini Mhe. Spika, kabla sijaanza kujibu hoja za Wajumbe zilizotolewa katika Baraza lako tukufu zilizoelekezwa ndani ya ofisi yangu, naomba niseme mambo matatu ya msingi kabisa.

La kwanza, serikali ni endelevu, hatuwezi tukafika pahala tukasema kwamba sisi tumeyakuta, serikali ni endelevu yale ambayo yaliyoachwa, yaliyorithiwa na serikali hii lazima yaendelezwe kwa manufaa ya wananchi wetu, na pale ambapo pameonekana pana changamoto lazima changamoto hizo tuzikabili na ndio maana tupo hapa leo. Na namshukuru sana Mzee wangu, kaka yangu Mhe. Ali Mzee Ali kwa kuyaona mambo mawili alipozungumzia suala la meli na suala la *Airport Terminal.* Ule ndio uendelevu na ndio ukomavu wa serikali.

Lakini la pili Mhe. Spika, nataka niseme kwamba Wajumbe nimewasikiliza sana sana michango yao, wote kwa ujumla wao michango yao wameelekeza katika mambo mawili makubwa ndani ya ofisi yangu. Suala zima la kuimarisha mapato na suala zima la kuhakikisha kwamba mapato yetu hayavuji. Nawapongeza sana kwa hilo lakini nataka nimwambie tu somo yangu, somo yangu alisema jana ataniwajibisha mimi kama siwawajibishi hao wanaovujisha mapato. Kabla hajaniwajibisha nadhani nitawawajibisha hao wanaofanya ubadhirifu wa mapato.

Lakini la tatu Mhe. Spika, nataka niseme kwamba Wajumbe karibu wote wameunga mkono hoja yangu hii kwa asilimia mia, na wengine wamefika mpaka mia na arobaini, wengine mia mbili. Nawapongeza sana sana. Wako Wajumbe wawili mmoja amenipa asilimia 90, mmoja asilimia 80, lakini yote hiyo mimi naita A+**.** Kwa hivyo, hii inaonesha kwamba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wana imani kubwa sana na mimi, na mimi nawashukuru sana kwa imani yao waliyonipa na ninaahidi nitafanya kazi nao, na siku zote nasema pale ambapo wataona kwamba wana haja ya kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu, basi nawaomba wasisite wanisaidie ili tuweze kuwatumikia wananchi wetu kwa faida yetu sote.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa niwataje wale waliochangia katika hotuba yangu hii. Waliochangia kwa ujumla walikuwa ni 15 wamechangia kwa kusema pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ambao naomba niwataje.

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo)
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
4. Mhe. Omar Ali Shehe
5. Mhe. Asaa Othman Hamad

6. Mhe. Fatma Mbarouk Said
7. Mhe. Hamza Hassan Juma
8. Mhe. Mohammed Haji Khalid
9. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
10. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
11. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
12. Mhe. Saleh Nassor Juma
13. Mhe. Abdalla Moh'd Ali
14. Mhe. Marina Joel Thomas
15. Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Spika, wengine walichangia kwa maandishi naomba na wao niwatambue. Waliochangia kwa maandishi walikuwa ni watatu, Mhe. Mahmoud Muhammed pia amechangia kwa maandishi, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na Mhe. Salim Abdalla Hamad. Nawashukuru sana na wale ambao hawakuchangia sio kwamba hawana michango, wanayo, lakini wameona kwamba hotuba yangu inatosheleza na michango ya wenzao nawashukuru sana.

Mhe. Spika, naomba sasa kwa bajeti hii nibadilishe ule utaratibu wangu wa awali wa kutoa michango ya jumla, leo kwa sababu ninao muda mzuri nitakwenda mmoja baada ya mmoja kwa mujibu alivyouliza. Yako maoni yametolewa Mhe. Spika, na Wajumbe wengi nitapokuwa nachangia basi nitataja na fulani naye hili tumeshalizungumza.

Kwanza kabisa Mhe. Salmin Awadh Salmin amewasilisha taarifa yake kwa ufasaha kabisa na mimi namshukuru sana. Amesema kwamba ni lazima serikali kwa ujumla wetu tufuate sheria na kanuni za fedha na matumizi. Nataka nikubaliane naye na yeyote ambaye atakuwa hafuati sheria sio za fedha na matumizi tu, sheria yoyote ya nchi atakuwa amefanya kosa na nitamuomba sana Mdhibiti na Mkaguzi awe anaangalia kwamba taasisi isiyofuata sheria za matumizi kwa mujibu wa sheria za Mdhibiti ahakikishe kwamba anaichukulia hatua. Hatuwezi sasa tukakaa tu hivi tunasema tu, kila siku tunaambiwa tunasema tu, hata na mimi inanisononesha. Tunadhani kwamba Waziri wa Fedha ndio ana kila kitu, lakini kuna taasisi nazo zina mamlaka hayo.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Salmin alitaka tuzichukulie hatua taasisi ambazo zimechelewa kuwasilisha hesabu zake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, nasema nitawasiliana na Mdhibiti anipatie orodha ya taasisi zote zile na ni dhahiri kwamba *enough is enough*! Tutaangalia sheria nani ana wajibu na mamlaka wa kuzichukulia hatua taasisi hizi, nitamuomba kama ni mimi nitahakikisha kwamba hili halitarudiwa tena.

Vile vile alieleza kwamba wako watumishi wameshafariki lakini bado wanaendelea kulipwa, wengine wanalipwa mishahara wengine wanalipwa pencheni. Tumeanza kazi Mhe. Spika, tumempa kazi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali sasa hivi mpaka mwezi wa tisa atakuwa ameshazikagua wizara zote. Wale wanaopokelea mishahara benki tumerudisha kipindi hiki kwenye madirisha ili tuwajue halali wako wangapi, na tunamtaka Mdhibiti vile vile kwamba baada ya kumaliza tu mishahara aingie katika pencheni ili tuweze kujua wale tunaowalipa pencheni wako hai. Na lile zoezi ambalo amelisema Mhe. Hamza Hassan sambamba na hapo tutamtaka vile vile Mdhibiti alifanye, aangalie kwamba pencheni zimelipwa kwa mujibu wa mishahara yao? Afanye ukaguzi huo vile vile ili tuweze kujuana jamani.

Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Hamza pale anasema Mhe. Waziri kila siku unawajibia watu tu, unawajibia watu tu, nataka niseme na mimi nachoka kujibia watu tu, sasa nataka tufanye yale yanayotakiwa kufanywa kwa mujibu wa sheria ili kila mmoja ajue wajibu wake. Mhe. Spika, zoezi linaendelea na Mhe. Salmin unaweza kuwasiliana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu akakupa *up date* mambo yanakwendaje.

Wahasibu kukaa katika taasisi kwa muda mrefu. Hili limezungumzwa. Tumehamisha wahasibu wengi na sasa hivi wamebakia wachache lakini tayari tumewapa mpaka tarehe 31 Agosti wamalize kufunga hesabu waliyobakia nao vile vile watakwenda kwenye taasisi nyengine. Hili nalo tunalifanyia kazi na panapo majaaliwa ikifika mwezi wa Septemba wale ambao hatujawahamisha watakwenda katika taasisi nyengine ili kuendelea na taaluma zao na kazi zao katika taasisi nyengine.

Pia ametaka tuwapatie idara ya bajeti wataalamu wa uchumi kulingana na kazi zao. Tayari tumesha-*recruit* wataalamu na tunasubiri tupitishe bajeti tu ili tuweze kupata kuajiriwa katika idara hiyo.

Mfumo wa *PBB* amesema bado haujaeleweka. Nakubaliana na yeye haujaeleweka sio kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tu hata ndani ya serikali yetu bado haujaeleweka, tumekubaliana kwamba tutatoa mafunzo ikiwa ni pamoja na Baraza la Wawakilishi ili muwe karibu zaidi na mfumo huu na muweze kuuelewa.

Pia ametaka kuwa fedha za umma zitumike zaidi kwa yale mambo ambayo kila mmoja wetu anayaona. Nakubaliana na yeye, lakini kuna baadhi ya mambo lazima zitumike fedha za umma ambapo hatuwezi tukayaona. Leo tunazungumzia *infant and child mortality*; vifo vya watoto chini ya miaka mitano lazima tuelekeze nguvu vipungue, lakini huwezi ukaviona kama

vimepungua, kwa sababu mtoto wa jirani amefariki jana huku lazima tupeleke pesa vile vile katika sekta ya afya ili hivi vifo vya watoto viweze kupungua. Mhe. Jaku Hashim amefurahi sana na mimi nashukuru kwamba umefurahi na ninajua umefurahishwa na nini.

Lakini vile vile tunazungumzia *maternal health*, lazima tupeleke pesa lakini huwezi ukaiona. Kwa hivyo kuna mambo nakubaliana na yeye Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwamba tu-*inject more money* katika vitu unavyoviona. *seeing is believing* tutafanya hivyo Mhe. Mwenyekiti na nitakuomba tuwe karibu zaidi ili uweze kuyaona baadhi ya maeneo ambayo tutakayo *inject* fedha kama vile barabara, ujenzi wa bandari, ujenzi wa maeneo huru, haya ni mambo ambayo unayaona.

Mashirikiano madogo umeeleza kati ya mamlaka zinazohusika na mamlaka ya *ZIPA*. Hapa wengi wamelizungumzia suala la *One Stop Centre*. Mhe. Spika, hata na mimi napata tabu sana nadharia ya *One Stop Centre* na mfumo wetu wa uendeshaji napata tabu sana. Kwa sababu Mhe. Spika, hapa toka tumekaa mpaka leo mnasoma kwenye vitabu vya bajeti mafungu hayo yameidhinishiwa na Katibu Mkuu ya *so and so*, tumempa uwezo Katibu Mkuu ndio msimamizi na mshughulikiaji Mkuu wa shughuli ya wizara ile. Unakwenda *ZIPA* pale muwekezaji anapotaka ardhi mamlaka anayo Katibu Mkuu wa Ardhi hayupo pale hata akija Mkurugenzi hana *decision*.

Lakini kuna wengine humu ndani wametoa mawazo makubwa sana marekebisho ya Sheria za *ZIPA* tuone kwamba tunafanyaje. Na mimi nitakuja nayo Sheria ya *ZIPA* haraka iwezekanavyo, sasa hivi imeshakamilika, ili tuje tuone tunafanyaje. Lazima tuumishe vichwa kuitengeneza *One Stop Center*. Kwa mfumo wetu wa uendeshaji shughuli za kiserikali hapa *One Stop Center* itakuwa ni nadharia, akitaka *permit* muwekezaji mwenye mamlaka ya kutoa *permit* ni Kamishna wa Uhamiaji. Haya tuyafikirieni ili tuje tusaidiane ndugu zanguni. Na mimi nitafurahi sana nadharia ya *One Stop Center* ikiweza kuonekana.

Mhe. Spika, umetaka *master plan* ya *ZIPA* pamoja na upimaji wa maeneo ya *ZIPA* ukamilike. Hatua zimeshaanza na Katibu Mkuu wa Ardhi katika suala zima la kupima atatusaidia na yeye. Lakini vile vile tayari *ZIPA* kuna wenzetu ambao wanataka kutusaidia katika *development,* tunaomba waanzishe mazungumzo nao kuona jinsi gani tutakavyoweza kufanikisha ile dhana yetu ya kuwa na Maeneo Huru ya Kiuchumi.

Tumeeleza vile vile kuweka mashine za kutolea risiti, tumefanya kazi kubwa kidogo Mhe. Spika, hapa kwa sababu mashine ambazo zimeletwa na wenzetu wa *TRA* wa Dar-es Salaam zile zimegundulika kwamba wafanyabiashara

wanaweza wakazikwepa. Tumewatuma wenzetu *ZRB* wakaangalie hali ya Nairobi wameshakwenda wameshaziangalia kule, na sasa hivi tuko katika mchakato wa kuhakikisha kwamba tunafanikisha suala hili. Lakini sambamba na suala hili tuko katika mchakato wa kutengeneza Mtandao wa kushughulika na ulipaji wa kodi. Kwa hivyo, tunaliangalia na tunataka tulifanyie kazi kwa haraka sana ili liweze kukamilika.

Kuachana na *package tour* kinadharia nakubaliana na wewe sana, lakini tumeanza katika *finance* ile ya mwaka huu tulipoisoma. Wenzetu hawa wanapoleta watalii wanasema kwamba *package tour* ni dola 38 kwa mtu kwa siku. Tumewaambia sasa kwa kukimbia kodi ndio mnatwambia dola 38 sasa tunawaambia *no* tunataka dola 100. Kwa hivyo, tumeanza kwenye *finance* ile tutatizama hatua tutakazokwenda nazo.

Kudhibiti mapato ya *visa*; sasa hivi tunafunga mitambo ambayo itadhibiti mapato wa *visa*. Hakuna mtu atakayekuja kulipa *cash* pale. Unakwenda na *master card* yako, *visa card* yako, una *swipe*, huna, kuna kadi utainunua pale ya Benki utaingia na *visa* inatoka risiti unalipwa unagongewa unaondoka. Tumechelewa kidogo kwa sababu tulikuwa tunatengeneza mambo vizuri pale *Airport*, ili tuweze kuimarisha hii.

Kudhibiti magendo ya mafuta, kazi ni ngumu sana kwa sababu wanaofanya magendo ya mafuta ni ndugu zetu, watoto wetu, Wazanzibari wenzetu. Lakini kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi tumesema kazi hii tutaifanya kwa nguvu zetu zote, ni juzi tu Jumamosi baada ya kupitisha hapa Bajeti ya Miundombinu na Mawasiliano, nilikwenda kuizindua Bodi ya *ZRB*, nikagundua mapipa yameshakamatwa pale yako tayari.Tutafanya kazi lakini na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mtusaidie kutupatia taarifa, ili tuchukue hatua. Kwa sababu hii kazi ya magendo lazima tushirikiane kwa umoja wetu na mimi nimeamini itafika pahala itakwisha.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ametutahadharisha na ametuonesha kwamba jengo letu la Dar-es Salamu hali yake ni mbaya. Na tumeliona hali yake ni mbaya, tumejaribu kutenga milioni 80 kwa ajili ya ukarabati wa jengo lile na kama bado litahitajia ukarabati zaidi na fedha hizi hazitatosha basi siku za baadae tutaona jinsi ya kuangalia kuweza kuhaulisha kutoka vifungu vyengine ili tuweze kukaribisha ukarabati wa eneo letu.

Umesema Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Wajumbe wengine mfuko wa barabara utumike kwa malengo yaliyokusudiwa, wengine wamesema kama mfuko wa barabara kazi yake kukarabati barabara sio kujenga barabara. Nakubaliana na nyinyi lakini ukiisoma Sheria ya Mfuko wa Barabara inasema kwamba haijakatazwa ujenzi, na sheria tumeitunga wenyewe na ndio kwa

maana sisi kwa asilimia kubwa sana tunapeleka kwenye kukarabati barabara. Sehemu ndogo kama inahitajika kama ya dharura tena kama hiyo barabara ni muhimu kama barabara ya Mtoni tunasema basi saidia na kujenga, lakini *priority* kukarabati, unaposema *priority* ukarabati hata hapa ndani ya Baraza letu kanuni zetu zikisema vaa suti, *priority black suit* haijakatazwa suti ya aina nyengine. Kwa hivyo, na sisi tunaangalia zaidi tutakwenda kwenye kukarabati.

Mhe. Mwenyekiti, umezungumza sana na hili nitaliweka mwisho kwa sababu kuna wengine na Mhe. Ismail Jussa amelifafanua zaidi suala la 4.5 hili nitaliweka mwisho.

Mhe. Mwenyekiti umezungumza kutoa mafunzo kwa watumishi wa Serikali hasa katika utoaji wa takwimu; hii ndio *function* moja ya Mtakwimu Mkuu si watumishi wa Serikali tu wanatakiwa wananchi wote, kunatakiwa kutolewa mafunzo kwa watumiaji wa takwimu ili waweze kuzitumia. Vyenginevyo itakuwa una takwimu unaziweka zinakaa kwenye *shelf* tu, kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti zitakuwa hazisaidii kitu. Hili limechangiwa na Wajumbe wengine vile vile tutakuja kuona huko mbele wale waliochangia.

Chuo cha Fedha cha Chwaka. Mhe. Mwenyekiti, ametahadharisha kisiingizwe katika *SUZA*. Nataka niseme tu kwamba Serikali imeunda kamati iangalie vyuo gani ambavyo vinapaswa kuingizwa katika Chuo Kikuu ili tuwe na Chuo kikubwa zaidi. Ripoti hiyo haijaletwa bado Serikalini, itakapoletwa Serikalini itajadiliwa, na kwa sababu Mawaziri sote hapa ni Wajumbe wa *cabinet* tumesikia *concern* za Wajumbe dhidi ya Chuo cha Chwaka. Mimi nina uhakika kwamba tukikijengea hoja, lakini tusubiri Mhe. Mwenyekiti, ripoti ikishaletwa ndani ya Serikali ili tuone inapendekeza nini.

Ulisema kwamba Mameneja wa *PBZ* wanatafautiana mishahara; nimelisikia na nimewataka *PBZ* na nimemuomba Naibu Katibu Mkuu asimamie kuliangalia hili na kufanya marekebisho.

Mhe. Makame Mshimba yako mengine Mhe. Spika, nayaweka mwisho yana ujumla wake sio kama nimeyaacha hapa, hapana, yako mawili matatu yatakuja mwisho.

Mhe. Makame Mshimba umesema kwamba kufanya utafiti katika sekta ya uzalishaji ufanyike haraka sana. Hizi tafiti zinafanyika na zinafanywa chini ya Mtakwimu Mkuu, na nitamuomba Mtakwimu Mkuu akupatie ripoti za utafiti huu ili na wewe uweze kuangalia kinachozungumzwa na matokeo yake ni nini. Ulizungumzia sana Mhasibu wa Idara ya Ujenzi; pale nataka niseme tu

kwamba kweli kulikuwa na matukio pale Mhasibu huyu amesimamishwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi.

Sisi tumemuomba *CAG* alichunguze hili tatizo lote lilivyo halafu atuletee ripoti. Naomba sana Mhe. Makame Mshimba tusubiri ripoti ya *CAG* atakachotwambia *CAG* basi tutachukua hatua kama Mhasibu huyo ana haki au kama anataka kutiwa hatiani kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* tutaangalia. Vyenginevyo tutakuwa sote tunasema tu bila ya yule tuliyempa dhamana hajafanya kazi zake.
Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba alitaka kujua vile vile kuna waajiri ambao hawajawasilisha mafao ya watumishi wao *ZSSF*. Akataka kujua ni wangapi wameshtakiwa. Nataka niseme tu kwamba hilo tatizo lipo kuna waajiri taasisi za uajiri 15 ambazo hazikuwa zikiwasilisha makato ya watumishi wao *ZSSF*. Na 13 wako mahakamani, 2 wamesema jamani sisi msitupeleke mahakamani hayo mahesabu yote tutalipa. Hawa 13 wamekaidi tumewapeleka mahakamani. Na kila atakayekaidi kwa mujibu wa sheria tutampeleka mahakamani na *penalty* atakayechelewa.

Umetaka kujua huu mpango wa kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo waliozungumzwa na *PBZ* utaanza lini. Kwa mujibu wa kalenda ya *BPZ* utaanza Januari mwaka 2014 baada ya kupata maelekezo zaidi kutoka *BOT*.

Mhe. Mohamedraza Hassanali umeanza na kutaka maelezo juu ya shilingi elfu moja za simu. Nataka nieleze yafuatayo:

Ukifuatilia kwa karibu zaidi kuna mzozo kwa hii ya shilingi elfu moja. Na taarifa za karibu nilizozipata kwamba kuna mswada unakwenda Bungeni kuifuta hii elfu moja. Lakini sisi kama ulivyosema Mhe. Mohamedraza Hassanali simu ni masuala ya Muungano, ukitoza shilingi elfu moja tuhakikishe kwamba Zanzibar zinakuja zetu, au simu zote zilizokuwa *registered* Zanzibar zisitozwe elfu moja. Huo ndio uhalali, kwa hivyo hilo tunalitazama kwa karibu zaidi, wakifuta basi na sisi tutapumua na hawakufuta tunakwenda nalo sambamba hii haki yetu. Lakini kwa bahati nzuri vile vile Mhe. Mohamedraza Hassanali ulitaka nikuhakikishie mimi hili hawakunishirikisha. Watakayonishirikisha nitasema, hawakunishirikisha sisemi, nitasema hawakunishirikisha.

Kwa hivyo, sina sababu mimi ya kudanganya Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, sikushirikishwa, kwa sababu ningeshirikishwa ningesema kuna hili na hili tunagawana vipi tungeelezana mapema.

Deni la Serikali ulitaka kujua katika *22 trillions* Zanzibar tunadaiwa ngapi na nani analipa na hili si la Muungano. Hapa kidogo nataka Mhe. Mohamedraza

Hassanali unisikilize; deni katika hiyo *22 trillions* vyenginevyo wenzangu wa Muugano wawe na hesabu tofauti. Lakini hesabu niliyonayo mimi Zanzibar deni letu la Zanzibar mpaka kufikia Juni ni bilioni mia 255. Deni la ndani bilioni 50 na deni la nje ukitoa bilioni 205 ndio deni letu katika hiyo *22 trillions*.Lakini katika hilo deni letu la 255; 195 bilioni *Guarantor* ni *URT* kwa mujibu wa sheria. Na ukitaka hasa kuitizama hiyo sheria yeye ndiye anatakiwa awe mlipaji kwa 195. Kwa sababu Serikali ya Muungano ndiyo inayomdhamini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ukiwa *Guarantor* maana yake wewe ndiye unayetakiwa usaidie kulipa hiyo, hatujawahi kuambiwa tulipe. Kwa hivyo, deni letu sisi ni 255 bilioni kwa mujibu wa hesabu ambazo wataalamu wangu wamenipa.

Ulitaka vile vile nikuelezee tunadaiwa kiasi gani na *TANESCO* kuhusiana na umeme. Na ukaeleza utaratibu wa kulipana, mimi nashukuru maana mimi nimeshauanza kwenye kero za Muungano wale mawaziri wenzangu waliokuwepo walinisikia siku ile *ZECO* inadaiwa na *TANESCO* bilioni 38. Lakini lilipokuja katika kero za Muungano nikasema haya wakanitaka mimi nitoe *statement* ya kulipa, nikasema sawa tutaanza kulipa hapa hapa. Nikawaambia naeleza yale ambayo nimezungumza, nikawaambia na mimi ninawadaini *PAYE* mwaka 2011/2012 bilioni 18. Nikawaambia toeni bilioni 18 tukamilishe 20 na hizi 20 tunazitafutia njia za kuzilipa. Nilielewa kama kuna utaratibu wa kulipana lakini nilitaka *message sent* na Mawaziri wenzangu tuliokuwepo walinisikia kule.

Kwa hivyo Mhe. Mohamedraza Hassanali nakushukuru sana kwa haya maelezo ambayo uliyotupa na mengi tumeyasikia na tutayafanyia kazi. Mhe. Ismail Jussa na yeye amezungumzia mapato mengine nikifika kwake nitayaeleza vile vile. Somo yangu Mhe. Omar Ali Shehe mbona kaingia mitini leo. Amezungumzia kufanya tathmini ya Miaka 50 ya Mapinduzi.

Wengi wamezungumzia; Mhe. Fatma Mbarouk amezungumzia, Mhe. Ali Mzee alimelizungumzia, wengi tumezungumzia tathmini, tumeanza tena vizuri sana, kuthibitisha tumenza na *zero report* tukizama toka tarehe 12 Januari mpaka leo mafanikio na changamoto tulizozipata katika kipindi cha miaka 50 tumeanza. Ripoti haijakuwa tayari imeanza katika *zero draft*. Lengo letu tunataka tujijue ili tujitathmini wenyewe tunakwendaje. Kwa hivyo, nataka nimwambie somo yangu kwamba alichokiona yeye na sisi wenziwe tumekiona.

Lakini la pili amelizungumza vile vile kuwepo na kongamano, tutafuta pesa na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia tutafanya makongamano ili kuboresha ripoti yetu hii.

Alisema hatujaweza kuitumia kikamilifu bahari jana nilikuwa nawatawani wenzangu, kweli hatujaweza kuitumia kikamilifu bahari, Wazanzibari tumeitumia bahari kikamilifu kwa kuogelea tu maana Wazanzibari katika kuogolea ni wazuri kabisa. Lakini kuitumia bado hatujaweza *and this is one of challenges* katika Serikali ya awamu ya saba, na ndio maana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameunda wizara nzima Mifugo na Uvuvi ili kuielekeza huko kuitumia bahari.

Mimi mwenye dhamana ya Fedha na Waziri wa Uwezeshaji nataka niseme kwamba tutasaidiana na Mhe. Waziri ili tuweze kuitumia. Lakini hii bahari iko katika maeneo mawili; hapa maji mafu sijui ndugu yangu Mhe. Haji Omar Kheri anapaitaje hapa maana yake wazee wa Tumbatu hawa wana majina yao. Hapa maji mafu sisi watoto wa mjini ndio tunavyoita, maji ya nyayo hapa tunapatumia kweli kweli ndio wavuvi wote wako hapa, kile unachokwenda sokoni ukakinunua kile kinatoka katika maji ya nyayo hapa tunapatumia kweli, lakini hatujapatumia *deep* na huko nako tufanye utaratibu wa kuweza kutumia ili tuweze kuwapatia ajira watu wetu pamoja na kuweza kupata mapato zaidi ya nchi yetu, hapa ndio pale ambapo inapotakiwa kuhamasishwa sekta binafsi iweze kushiriki kikamilifu.

Alizungumzia vile vile kwamba bado hatujaitumia Zanzibar kijiografia; *geographical position* ya Zanzibar tumejipanga vizuri sana kuitumia *geographical position* ya Zanzibar, tumejipanga katika *expansion* ya bandari sasa hivi wataalamu wako kwenye *feasibility study* tumejipanga kuipanua *Airport* yetu. Mhe. Ismail Jussa anafurahi akisikia *Airport*.

Miradi ambayo imezungumza hapa na Mwanasheria Mkuu na nimekuwa nikiizungumza muda mrefu matangi ya uwekaji wa mafuta sio kwa ajili ya *domestic consumption,* kwa ajili ya *export,* mazungumzo yanaendelea. Nimesema kuna kampuni nne tunaendelea nazo na mazungumzo, tutakayoiona ipo *serious* tutaipa eneo waweke matangi *for export purpose*.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui amezungumzia vile vile maonesho ujenzi wa sehemu ya Maonesho ya Kimataifa unataka kuitumia Zanzibar *geographical* yake tutasaidiana *inshaallah* tuone tunafikia wapi.

Mmezungumzia nyinyi wenyewe uendelezaji wa *EPZ;* maeneo huru. Mhe. Spika, linalogomba hapa ni umasikini tu. Tukianza kutia sururu nchi hii tukavumbua gesi yetu na mafuta yetu basi mimi nasema haya yote yatakuwa ni historia yote haya. Hatujaweza kutumia vizuri rasilimali watu. Kwa kweli nasema nataka niwambie tu rafiki yangu kwamba rasilimali watu tunawatumia vizuri sana. Tatizo letu kubwa si kuwatumia, tatizo letu kubwa ni tija wanayoipata baada ya kutumiwa bado ni ndogo. Amezungumzia vile

vile *DIASPORA*. Kweli kuna kitengo cha *DIASPORA* kiko chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nacho vile vile tunakiandaa ili waweze kusaidiana na wenzao walioko ndani.

Alisema kwamba ili tuweze kuendelea tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Lakini nataniana na wenzangu wengine wanasema na mzungu awepo. Haina maana hapa kwamba ni mzungu sio *white man*, hapa maana yake ni tekhnolojia ili waweze kutumia fursa zilizopo. Nakubaliana na yeye hili tutaliangalia na tutalifanyia kazi.

Hili lilizungumzwa vile vile na Mhe. Hamza Hassan Juma alilitilia *ECHO*. Namna ya kufanya mapitio ya Sera zetu za Kiuchumi na Sera za Kodi ili kuwalinda wafanyabiashara wa ndani wadogo wadogo. Tuna sera hapa lazima uzioanishe, tuna sera ya Kukaribishwa Uwekezaji, tuna Sera za Kuwainua Wananchi wetu hizi lazima tuzioanishe. Nimeliona hili na nimesema hili muhimu sana kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, sina majibu leo moja kwa moja, mengine maana jana ilikuwa Jumapili na hakuna watu ofisini, lakini mengine yanahitaji kufanyiwa kazi ya kina kabisa ili Serikali itakapokuja hapa ije na maelezo mazuri zaidi na mipango mizuri zaidi. Mimi nimekufahamuni sana Waheshimiwa vyanzo vyetu vya mapato ni vichache ni kweli kama hajashughulikia, na ndio maana tunataka kwenda *deep sea*, na huu utaratibu wa meli inasajiliwa inalipa leseni tu si utaratibu muafaka.

Meli inasajiliwa *capacity* yake tani 30 ya samaki yeye analipa dola 30 elfu kwa mwaka mzima anachukua tani 30 anapeleka kwao si utaratibu mzuri. Nimesema tukimaliza bajeti hii tutafanya kikao Wizara ya Biashara, Mamlaka ya *deep sea* ili tuone tunakwenda na utaratibu gani. Kile kinachochukuliwa kule ni mali yetu, ile hakuna kodi aliyolipishwa kwenye ile mali. Sisi tumebakia tunatoa leseni tu mwaka mzima yeye anavua tu anapeleka kwao. Historia ametuonesha Magufuli alikamata meli pale meli moja tu samaki waliokuwemo ni *2 million dollars*. Naomba Waheshimiwa tushirikiane ili tuweze kufanikisha ushiriki wa sekta binafsi na kuisaidia sekta binafsi. Wazo zuri na ukisoma MKUZA *goal number 4* tumeeleza. Sekta binafsi lazima isaidiwe katika ku-*make product* zao. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tutalazimika kukaa ili kuona *to what extent* tumeisaidia sekta binafsi. Sekta binafsi ni lazima isaidiwe kutengeneza *skills* zao, kuna sekta binafsi wengine hawajui hata kutengeneza *statement* zao, *profile* zao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika, lazima tukae tutengeneze *strategy* ya kuzisaidia, sekta binafsi inatakiwa isaidiwe *finance*. Jana ilizungumzwa hapa,

sijui lakini tutaliona huko tukienda. Kuna Mheshimiwa mmoja aliuliza hapa ni sifa gani mpaka Wazanzibari waweze kupata mikopo *PBZ* ni Mhe. Jaku Hashim huyo nimekuona, na hata mimi niliuliza ni sifa gani? Uzanzibari wangu, na kwamba ile benki yangu haitoshi.

Nimewaambia wenzangu wa *PBZ you have to customize, if you can't beat them, join them*. Kama unaona wewe sifa zako haziwezi zikamsajili na kumpa mkopo Mzanzibari basi angalia Mzanzibari ana sifa gani, na kama haikuathiri *adopt* sifa zake, acha tuliangalie hili. Ndio wenzenu huko wanakopesha wala hawatazami sifa wala chochote, ilimradi ana kitu cha kukamata.

Nimewaambia hili tukataa, na nimemwambia Naibu Katibu Mkuu kwa sababu na yeye anatoka *PBZ* tutakaa ili tuweze kuona *to what extent* tunaisaidia sekta binafsi na Wazanzibari katika kukopa *PBZ.* Mimi naamini Wazanzibari hawatotaka kuiona PBZ inafilisika.

Jengine ni kuwawezesha wakaguzi wa ndani, hili nalo limezungumzwa na wengi sana. Mhe. Omar Ali Shehe umelizungumza, Mhe. Fatma Mbarouk umelizungumza, na leo Mhe. Marina Joel Thomas umelizungumza na wengi wamelizungumza. Nataka niseme hivi tunakuja na marekebisho ya sheria ya fedha, tunakuja na marekebisho ya sheria ya manunuzi. Katika sheria yetu hii mule ndani tumezungumzia kuhusu habari ya kuanzisha suala zima la utawala wa ukaguzi wa ndani. Kwa sababu ni mwaka 2011 tu hawa ndio tumewaandalia muono sio zamani sana. Huko nyuma naambiwa kwamba akimkera Katibu Mkuu mtu basi unaambiwa wewe ukae Mkaguzi wa ndani, ni mwaka 2011 ndio wametengenezewa ule utaratibu, hawa bado ni wachanga sasa hivi. Lakini tunakuja sisi na hiyo sheria, huko ndani tunaielekeza, na tutaiomba serikali ituruhusu, tutakuja hapa tuliombe Baraza, Baraza likiruhusu nasi tutaweza kukianzisha hiki kitengo chao.

Vile vile ulisema pale somo yangu sheria zetu za fedha na manunuzi zina mapungufu na wengine wamesema, nakiri na ndio maana tunakuja na marekebisho.

Mhe. Asaa Othman Hamad na wewe umeanza kusema kwamba hatujaitumia vizuri bahari. Hili nadhani nimelieleza na ukasema jambo moja kubwa sana, kwa sababu sikuwepo mimi kwa hivyo siwezi nikasema kwamba sio kweli au ni kweli, lakini nataka ni *trust* maneno ya Mhe. Asaa kwa sababu umezungumza ndani ya chombo hiki kikubwa. Benki Kuu kusema kwamba haiwezi kusimamia chumi mbili, wangekwenda zaidi wakatuambia kwa nini? Lakini nimesema basi na mimi nipate fursa ya kuonana na *Governor* angalau anielimishe hili, halafu niweze kulifahamu hasa kwa nini. Kwa sababu zipo nchi nyingi zimeungana na kiutamaduni na kiutaratibu benki zao zinasimamia

chumi zao. Lakini jibu la hili ni Katiba mpya, katiba mpya imependekeza kwamba Zanzibar watakuwa na *state bank* na Bara watakuwa na *state bank*, wamezipeleka hizo *function* za uchumi kwenye *state banks*, halafu yeye wamembakishia suala la *currency*. Kwa hivyo mkiyasoma yale marekebisho ya katiba mpya nadhani hii ndiyo *solution* yake.

Tozo la simu nimelizungumza Mhe. Asaa Othman. Tufanye tathmini ya miaka 50 nimeizungumza, mkongo wa taifa nitauleta mwisho.

Umeeleza kuhusu habari ya *ZIPA*, ng'ombe na kamba nimelieleza. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, wengi wamelieleza suala hili. Ni kweli kuna watu wanaweka pesa zao pale, michango yao, baadae wanapoteza ajira wanataka kwenda kuchukua pesa zao kule wanaambiwa *no* hamuwezi. Sheria tumeipitisha sisi hapa Barazani, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, sheria inasema kwamba ile ni *pension fund*, sio *provide fund* na *pension fund* maana yake nini. Maana yake ile pesa yako ya kuja kukusaidia uzeeni, na sisi hapa *voluntarily* ukitaka kujiita mzee basi ni kuanzia miaka 55 *voluntarily*, maana yake unaweza ukastaafu miaka *55 compulsory* miaka 60.

Lakini haya malalamiko tumeshayapata na sisi wenyewe tunajikita, tuipinde sheria tumpinde mtu. Ukimpinda mtu ni bora zaidi kuliko kuipinda sheria, maana yake mwisho wa siku huyu Mkurugenzi mtampandisha mahakamani, lakini nawaombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi tustahamili tunakuja na marekebisho. Marekebisho yataruhusu kumsaidia huyo aliyepoteza kazi, kwa kile kipindi anachohangaika kutafuta kazi basi mfuko utamsaidia, tutakuja na marekebisho hayo. Kwa hivyo, nakuombeni sana.

Kwa nini *TRA* kazi zake zisifanywe na *ZRB;* suala hili lilizungumzwa na Wajumbe wengi sana. Mwisho Mhe. Mwakilishi wa Mtambwe na yeye kaniuliza sababu, hasara, hasira yote kaniuliza hayo, hizi kazi katiba mpya nayo vile vile imeshaweka vizuri, kutakuwa hakuna tena *TRA* Zanzibar, katiba mpya hiyo sio mimi. Tukiipitisha Wazanzibari kutakuwa hakuna *TRA* Zanzibar, kwa sababu Serikali ya Muungano itakuwa ina pato lake, *source* yake moja, *ZRB* watakuwa ni wakala wa hiyo. Lakini Katiba sasa hivi inatutaka *TRA* iwepo kwa sababu ya kukusanya mapato ya Muungano, ukisema unataka kuiondoa sasa hivi basi mishahara yote wanayolipwa na *TRA* maana yake ilipwe na *SMZ*. Tusubirini katiba, katiba itatupa *solution*, wale wataondoka na pengine tunaweza tukavivunja vyote vyombo viwili tukaunda *very strong institution.*

Kuhusu *PBZ* itazame katika maeneo ya kilimo ili iweze kufungua matawi. Mimi nimefahamu sana, anazungumzia maeneo kama vile ya Rukwa, Mbeya na Iringa ambayo yanazalisha sana kufungua matawi kule. Tutaliangalia acha

tuanzishe na haya ambayo tunataka kuyafungua, halafu tutakuja kuangalia *analysis* zetu zinasemaje na huko tutakwenda.

Vile vile aliuliza kuhusu mfuko wa pamoja tunasubiri lini. Mhe. Asaa Othman ukiusoma huu mswada wa katiba mpya, mfuko wa pamoja umekufa haupo. Mimi nimeisoma na nakuombeni ndugu zangu Wawakilishi muisome, angalau ukipata siku soma japo *page* mbili tu, watu wasije huku wakaku-*take by surprise*. Ngoja niisome *joint finance commission* haiko tena katika katiba mpya, lakini kama yalivyoelezwa, Mhe. Hamza Hassan Juma umeeleza, Mhe. Asaa Othman umeyaeleza na Waheshimiwa Wajumbe wengine katika vipindi mbali mbali mmeyaeleza kwamba sisi Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa imeshamaliza kuipitia ripoti na tulikuwa tumeshaweka maoni yetu, tunasubiri na kule na wao wapitie yao watoe maoni yao.

Sasa mimi kama Waziri wa fedha niende nikamburure Waziri mwenzangu wa fedha kule katika kupeleka ripoti kwenye *cabinet*, nadhani nitakuwa nakwenda mbali. *Responsibility* yangu na maeneo yangu nimeshakamilisha, mimi nasubiri waniambie sasa tayari na kule tuzipeleke ripoti zetu.

Mhe. Fatma Mbarouk ulieleza mapungufu katika utekelezaji wa sheria nimeshalisema hilo, wahasibu wasimamiwe na kupatiwa elimu. Hili nalikubali kabisa pamoja na *rotation* hiyo. Ulieleza kuhusu kitengo cha ukaguzi wa ndani, ulieleza uwezo wa mfuko wa barabara wa kukusanya. Tatizo kubwa tulilonalo, sheria ya mfuko wa barabara *source* yake ya *revenue* ni moja tu; ni mafuta, na inakusanywa na Mfuko Mkuu kupitia ZRB, halafu zinarudishwa kama ni ruzuku. Pesa zote zinazokusanywa na serikali ukizipeleka kwenye taasisi, unatakiwa uzipeleke kama ni ruzuku. Kwa hivyo, tumezipeleka kule kama ni ruzuku.

Lakini sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu tunaweza tukavunja vichwa Mhe. Spika, tukasema hatuwezi tukawatafutia *source* nyengine, angalau mwaka huu tukajipanga vizuri tukazifikiria *source* nyengine, halafu tukasema kwamba hii nayo iwe ni *source* yao ya mapato, lakini natahadharisha *whatever the source* tutakayoitafuta, isije ikawa ni *source* ya kumkandamiza mwananchi wa kawaida. Kwa hivyo, inawezekana vile vile.

Pia ulizungumzia kuhusu wafanyakazi wanaoachishwa kwenye *ZSSF*, suala hili nimeshalizungumza.

Mhe. Hamza Hassan Juma umeeleza kwamba kuna watu wamefanyiwa tathmini kinyume cha mishahara yao na pencheni zao ziko tofauti. Unajua Mhe. Hamza Hassan Juma alifanya *analysis* nzuri kama wenzangu mulimsikiliza. Mimi nataka nirudie tu, alisema kama mshahara wangu mimi

ni shilingi 200,000 halafu nikafanyiwa *analysis* ya mafao ya shilingi 300,000 maana yake sio nitapata mafao makubwa tu ambayo yale nitapata mara moja niondoke, lakini mpaka pencheni nitaipata kubwa.

Kwa hivyo, *throughout my life time* nakula pencheni kubwa ambayo haikuwa haki yangu. Mdhibiti atafanya kazi hii, akimaliza tu kupitia mishahara, tumeshampa na kazi hii na kama ulivyo-*request* kwamba tumuwezeshe Mdhibiti. Tumeshamuezesha awamu ya kwanza na tutamuwezesha zaidi.

Zoezi la kusajili mali za serikali liharakishwe; ni tatizo la bajeti tu lakini wizara tano tumeshakamilisha, tumesajili mali na tathmini ya mali hizo na mwaka huu tunaanza na wizara tatu, tunasajili na tathmini, halafu tukimaliza mwakani tutakwenda na zile zilizokuwa zimebakia, inategemeana na hali ya bajeti tutakayowekewa. Lakini kweli ni lazima tuwe tuna-*register* na mali za serikali.

Tumesema Idara ya bajeti ipewe misaada; nimelieleza pia na Mwenyekiti naye kasema. Jengo letu, hapa ndipo Mhe. Hamza Hassan Juma uliponifurahisha. Jengo letu la ofisi la Pemba liko katika hali gani au linataka mshauri mwelekezi wa kulibomoa. Hili halihitaji mshauri mwelekezi, hili wala halirekebishiki, hili lazima tulibomowe, lakini sasa hivi tuko kwenye *arbitration* na taarifa ambazo tumezipata kwamba *ruling* itatolewa Novemba. Tukishapata *ruling* lile jengo halirekebishiki ni kulivunja tu, wala mimi sitaki kusema kwamba limeanza na Mwinyihaji nalikamata mimi, hapana, serikali ni endelevu.

Kuhusu *ZSSF* wamesema kuandaa utaratibu wa kuwajengea na kuwakopesha nyumba wanachama wao. Tayari ZSSF anazungumza na wenzake ambao wataweza kushirikiana katika ujenzi wa hizi nyumba. Lakini vile vile *ZSSF* anazungumza na *PBZ* kwa kutumia sheria ya *movement finance*, ili unaweza ukaenda kule ukakopa ukainunua ile nyumba na ukalipa kidogo kidogo. Nimezungumza na *PBZ* kiwango cha kulipa *minimum* miaka 15, utalipa kidogo kidogo kwa muda wa miaka 15. Mimi nimeipanga jana kama nitalipa shilingi 100,000 kwa mwezi basi kwa mwaka nina shilingi milioni 1.2 kwa miaka 10 nina shilingi milioni 12, kwa miaka 15 nina shilingi milioni 18. Hiyo ni rahisi tu utaweza kuona hesabu jinsi inavyokwenda yale malipo yako yatakavyokuwa yanaweza kuilipia hiyo nyumba, ukilipa shilingi 300,000 kwa mwezi basi miaka 15 una nyumba nzuri tu.

Vile vile umezungumzia *TRA* kwa nini Naibu Kamishna wa Zanzibar anaitwa Naibu Kamishna asipewe *full* Kamishna. Hili Mhe. Spika, nataka nikiri kwamba sina majibu, lakini nitakaa na wenzangu ili tuweze kuliona. Lakini

vile vile litakufa hili Katiba mpya itakapokuja, kwa sababu *TRA* atakuwa hayupo.

Kuhusu sera za kodi. Nimezieleza vile vile. Mfuko wa Barabara nimeueleza tayari. Kuhusu taasisi ya ujenzi wa barabara, ile taasisi yetu, Mfuko wa Barabara hauwezi ukainunulia vifaa. Lakini ndugu yangu Mhe. Marina Joel ametoa rai nzuri, amesema tuunde *agency*. Basi tutaliangalia suala hili na wenzangu tuweze kuona pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Mhe. Mwanasheria Mkuu, kama itaweza kukidhi haja.

Kuhusu wajasiriamali kutopatiwa pesa hizi za mikopo kutoka BOT. Taarifa ya kwanza nimeambiwa masharti yao, acha tupate *in writing* masharti yao ni yapi, halafu tuwatizame wajasiriamali wetu kama wanayaweza au hawayawezi, tutalifanyia kazi Mheshimiwa hili.

Vile vile umetaka wataalamu wetu waje wakufanyieni semina maeneo gani ya kiuchumi yabakie na yatoke katika Muungano, na umependekeza kabla hatujaondoka. Hili ni wazo zuri lakini tuondoke kwanza, kwa sababu hapa tuna skukuu. Leo mimi hapa natakiwa hii niimalize na nisome *appropriation bill*, tuna na skukuu hapa, acha tuondoke tutaandaa halafu tutakuja kufahamiana.

Kuhusu *one stop centre* nimeshauelezea. Huu mradi wa ujenzi wa *Air Strip* kama ulivyosema. Sasa hivi kwa mujibu wa mipango miji ya watu wa ardhi, wanasema kwamba iwekwe katika maeneo ya Kaskazini kwenye maeneo ya Nungwi. Tunawasubiri wenzetu wa ardhi watupatie hiyo ardhi, lakini Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wameshatoa *go ahead* hawana matatizo, na *ZIPA* wameshatoa *go ahead* hawana matatizo. Kwa hivyo, sasa hivi tushirikiane kufuatilia ardhi tu ili tumalize hili suala.

Vile vile umesema *ZIPA* wasijitangaze wakati wanakwenda na Rais tu. ZIPA wanajitangaza, lakini hili lilitokea kwamba wakati ule ilibidi wajitangaze vile vile.

Ulizungumzia kuhusu habari ya Cristal Hotel ya Paje. Hawa kwa taarifa zetu tulizonazo ni kwamba wameshawalipa, lakini Artlass Michamvi Maghembe hawa wanadaiwa shilingi milioni 16, tumemtafuta yule jamaa tumeshampata yuko nje, atakaporudi atakaa na sisi, na amekubali kwamba atafanya *settlement* hiyo ya shilingi milioni 16.

Kuhusu eneo huru kupimwa nimeshalisema. Tunguu iwekwe *ATM*. Wataiweka *ATM* haraka iwezekanavyo wameshapata *quotation* tayari. Tozo la simu nimeshalisema, *e-Government* nitaiweka mwisho, Visa nimeshalisema.

Mhe. Mohammed Haji Khalid umetaka tupange miradi kwa mujibu wa uwezo wetu. Ni wazo zuri na tume ya mipango tayari imeshakubali kwamba kui-*review* miradi ya mawizara yote, halafu tutakubaliane miradi ipi tutaiacha.

Vile vile umetutaka Mfuko wa Barabara usingoje mpaka barabara ikabomoka. Hili ndilo agizo, kwamba wao wanatakiwa kuitazama barabara, barabara ikishaanza kufanya mashimo wairekebishe. Lakini tutawakumbusha wenzetu.

Pia uliulizia suala la *ZSSF* nimeshalitolea maelezo na la mwisho ulisema skukuu iko karibu mishahara vipi. Leo tarehe 05/08/2013, skukuu tarehe 08/08/2013. Mhe. Spika, kiutaratibu hapa siwezi kusema kwamba nitatoa mishahara na wala Waziri wa utumishi sidhani kama atatoa hiyo mishahara, kwa sababu *system* yetu hairuhusu. Mimi nadhani tujivuteni tu hivi, basi tumuombe Mwenyezi Mungu tumalize salama Ramadhani yetu, tumalize salama na skukuu yetu na watoto wetu wafurahike vizuri.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, kuhusu suala la mashine ya kutengeneza risiti nimeshalieleza. Sheria nilizozitaja mwaka jana kwamba nitazifanyia marekebisho na mwaka huu nimezieleza na marekebisho yake yako tayari na nitazileta.

Umeuliza ni namna gani tumepanga ili kuwaondoshea umaskini wananchi wetu. Tumeunda hii wizara na tumewaongezea mtaji mfuko huu wa mikopo ya JK na AK. Tatizo letu Waheshimiwa Wawakilishi wananchi wetu ndani ya maeneo yetu, bado hawakuwa *aware* wengi wao, nini wafanye cha kuwaondoshea umaskini. Naomba sana tusaidiane kuwaelimisha kwa vikundi. Maana yake na mimi nilikuwa Mbunge katika Jimbo haya niliyaona, utakuja wewe na mawazo utasema tuanzishe hiki hakiendi mbali, na wakianza wenyewe hawajui waanze kipi. Mimi nadhani tuendelee kusaidiana halafu tutaona ni jinsi gani ya kuweza kusaidia.

Vile vile umetaka kujua misamaha ya kodi. Mwaka jana serikali ilitoa misamaha kwa wawekezaji pamoja na serikali yenyewe katika miradi yao shilingi bilioni 34, na mwaka huu unaokwisha shilingi bilioni 30. Namna gani tulitumie eneo la Nyamanzi maduka ya kuuzia magari yapelekwe huko. Hili nimeliacha kwa Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, maana sasa hivi ile ni biashara. Sasa mimi nikitoa hapa fat-wa nitakuwa namuonea Mhe. Nassor Mazrui. Mhe. Mazrui akishirikiana na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Waziri anayehusika na Tawala za mikoa wataangalia wao ni namna gani ya kuyahamisha haya maduka ya magari na kuyapeleka Nyamanzi, kwa sababu, Tawala za Mikoa, Waziri wa ardhi na Waziri wa biashara. Mimi nitakapokwenda kokote kule kazi yangu ni kutafuta kodi tu. Kwa hivyo, suala hili nadhani Mhe. Mazrui amelisikia na atalifanyia kazi.

Kuhusu magendo ya mafuta nimelizungumzia. Pia ulitaka kujua uwiano wa *paye*, wafanyakazi wanaofanya kazi wa Muungano walioko hapa kwa sababu ya kodi zao ni kubwa *paye* yao mpaka sasa hivi ni 21 bilioni na wa kwetu ni 18 na kidogo bilioni. Vile vile ulizungumzia suala la salio. Nadhani hili salio la bilioni 5 nililieleza, na tokea mwaka jana nimelieleza, unapoamka serikali ni lazima uwe na kitu kidogo, ukiamka kama huna kitu unaweza ukatokewa na mambo haya ikawa balaa. Kwa hivyo, hizi zimewekwa ili ziweze kuamkia katika bajeti mpya.

Kuhusu uhakiki wa mitaji ya umma, uliuliza kwamba yale mapato ya idara ya uhakiki mali ndio yale tu. Kwa idara ile ndio yale, lakini kwa idara zangu nyengine yapo mengine vile vile ambayo ukitizama kwenye kitabu cha mapato utayaona.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, karibu nitamaliza sasa hivi. Mhe. Jaku uliitaka Wizara ya Afya, kidogo umepata hamasa na mimi sistaajabu. Afya zetu jamani ni muhimu kuliko kitu chochote kile, ni lazima nikubali. Ndio maana muda wote Waziri wa Afya ananitaka tuonane mimi kama mimi, mimi kama Waziri wa fedha. Hata siku moja sijamwambia Waziri wa Afya leo niko *busy*, yule pale. Tena bahati nzuri yeye haogopi kama anavyoogopa Mhe. Ismail Jussa, hata usiku tunaonana yule. Kwa sababu afya zetu jamani ni muhimu.

Sasa nataka nikwambie kwamba wenzetu hawa hasa katika hospitali ya Mnazi Mmoja, wao wamesema kwamba wanahitajia shilingi milioni 30 kwa matumizi yao ya mwezi. Tukasema sawa. Tatizo lao wanasema zinakuwa zinachelewa. Tumejiwekea *time* sasa hivi isizidi tarehe 3 ya kila mwezi, ziwe zimeshatoka Hazina zimekwenda Wizara ya Afya na isizidi tarehe 5, iwe zimekwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Jaku Hashim tunafahamiana. Lakini tumewawekea na *impress* ya shilingi milioni 10. Maana yake shilingi milioni 30 wanatumia na kama kuna chochote kimetokea cha haraka na hizi za mwezi hawana, ndio watumie ile *impress* ya shilingi milioni 10. Kwa hivyo, kila mwezi kwa tafsiri ya haraka haraka watakuwa na mzunguko wa shilingi milioni 40. Hizi ni hesabu za wenzetu Wizara ya Afya na tumekubaliana, na tatizo la muda ndilo lililokuwa likiwasumbua, tumeshawekeana misingi, muda huu sasa uheshimiwe. Kwa hivyo, mimi nakubaliana na wewe kabisa hatupaswi kuchezea afya zetu. Mimi namuomba sana Mhe. Waziri atakapoona afya zetu zinachezewa chezewa basi tukae turekebishe, na hizi shilingi milioni 40 za mzunguko, ikifika pahala *population* inakua hazitoshi, tukae tena tu-*review*, maana yake sio *fix* tunasema tuta-*review*.

Kuhusu jengo la benki ya Mwanakwerekwe. Hata na mimi nakubaliana na wewe, pale lilipo vurugu tupu, ingawa tuna hamu ya kuweka mabenki karibu

na wananchi, lakini pale na benki yenyewe. Tumeshawaambia wenzetu wa benki, wenzetu wa jengo lile *ZSSF* waangalie utaratibu wa kuweza kulifanyia marekebisho.
Sifa ambazo mzanzibari anahitaji tayari nimeshazizungumza kuhusu habari ya kukopa. Mhe. Spika, njia yake Mhe. Mjumbe ya Jambiani kwa kuwa Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, basi nitampelekea hili, ili tuweze kulifanyia kazi pamoja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, yeye alikuwa na maelezo lakini mambo ya msingi hasa yalikuwa kama manne au matano na mimi nataka niyakusanye kwa pamoja. Jambo la kwanza ulitushtua kwamba kuna fedha zetu nyingi Tanzania kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba fedha za wafadhili ziko katika mafungu matatu; kwanza kuna kitu wanakiita *GBS*. *GBS* sisi ndio tunapata asilimia 4.5 na kwenye *calculation* zake Mhe. Mjumbe ametupa bilioni 52 na sisi tumeweka bilioni 40 na tumeweka hivyo kwa sababu, kwamba katika taarifa hii ambayo Mhe. Waziri hakuisoma kuna fedha ambazo zimekuwa *earmark* haziji Zanzibar.

Kwanza kuna fedha ambazo United Kingdom wamezi-*earmark education Mainland* shilingi bilioni 79.9. Vile vile kuna fedha ambazo zimetolewa na *European Commission Road Sector* ni bilioni 21.2, na hizi si kwa ajili ya barabara za Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna fedha ambazo zimetolewa na Canada *education* kwa ajili ya Bara bilioni 49.8. Pia kuna fedha zile alizozungumza za *energy* ni madeni ya *IPTL* bilioni 122 haziji Zanzibar, na ukijumuisha fedha zote hizo zinazokuja Zanzibar ni bilioni 40.48. Kwa hivyo, hesabu ambayo niliyonayo mimi na hesabu ambayo anayo Mhe. Mjumbe ni sahihi, lakini ulichonacho wewe umeingiza hizi fedha ambazo haziji Zanzibar, sasa ukizitoa hizi utapata bilioni 40 na hiyo ni ya kwanza.

Pili kuna fedha ambazo zinaitwa *Basket Fund*, fedha hizi kuna mradi ambao umetayarishwa pengine kwa pamoja kwa mfano *BEST* Zanzibar itapewa *according to activities* zake.

Tatu kuna fedha zinazoitwa *Project Fund*, fedha zinazokwenda *specific* kwenye miradi kwa mfano ile ya *MCC* Zanzibar ina miradi yake na itapewa fedha zake. Hata hivyo, Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wengine kwa jumla, tumeona ni vyema bado tukakaa zaidi na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano tukazi-*review* tena hizi tukaona wapi ambapo kuna fedha za ziada tunastahiki kupata, na tumeona ni bora tukakaa na kuzitizama

tena. Mhe. Spika, hilo tutalifanya mara baada ya kumaliza Sikukuu *inshaallah* tutakaa, ili tuweze kuzipitia na kama kuna pahala tunayo haki yetu mimi sidhani kama wataichukua, basi lazima haki ile tuweze kuipata.
Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe alisema kuna fedha ambazo zinazokusanywa na taasisi za muungano kama vile *TCRA*, *TCAA* na *TTCL*. Kwa bahati nzuri katika *level* ya Makatibu Wakuu wameshaandikiana zamani kuulizia hizi fedha zetu, bado hatujapata jibu, ndani ya wizara yetu tumeshazungumza na sasa itakuwa *level* ya Mawaziri na nitamuandikia barua Mhe. Waziri mwenzangu, ili nimuelezee kwa sababu muda umepita hivi sasa zaidi ya miezi sita hatujapata majibu.

Kwa hivyo, sasa itakuwa kazi yangu mimi kumuandikia Waziri mwenzangu kukumbushia barua iliyoandikwa na Katibu Mkuu, na kama mimi sijapata jibu basi nitapeleka kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na yeye anajua ngazi gani ya kuwasiliana nayo, na kila mmoja anayo ngazi yake. Mhe. Spika, mimi naamini kwamba tutafika pahala kama tulivyofikia kwenye *Paye* na haya mengine tutafikia.

Vile vile Mhe. Mjumbe kuna suala moja ambalo alitaka kulijua pia na hapa alitaka kunionea hapa. Mhe. Spika, hapa Mhe. Mwakilishi alipoona katika idara zangu zote kuna *hundred percent* katika *recurrent* na huku Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameshamwambia kwamba Wizara ya Afya hawana fedha hee! Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kunila.

Mhe. Spika, nataka niseme hivi tulikuwa na zoezi la meli, na hili nikwambieni na wala sikutaka kulisema kwa sababu umeliuliza basi itabidi nilitolee maelezo tu. Kwa kweli tulikuwa na zoezi la meli hapa na Mhe. Spika shahidi na tukasema tutakutana kwa kipindi cha miezi 12 taasisi zetu zote, na nikapewa orodha hapa na Mhe. Spika alikuwepo pale alipoichungulia akakuta na Baraza la Wawakilishi nayo ni bilioni 2 na alikunja macho kidogo, lakini baada ya kuangalia kwamba Baraza la Wawakilishi shughuli zake zilikuwa ni nzito kidogo na baadhi ya taasisi pia, tukasema aa! Taasisi hizi tusizikate na fedha zake tumezielekeza wapi, baadhi ya fedha tumezielekeza kwenye taasisi zangu.

Kwa hivyo, kwa mujiu wa bajeti taasisi zile lazima zionekane zimepata *one hundred*, lakini nime-*rescue activities* za Baraza na nikasema kule nitazikata zaidi na zipo taasisi nyengine. Kutokana na hali hiyo, ndio maana ukakuta kuna *one hundred* pale, lakini *otherwise* ukitizama vitabu vya nyuma *still* na mimi nina 60 au 65 na hiyo ndio hoja, tena nafikiri tumefanya kwa nia safi kabisa.

Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe alitaka pencheni tuzifanyie uhakiki tayari nimeshalieleza.

Mashirika na taasisi zinazojitegemea zilete bajeti zao na angalau kujua tu mapato yao, na nadhani hili ni wazo zuri, ndio maana na mimi nimeanza kwenye yale ya kwangu nimeanza kutoa taarifa.

Pia kuhusu deni la taifa. Mhe. Spika, deni la taifa siku zote anapelekewa *CAG* na wala hazuiliki kulikagua anaweza kwenda kulikagua, kwa sababu siku zote anapelekewa taarifa ya deni la taifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, yako mengine mawili nimeyaacha mwisho kabisa huko.

Mhe. Saleh Nassor Juma kuhusu tozo la simu tayari nimeshalielezea na leo hayupo pamoja na Mfuko wa Barabara.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali ametaka kodi ya mchanga. Mhe. Spika, hii sio kodi ya mchanga isipokuwa ni vibali vinavyotolewa na Idara ya Misitu na Mali asili zisizorejesheka na wala sisi hatuna kodi ya mchanga.

Ruzuku kwa *ZIPA* amesema ndogo tuwaongezee. Mhe. Spika, tumelipokea na tutalifanyia kazi na tutawaongezea.

Vile vile amezungumzia mashirika yaliyochangia milioni 400/= isipokuwa *PBZ* inachangia asilimia 15 ya faida na haya mengine tumeyawekea Bima, *ZSTC* na Bandari asilimia 10, lakini tutakuwa tuna-*monitor* faida zao zinavyokwenda, ili tuweze kufikia pahala pazuri.

Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka zile fedha ambazo wanazosaidia Chuo hicho tunaita *social responsibility*, kwa sababu na wao wana wajibu wa kusaidia jamii kwa kuwa wanayo mapato ambayo wanayakusanya, basi wanao wajibu wa kusaidia jamii ni shilingi milioni 8,000,000/= tu na wala sio fedha nyingi wanazitoa kutoka kwenye makusanyo yao.

Mhe. Marina Joel Thomas kuhusu suala la uwakala tayari nimeshalielezea pamoja na suala la wakaguzi pia nimelielezea.

Mhe. Ali Mzee Ali, yeye ameanza kwamba tufanye tathmini ya miaka 50. Mhe. Spika, nimeeleza wazo ni zuri na tutalifanya, nimefurahi aliposema kuhusu habari ya ununuzi wa meli na ujenzi wa *Terminal Building* zimeanzwa na awamu ya sita, awamu ya saba imepokea na inaendelea nayo. Kwa hivyo, ndio serikali endelevu na tunaendelea nayo na wala huwezi kusema kwamba

kitu hichi sikitaki kwa sababu kimeanzwa na awamu iliyopita, isipokuwa unaendelea nayo kwa manufaa ya nchi yetu na watu wetu.

Pia ameipongeza *PBZ* na tunakushukuru kwa pongezi, na ameielezea jinsi hali yake ilivyokuwa na ametaka mashirika yote yawe chini ya Hazina yaangaliwe na yasimamiwe. Mhe. Spika, hilo ndio jukumu lao na tutawakumbusha Idara ya Uhakiki Mali wasimamie na wayaangalie.

Mhe. Mjumbe, ameeleza kwamba matumizi yetu ni makubwa kuliko mapato. Mhe. Spika, kwa kweli hapa ndipo penye jukumu letu sote kwamba taasisi zetu zote pamoja na mihimili yote mitatu, ili tuweze kufanikisha suala hili na kazi kubwa mbele yetu ni kuongeza mapato. Mhe. Spika, nataka niahidi kwamba juhudi hizo nitazifanya, lakini na nyinyi nakuombeni muendelee kunisaidia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la ubadhirifu na wizi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tayari ameshasema na ile ndio ahadi aliyoipa Baraza hili. Kwa hivyo, mkubwa wangu ametoa ahadi na nadhani serikali nzima tutaisimamia.

Hata hivyo, namshukuru sana Mhe. Ali Mzee Ali kwamba amenipa jina la meli, kwamba meli iliyoondoka ilikuwa inaitwa MV. Mapinduzi na hii amependekeza iitwe Mapinduzi Daima. Mhe. Spika, kwa kweli jina zuri, tamu na mwanana, na mimi nitawaambia wenzangu serikalini iitwe Mapinduzi Daima. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika maelezo niliyopata kwa maandishi Mhe. Salim Abdalla Hamad ameniuliza vile vile deni la mkandarasi aliyejenga Ikulu ya Micheweni. Kwa kweli wakati mwengine Wizara ya Fedha ni jaa, lakini hili alikuwa aulizwe na Mhe. Waziri ambaye anayehusika na Ikulu ya Micheweni, lakini kwa sababu umeniuliza mimi na serikali ni ya pamoja basi nitakujibu.

Nimeomba ripoti pamoja na taarifa kamili niandaliwe niisome na halafu niitishe kikao cha wadau na huyu mkandarasi. Kwa bahati nzuri mkandarasi amekuja kuniona na nimezungumza naye na nimemwambia haya. Mhe. Spika, nataka nithibitishe mbele yako leo nimepokea asubuhi ripoti inayoelezea kadhia nzima; *copies* mbili na moja nitampa Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na *copy* ya pili nitaisoma mimi mwenyewe.

Kwa hivyo, nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba baada ya Sikukuu na mimi napenda nipumzike, basi nitaitisha kikao kwa ajili ya kulijadili suala hili. Mhe. Spika, kama mkandarasi huyu anayo haki basi haitapotea na hayo ndio maelekezo aliyonipa Mhe. Rais, na kama hana haki basi aelezwe

kwamba hana haki. Vile vile mkandarasi nimeshamwita na kuzungumza naye tena amewafiki kwa nia safi kabisa tena ameshukuru, na anasema tatizo lote hili kwa sababu sijaitwa na leo umeniita, basi nimefurahi na mimi nitakuwa *clean heart* na serikali yangu na tutamwita.

Mhe. Spika, nimesema sana kwa sababu leo nilitaka *style* ile ya ujumla niibadilishe, isipokuwa leo nataka nipitie mmoja baada ya mmoja. Lakini wa mwisho kabisa na nataka nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Mbarouk Wadi Mussa yeye ameniletea kwa maandishi na ya kwake imepigwa chapa. *(Makofi)*

Kwa kweli amenipa pongezi nyingi pamoja na watendaji wangu tena amewataja kwa majina mmoja baada ya mmoja na mwisho akaunga mkono kwa asilimia mia moja. Lakini amesema tukitaka utawala bora, basi lazima kitengo cha ukaguzi wa ndani kijitegemee wenyewe. Mhe. Spika, nasema yote haya nitayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nimalizie mawili ya mwisho sasa. Suala la *E-Government*; kweli *E-Government* ndio tumeizindua, maana yake ni kwamba ndio mkandarasi amemaliza kazi na *application* yake bado. Kwa hivyo, *application* yake itaanza baada ya kukamilika kwa kazi ambazo tumekatibiana na *ZANTEL*. *ZANTEL* tumempa kazi ya kuunganisha taasisi zote pamoja na vituo vyote vya *television* na *radio* na hatimaye kuweza kuifanyia kazi kibiashara mkongo wa taifa.

Mhe. Spika, mkongo huu *capacity* yake ni 40 *GB* na sisi serikalini tutatumia *hardly* 2 *GB*, na 38 tumemtaka *ZANTEL* azifanyie biashara ili ziweze kutupatia mapato. Kwa kweli tumeweka hapa na kwa bahati mbaya kwamba tumechelewa tu kuanza ile shughuli na *ZANTEL*, lakini sasa hatua tuliyofikia inaonekana kwamba tunaendelea kukamilisha na wakati wowote *ZANTEL* itaanza kuziunganisha taasisi zetu, ili tuweze kuutumia mkonge wa taifa, tutatumia simu bure. (*Makofi*)

Kwa mfano, leo ukichukua Mhe. Spika, tathmini ya simu tunazotumia wakati tunapowasiliana wizara na wizara au taasisi sijafanya mahesabu lakini *it's a lot of millions*. Kwa hivyo, kwa kutumia huu mkongo tutamia simu bure, *internet* bure ndani ya serikali, lakini *ZANTEL* itafanya biashara na halafu atakuwa anatupa fedha na itakuwa *internet* iko *very faster*.

Mkongo huu umegawika katika sehemu mbili kubwa. Sehemu ya kwanza miundombinu ambapo *Chief Secretary* ameshatoa barua na miundombinu sasa itasimamiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Sehemu ya pili ni *application within the government machineries* ambapo *Chief Secretary* ameshatoa barua na wala hakutoa jana au juzi, hivyo *application within the government* itasimamiwa na Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Hazina nitaingia kama ni *share holder* tu katika mkataba wangu na *ZANTEL*. Kwa hivyo, fedha zitakazopatikana kutoka *ZANTEL* nitaletewa mimi na nitaingiza kwenye bajeti ya serikali.

Mhe. Spika, lilikuja swali kwamba kulikuwa na ubadhirifu wa fedha katika mradi huu. Kwa kweli huu ni mradi wa kwanza Zanzibar ambao umetumia *Exim Bank of China* mkopo huu ni wa kwanza. Mhe. Spika, nataka nieleze ili Waheshimiwa Wajumbe mutufahamu utaratibu wa mkopo wa *Exim Bank of China*.

Kwanza munatengeneza *feasibility study* munaipeleka China na *Exim Bank of China* wanaleta wataalamu wao, kwamba yale yote uliyoyazungumza pamoja na *cost* zako wanafanya *assessment*.

Mtaalamu alikuja na akapitia moja baada ya moja na akafanya *assessment* na huu mradi kama nilivyosema kulikuwa na kampuni mbili mwanzo *HUAWEI* ametaka dola milioni 36 na *ZTE* ametaka dola 33 na ukapunguzwa *scope* ndio tukafikia dola milioni 20.

Utaratibu ni kwamba mkandarasi anapomaliza kujenga kwa mujibu wa awamu muliyokubaliana, basi analeta *certificate* yake kwenu serikalini, na *certificate* yake ni karatasi kama *size* ya A4 kwa ajili ya kueleza kazi hii nimeshafanya na hii nimeshafanya na unafanya *reference* kule kwenye *document* kwamba kila kazi ina kiasi gani.
Kwa hiyo, nyinyi kazi yenu kuangalia kwamba kazi ile imefanyika na baadaye munazipeleka Wizara ya Fedha Muungano na wao wanazi-*foward bank*, na benki inathibitisha na baadaye fedha zinaingia kwenye *account* ya mkandarasi na wala haziingii kwenye *account* ya serikali. Mhe. Spika, ninaposikia kwamba hapa kuna ubadhirifu sijui, lakini *procedure* ya fedha zinaingia kwenye *account* ya mkandarasi na wala haziingii kwenye *account* ya serikali na wenzangu wametaka.

Kwa maana hiyo, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na wengine wametaka mchanganuo wa bajeti ambao huu hapa na ipo hapa dola milioni 20 zilivyotumiwa na wakandarasi kwa mujibu wa mkataba na makubaliano ipo hapa kama hivi ifuatavyo:-

1. *Transmission Equipment;* dola milioni 4,790,000;
2. *Communication Software System;* dola milioni 2*;*

3. *Optic Fibre* dola 658,000;
4. *Microwave and Support Equipment;* dola milioni 1,350,000;
5. *Engineering and Service for Equipment including civil work;* dola milioni *10,200,000;*
6. *Training;* dola milioni *50,000,000;*
7. *Transformer Generator Security System dollar 686,000;*
8. *Freight and Insurance* dola *218,000.*

Mhe. Spika, ukizijumlisha hapa unapata hiyo dola milioni 20,000,000.

Sasa mimi ninachokisema ni kwamba namshukuru sana Mhe. Marina Joel Thomas kwamba bado kazi hazijaanza. Mhe. Spika, tuitake hii idara na Mhe. Rais amemchagua Mkurugenzi basi waanze kazi kwa kushirikiana na *ZANTEL,* na kama kuna tatizo lolote Mhe. Spika *CAG* anaruhusiwa kwenda kuikagua hii na aende *CAG* akakague na baadaye alete ripoti yake hapa kama kuna mtu amekula, basi atwambie kala nani na sehemu gani zimeliwa na kiasi gani? *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, kwamba mimi nina uchungu na fedha za wananchi kama mulivyo nyinyi. Mhe. Spika, nimeingia hapa kabla Mhe. Rais hajanitangaza, kaangalieni picha yangu wakati Mhe. Rais ananiapisha, kaangalieni picha yangu sikuwa na ndevu nyeupe mimi na leo ndevu zote zimekuwa nyeupe kwa kazi ya kutafuta mapato. *(Makofi)*

Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe, niko pamoja na nyinyi, lakini nataka niseme kwamba hali ya mradi wetu ni ya matumaini makubwa na leo hatuwezi tukaiona. Mhe. Spika, ukishakuanza *gradually* mtaanza kuona na tutaripoti kila mwaka hapa *E-Government* inaingiza kiasi gani. Vile vile mkongo huu ndio tunataka tuunganishe na *E-Tax, E-Health,* baadaye *E-Education, E-Justice, E-Services* na kote huko mnakuja kuona *how much* tunaweza kutengeneza na tunaweza tuka-*save,* kwa hivyo mimi nakuombeni sana.

Mhe. Spika, katika ripoti ya mwaka jana aliyoisoma Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* alisema *CAG* hana ruhusa ya kwenda kuikagua miradi inayofadhiliwa, nilijibu anayo ruhusa hiyo na aende akakague huu.

Mhe. Asaa Othman Hamad alitaka kujua kwa nini tumejenga karibu na barabara hauna athari. Kwa kweli hauna athari yoyote kwa sababu ile ndio *road reserve* ya nchi na pale ndio ardhi ya nchi unaweza ukaujenga, nje huko kwenye ardhi mtu ndio ukapata hasara zaidi. Lakini huu mkongo umejengwa kila mita mia tatu kuna tundu, kwa hiyo hata ile barabara ukiifukia

ukiharibika basi unauvuta tu kwa kupitia ile, wako wenzetu wanaujenga katikati ya barabara, ili kuuwekea uimara zaidi.

Mhe. Spika, ule mkonge wengine wameuliza kwa nini haukuvishwa nguo, katika maeneo mengi umezikwa na nguo. Lakini unavyouona ule mkonge kile chuma kilichopo juu ndio *protection* na ndani kuna kama unywele umo ndani, yaani ni *glass* na ule ndio mkonge umefichwa, ndani kuna *layers* nyingi umeuficha ule. Mhe. Spika, mkonge wetu uko salama na inapotokea tatizo lolote unaweza kutolewa ile mita au mita zile zilizoharibika zinarekebishwa. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu wanazungumzia *frequence* moja wanafahamiana hawa. Kwa hivyo, Mhe. Spika nawaomba Waheshimiwa Wajumbe sana *with due respect* tupeni muda tufanye kazi na mkongo wa taifa, na kama gharama hizi munaona zimechakachuliwa basi *CAG* aende na baadaye aje atupe ripoti nzuri. Nadhani turuhusu mkonge wa taifa ufanye kazi na *ZANTEL* hivi sasa tayari wameshapanga *plan of work* wakishirikiana na timu yetu, kwa ajili ya kuweza kukamilisha ile hatua ya awali.

Lakini la mwisho Mhe. Spika *ZANTEL*. Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliyoyazungumza kuhusu *ZANTEL* yote nimeyasikia. Kwa hivyo, nataka nikuhakikishie mimi na wewe pamoja na wenzetu wengine wenye *interest* za Zanzibar tunaipenda sana *ZANTEL*. Mhe. Spika, hakuna mzanzibari ambaye hana *sim card* ya *ZANTEL,* au niseme *majority* tunazo *sim card* za *ZANTEL* na wala *ZANTEL* haitauzwa. *(Makofi)*

Kwa kweli serikali ina *share* asilimia 18 na ukitaka kuiuza *ZANTEL* maana yake na serikali yenyewe ikubali, kwa sababu ni *share holder unless* ukisema kwamba una-*declare* kama *ZANTEL* imefilisika, kwa sababu unaniambiaje kuhusu *share* zangu. Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Mjumbe kwamba yote ambayo ameyazungumza mimi nayafahamu, Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Mhe. Rais anayafahamu, tunayafanyia kazi kwa ukaribu zaidi. Nataka nikuhakikishie kwamba tupe muda ili Zantel tuweze kufanya kazi nayo kwa karibu zaidi.

Naambiwa tutaifanyia kazi, lakini nataka nikuhakikishie kwamba Zantel haitouzwa. Licha ya kwamba matatizo waliyonayo Zantel, matatizo yanaweza yakarekebishika, sisi kama serikali tusaidiane na Zantel, tuweze kurekebisha matatizo yaliyopo na tutafanikisha. Tuombe Mungu haya ambayo mengine umetaka niyaeleze nakuomba sana nisiyaeleze kwa sababu Zantel anafanya biashara, nikiyaeleza hapa na washindani wenziwe wengi kibiashara,

nitamuumiza sana Zantel nikiyaeleza. Mashirika mengi ya simu na huwezi ukali *expose* shirika kibiashara.

Nataka nikwambie tu kwamba sote tuna *sympathy* na Zantel, sote Wazanzibari tunataka Zantel i- *exist* Zanzibar. Nakuomba sana kama kuna mengine unahitaji ya kibiashara mimi na wewe Mhe. Ismail Jussa, ingawa nakukaribisha sana tuje kuongea wakati wa Ramadhani usiku hutaki, basi hata mchana tutaongea. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba Mkonge wa Taifa hauhitaji kuhamishwa, pale ulipo ndio umeshakaa. Barabara zinaweza zikapanuliwa wala hakuna matatizo yoyote. Mkandarasi, na watu wa Mkonge kile kitengo chetu au Kamati yetu ya Wataalamu wanatakiwa wamfahamishe Mkandarasi wapi tumeweka ile *hole* ya kuvutia Mkonge, ile *hole* hatakiwi kuiziba kwa lami, anatakiwa aiweke wazi, tutaweka *plate* pale kuonesha zile *hole* kama kuna Mkonge wa Taifa. Hata nchi za watu nyengine mkisafiri ziangalieni barabara kuna *hole* vile vile. Zile kuna Mkonge wa Taifa ule ndani. Kwa hivyo Mkonge wa Taifa hauhamishwi hapo ulipo ndio umeshafika na uko katika maeneo mazuri katika maeneo ya jiwe tumepata kazi kubwa sana lakini tumeweka vizuri wala msiwe na mashaka. Tunao wataalamu wazuri sana katika suala hili.

Mhe. Spika, leo sikutaka niseme sana lakini kutokana na hali nimelazimika kidogo kusema ili kila mmoja niweze kumtolea ufafanuzi yale masuala ambayo ameniuliza. Ni matumaini yangu basi buti leo zitakuwa hakuna, ili muniruhusu baadaye niweze kusoma *Appropriation Bill*. Tuna kazi mbili hapa leo, tupitishe Bajeti hii halafu nisome Mswada ili turuhusu pesa zetu tuanze kuzitumia.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba sasa kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana tunakushukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Nchi,(OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka 2013/2014 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 19 - OFISI YA RAIS FEDHA UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

Kifungu 0202	Idara ya Kodi za Ndani (TRA)	49,107,238,000
Kifungu 0203	Idara ya Forodha (TRA)	98,792,762,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	5,425,993,000
Kifungu 0701	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitakuwa sitendi haki kama sikumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo kwa maelezo yake ya kina juu ya zile hoja ambazo niliziuliza.

Baada ya kumpongeza na kumshukuru Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nazungumzia zaidi kuna fungu hapo linalohusu misaada kutoka nje, *current grants from foreign government*, misaada ya kibajeti, *general budgets sort*, ambacho ni kifungu 131101. Nimesimamia hapa Mhe. Mwenyekiti ingawa yale nitakayoeleza yanahusu zaidi ya GBS. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri, kwamba leo kawa wazi katika hili na ule mfano wake aliokuwa akiutoa ule wa mkonga nafikiri ni mfano mzuri kwa jinsi alivyokuwa wazi leo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya uwazi wake ndio maana mimi hutaka tuonane mchana, tusionane usiku kwa sababu najua haogopi kitu hata akataka tuonane kiza usiku. Ata mchana tunaweza tukawa wazi na mambo yetu tukayafanya kwa uzuri kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimezungumzia mapato ya maeneo matatu ambayo tulipaswa tuyapate kutoka kwa ndugu zetu wa damu, lakini hizi si zao ndugu zetu wa damu. Maana wamezowea kutudhalilisha na kutufanya kama vile sisi tunakwenda kuomba hisani pale. Hizi ni fedha ambazo zinatoka nje ambazo zinakuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, niliuliza kama kulikuwa na mafungu matatu, ambayo bahati nzuri Mhe. Waziri kayafafanua vizuri sana suala la misaada ya kibajeti, misaada na mikopo katika miradi ya maendeleo, halafu kuna misada ya mifuko ya kisekta. Sasa leo sitaki kurejea hesabu hapa kwa sababu nilisema jana.

Lakini katika majibu yake Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kasema kwamba katika lile fungu la misaada ya kibajeti (GBS) hatukuweza kupata bilioni 52 ambazo nilizifanyia hesabu mimi, kwa sababu kuna maeneo ambayo ameyataja ambayo yanakwenda katika maeneo mahsusi. Akataja kwa mfano Uingereza imetoa bilioni 79.9 kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya Tanganyika. Lakini akasema EU, imetoa fedha shilingi bilioni 21.2 kwa ajili ya Sekta ya Barabara. Mfano mwengine akatupa wa Canada wa bilioni 49.8 kwenda katika elimu. Baadaye bilioni 122, zimekwenda katika sekta ya nishati.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nimepata matatizo kwa sababu sekta hizi zote na Zanzibar zipo. Sasa kama kuna fungu limetolewa. Mimi ufahamu wangu GBS ni zile fedha ambazo zimeamua kusaidiwa bajeti ili serikali yenyewe iamue vipaumbele vyake. Sasa kwa nini hizi zikatwe kwamba ziwe kwa ajili ya Tanganyika tu**,** Wazanzibari wawe hawana haki katika hili, matokeo yake inatukosesha bilioni 12.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hoja yangu; katwambia kwamba katika mfuko wa vikapu kwa maana ya (*basket fund)* misaada imetolewa kulingana na miradi, akamalizia akasema katika *project fund* vile Zanzibar ina *project* zake. Mhe. Mwenyekiti, nataka anisaidie suala moja tu hapa. Kwamba hata haya maeneo ya *basket* yanayosimamia maeneo ambayo siyo ya Muungano, lakini inapokwenda kuombwa zinaombwa kwa ajili ya Jamhuri ya Muungano na vile vile katika miradi.

Nashukuru baada ya maelezo yake aliyokuwa katupa bado kasema kwamba atakwenda kukaa na wenzake, lakini Mhe. Mwenyekiti, haya mazungumzo ndiyo yamechukua miaka 50 na kuundwa kamati tele na kero za muungano hazishi na chini ya mfumo huo hazitokwisha mpaka Kiama. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka katika hili anisaidie yeye au kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza hili la Wawakilishi anambie kwamba tunafanya nini kusimamia fedha hizi kuja fungu letu Zanzibar.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tunaweza kuchukua mazungumzo yakamaliza mwaka huu wa fedha zikawa zimepotea hizi, kama ile *PAYE* ya mwaka jana ikawa hatukulipwa tukaambiwa kwamba inaanza mwaka huu. Kwa hivyo kila

siku fedha zinapotea halafu hazihesabiwi katika mapato yetu wao wanahesabu madeni.

Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri anisaidie hili, kwamba serikali zaidi ya mazungumzo ambayo hayeshi imepanga hatua gani. Kama yeye hana jibu basi namuomba Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza anijibu, serikali imepanga hatua gani kulinda haki za Zanzibar na kuhakikisha zinarejeshwa katika Hazina ya Zanzibar ili zichangie kama inavyochangia kuendesha mambo yao Tanganyika, kila siku wanajenga nchi yao na Wazanzibari tunahitaji kujenga nchi yetu chini ya mfumo ambao tumekubaliana kwa pamoja kuwa mambo haya yanaendeshwa katika jina la Muungano. Nataka maelezo zaidi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Ismail Jussa, sekta ambazo zimechangiwa Bara tu peke yake na Zanzibar zipo. Kama nilivyoeleza kwamba bado suala hili tutalifuatilia na kuna njia mbili za kulifuatilia. Njia ya kwanza ni kufanya mazungumzo na wenzetu Tanzania Bara, Wizara ya Hazina lakini njia ya pili vile vile ni kufanya mazungumzo na watoaji wa fedha hizi ili tuweze kujua kama fedha hizi zimeombewa kwa ajili ya barabara ya Chalinze, Kilosa basi. Lakini kama zimeombewa kwa ajili ya barabara tu hakuna mchanganuo wa barabara za aina gani, pale tutastahiki na sisi kuweza kupata angalau sehemu ya fedha hizo.

Kwa hivyo mimi namtoa wasi wasi Mhe. Ismail Jussa kwamba bado atupe nafasi na mimi naamini tutalifanyia kazi na tutaweza kupata *solution* na hizi pesa kama za kwetu zipo basi tutaweza kuingia. Hata ukitizama katika utoaji wake hizi pesa, ukitizama hizi kutoka UK za Elimu zinatakiwa zitoke katika mwezi wa Julai. Bado tunaweza tukazifuatilia na hizi za *EEC Road Sectors* zinatakiwa zitoke Septemba, bado hizi pesa hazijatoka, kwa hivyo bado tunao muda wa kufanya nao kazi na wenzetu *at least* na sisi tuweze kuona tunafanya kiasi gani kuweza kufanikisha hayo. Namuomba sana avute subra tutalifanyia kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru tena Mhe. Waziri ingelikuwa suala hili ni la Ismail Jussa ningevuta subra sana. Lakini hili suala ni la Wazanzibari ambao wamechoka na wamechoshwa Mhe. Mwenyekiti, kwa miaka 50 ya kusubiri na utatuzi wa kero za Muungano zisizokuwa na mwisho chini ya mfumo huu wa serikali mbili kuelekea moja.

Mhe. Mwenyekiti, katika aliyoyazungumza, nitoe mfano mdogo halafu nifunge hoja yangu. Juzi tumesoma katika vyombo vya habari kwamba kumesainiwa msaada uliotolewa na *World Bank* wa dola 93 milioni kwa ajili

ya kujenga barabara kwa upande wa Jamhuri ya Muungano, lakini najua itaishia Bara. Jana pia nilitoa mfano wa mkopo wa *World Bank* wa 196.5 *millions* kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Gesi na Nishati, ambayo mpaka sasa hivi naambiwa ya Muungano lakini inatumika kuendeshea Bara Zanzibari haipati kitu. Ipo mifano mingi sana.

Sasa mimi niwambie Wazanzibari kwamba wakati wa kufanya maamuzi ni sasa, tukikosea kufanya maamuzi tumekwisha. Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti hili nimuombe rafiki yangu Mhe. Waziri, mwaka juzi na wewe ukiwa shahidi nilileta hoja, halafu nikaleta suala na Mhe. Waziri akakubali, haya mengine haya ni yetu sisi wenyewe ya kujitakia. Mhe. Mwenyekiti, haya mengine wanatumia jina la Jamhuri ya Muungano katika vile vikao vya *Consultant Group Meeting* (CG) wakapeleka maombi yao ya misaada ya kisekta wakapata wakatumia wao, miaka 59 Tanganyika inajinufaisha kwa jina la Muungano, Zanzibar inaangamia.

Nikamwambia hapa nimezungumza na baadhi ya nchi wafadhili wapo tayari tuwe na *Consultant Group Meeting* ya Zanzibar peke yake. Aliniahidi mwaka juzi Mhe. Waziri kwamba matayarisho yapo. Kwa sababu nilifika mpaka kumpa *content* ya namna ya kuwasiliana nao kama nilivyokuwa nikizungumza nao miye, akaniahidi na imo katika *hansard* Mhe. Mwenyeki, kwamba kuanzia mwezi wa Oktoba mwaka juzi 2011, tungeanza kuwa na *CG Meeting* ya kwanza kwa ajili ya Zanzibar ili mambo kama haya tukapeleka miradi yetu na sisi tukapata misaada.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimuombe basi Serikali ya awamu ya saba Wazanzibari wanailaumu sana, kwa maneno mengi vitendo kidogo. Tofauti na serikali zilizotangulia. Niombe sasa hili ambalo aliliahidi na likabakia katika *hansard*, walifanyie kazi isije Wazanzibari wakaihukumu vibaya serikali hii mwaka 2015. Mhe. Mwenyekiti naomba sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaendelea kusema kwamba Ismail Jussa ni mpenzi wangu nampenda sana. Rafiki yangu sana, na yote ambayo anayonishauri sio kwamba siyafanyii kazi. Nayafanyia kazi sana. Hata hili ambalo amelizungumza sasa hivi tayari nimeshaandaa *document* kwa sekta zote ambazo zinahitajiwa kusaidiwa na wafadhili na tayari nimeshaziwasilisha huko ambako alikonambia yeye niziwasilishe siko tulikotakiwa tuziwasilishe, nimeshaziwasilisha. Kumeandaliwa Kamati ya wataalamu ambao watashirikiana na Wataalamu wetu wa ndani ili kutengeneza *acceptable paper* kwa ajili ya kupata fedha.

Namuomba tu juzi na mimi nilifanya mazungumzo hayo na wahusika. Namuomba kwa sababu sitaki kuyafafanua zaidi ni nani, lakini sasa yameshakabidhiwa, nimeshawakabidhi, avute subra kidogo atakuja kusikia na hao wafadhili wote wataalikwa. Na kama huo mkutano wa wafadhili utafanyika Zanzibar na yeye atauona na pengine na yeye ataalikwa.

Kwa sababu siku hizi Mhe. Mwenyekiti, mikutano ya wafadhili katika kuchangisha inaweza ikafanyika nje ya nchi yenu. Juzi ulifanyika kuichangia Somalia ulifanyika London, wa Msumbiji kuichangia ulifanyika Lisbon, kwa hivyo na sisi unaweza ukaambiwa utafanyika nje, lakini atapata habari. Sasa hivi nataka nimuhakikishie kwenye wizara yangu ile kazi sasa hivi imeshaondoka nimeshawakabidhi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mifumo anayoieleza Mhe. Waziri na mimi naifahamu, lakini akilitizama mara nyingi linalofanyika nje ya nchi zamani ilikuwa kuna kitu kinaitwa *Paris Club* ikifanyika yote nje, lakini baadaye wakaamua kwamba inafanyika ndani ya nchi ili kuonesha kumiliki na uhodhi wa maamuzi kwamba yapo kwa wananchi wenyewe kupitia kwa watunga Sera na watunga Sheria, sitaki niingie huko.

Ninachotaka kumwambia Mhe. Mwenyekiti, halafu niruhusu tuendelee ni kwamba hili suala, Serikali ya awamu ya sita hili ilishalifanyia kazi na ukafanyika mkutano mmoja hapa kwa sababu ya uongozi jasiri, kujiamini na ukereketwa na uzalendo wake Mhe. Dokta Amani Abeid Amani Karume akiwa Rais wakati huo.

Kikao kilifanyika Bwawani nafikiri wanakumbuka kina Mhe. Hamza Hassan Juma na wakati ule hakuna Umoja wa Kitaifa. Lakini kwa sababu ya kujali misingi ya utu na kufanya kazi kwa pamoja. Nakumbuka mimi nikiwa mfanyakazi katika Ofisi ya Makao Makuu ya CUF tuliletewa barua kutoka Ofisi ya Rais Fedha, Dokta Mwinyihaji atakuwa anakumbuka tukatakiwa Chama cha Wananchi CUF tupeleke wataalamu wetu wakashiriki katika kila sekta katika *cluster* zote kabla ya Umoja wa Kitaifa, na tukafanya mimi nikafanya mafanikio makubwa. Tatizo letu tunashindwa kuendeleza.

Kwa hivyo naiambia tena Serikali ya Awamu ya Saba, kwamba na Wazanzibari wanaitizama, wanaipima. Moja wanalolipimia sana ni uthabiti wao na umakini wao na uzalendo wao katika kuisimamia Zanzibar kwamba je, tunaweza kuisimamia Zanzibar kama alivyokuwa Komandoo Dokta Salmin Amour, kama alivyokuwa Dokta Amani Karume. Au katika hili tuna woga na tunatafunatafuna maneno katika kusimamia haki za Zanzibar baada ya kupiga kura, tukayasimamia maslahi yao.

Kwa hivyo nasema Mheshimiwa nimemsikia Mhe. Waziri huko nyuma ameniahidi sikuliona leo nalipokea tena, mwakani tukijaaliwa si mkubwa tutarudi tena hapa. Naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0701	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	101,047,000,000
Kifungu 1301	Idara ya Uhakiki mali na Mitaji ya Umma	558,760,000
Kifungu 1801	Bodi ya Mapato (ZRB) Tawi la Pemba	7,747,411,000
Kifungu 2203	Bodi ya Mapato ZRB Afisi Kuu Zanzibar	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ninachozungumza hapa nazungumza kwa nia njema kabisa ya kutetea maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Zanzibar yake. Mheshimiwa jana nilichangia kwa mdomo hapa nilimwambia Mhe. Waziri hivi sasa mafuta Tanzania Bara rahisi kuliko hapa kwa tofauti ya karibu sh 150/-.

Watendaji wetu wa ZRB kutokana na umakini wao na kwa uhodari wamekuwa wakivamia vyombo kwa kuangalia mafuta kwa nia njema kabisa wala sio kwa nia mbaya. Nataka anihakikishie tu Mhe. Waziri Je, ni makosa kununua mafuta Tanganyika kwa kutumia chombo chako? basi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaomba sana ndugu zangu wafanyabiashara wanaofanya biashara Zanzibar wasome sheria za Zanzibar.

Sheria ya Zanzibar inasema kwamba vyombo vyovyote vya usafiri baharini vilivyosajiliwa Zanzibar vinatakiwa vitiwe mafuta Zanzibar, vyombo vyote; hiyo ndiyo sheria inavyosema. Uzuri ukatia mafuta Zanzibar, kwa sababu wanaweza wakaja *auditor* wa ZRB wakakukagua, watakwambia tupe risiti zako ulizotia mafuta Zanzibar. Ikiwa huna wanaangalia *capacity* ya chombo chako halafu wanakupiga kodi.

Bora utie mafuta Zanzibar kwa mujibu wa sheria, lakini unaweza ukaenda Dar-es-Salaam, mafuta yale ukawa umetia Zanzibar, ukafika Dar-es-Salaam na abiria wako au na shughuli zako ukamaliza. Chombo unataka kurudi nacho kikapata athari, katika kupata athari ukakitengeneza na huku unakifanyia majaribio, ukikifanyia majaribio maana yake mafuta unayala, ukapungukiwa na mafuta, ukatia mafuta Dar-Es-Salaam kwa sababu hizo zinakubalika.

Lakini kwa sababu nyengine yoyote ile sheria inataka vyombo vyote tulivyovisajili Zanzibar vitie mafuta Zanzibar. Kwa hivyo si kosa kutia mafuta Tanzania Bara kama uko katika misingi hiyo niliyoieleza. Chombo chako kimekuharibikia, yale uliyokuwa nayo kwenye hakiba umeyatumia kwenye majaribio, sasa unajaliza ili uje zako Zanzibar. Lakini kama chombo kizima

hutii mafuta Zanzibar unatia mafuta Tanzania Bara kwa vyombo vilivyosajiliwa baharini ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa aliyonijibu Mhe. Waziri hebu anieleze kwa nini mafuta Dar-es-Salaam au Tanganyika yawe rahisi zaidi kuliko hapa Zanzibar ambako ni watu kidogo sisi, haoni hii amri anayoitumia ni ya kijeshi, hivi sasa na wananchi wetu watazidi kuumia kutokana na hali ya maisha inavyokwenda hivi sasa. Na faida ya Muungano ndio huu, kuwa nao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama hivi ifuatavyo, zipo sababu mbili tu na hizi nina imani kubwa sana zitaondoka kama Waheshimiwa hawa watakubaliana na mawazo ambayo sisi tunakuja nayo.

Leo waingizaji mafuta Zanzibar ni wengi kila mmoja ataingiza tani mbili, tani tatu, ile *cost* ya kuleta ni kubwa. Wenzetu Bara wanaingiza mafuta *in bulk*, meli moja kubwa inaleta mafuta huku ndani ndio kuna mnyumburuo kila mmoja anayataka yake, wewe lita ngapi umeagiza, 10, chukua 10, wewe lita ngapi, 30, haya chukua 30 hilo ni moja. Kama hatukwenda katika *bulk procurement* hivi tunavyokwenda mafuta Zanzibar itakuwa kidogo ni ghali.

Lakini hili analolizungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akumbuke kwamba kuanzia mwaka huu tarehe 01/07/2013 *Road License* tumeiondoa na imo ndani ya mafuta. Kwa hivyo hizo anazozizungumza kwamba ni ghali mle ndani kuna *road license* vile vile. Sawa shilingi 30 na hiyo *bulk procurement* ndio unapata hiyo mia. Sasa tukiyaondoa haya sisi tunaweza tukawa *much cheaper* kwa Zanzibar.

Lakini natoa wito kwa wafanyabiashara wakubwa wawekeze Zanzibar kuja mafuta, wawekeze matangi makubwa makubwa. Nilisema mwanzo katika Bajeti nikavamiwa hapa nikaambiwa watu wanafikiri tunataka tumpe mfanyabiashara fulani alete mafuta, hapana. *Petroleum* analeta mwenyewe, GAPCO analeta mwenyewe, na wengine wanaleta wenyewe na wote wanaleta tani tano tano, tani kumi kumi. Ile gharama za kusafirisha ni ile ile na kila mmoja ataipeleka kule kwenye mafuta ili mteja alipie. Wenzetu wameshaondokana na utaratibu huo, wana chombo kikubwa kinamwaga mafuta pale halafu wao wenyewe wanasema tani ngapi, tukifika pahala tukaondoa utaratibu huu mimi nadhani Mhe. Jaku, mafuta kwetu yatakuwa ni rahisi zaidi kuliko kwengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti alipokuwa akijibu hoja alisema unaweza kununua mafuta Bara, anieleze tu hivi sasa angalau lita ngapi maana yake na baharini kule, hakuna mti kule unaweza ukaifunga meli, aeleze hasa kima gani kama lita kumi au kumi na tano za kuweza kununua kwa ndugu zetu Tanganyika.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu rudia hoja Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Alipokuwa akijibu hoja Mhe. Mwenyekiti alisema unaweza kununua mafuta kutoka Tanganyika kwa ndugu zetu wa Bara, ili kukidhi safari yako mpaka utapofika, lakini ninachotaka kumueleza ni bahari ile aweze kuweka *at least* watendaji wake wa ZRB waweze kujua lita ngapi kama elfu kumi au kumi na tano. Ile ni bahari na hujui unakwendea wapi sasa Mhe. Waziri atueleze lita elfu kumi, ishirini.

Mhe. Mwenyekiti: Unakusudia yale mafuta ya dharura.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ya kununua Tanganyika kule.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nataka nimuombe sana Mhe. Jaku ndugu yangu asije akaitumia hii kwamba kila siku meli yake ina dharura. Hii ni dharura, nasema hii ni dharura, meli inaweza ikakuharibikia iko Dar es Salaam na ikishafanya matengenezo meli inahitajia iwe *testing*, unai-*test* pale pale unarudi nayo mainjinia wanaokwenda nayo wanaona kwamba sasa iko *okay*. Ukajikuta kama mafuta uliyonayo yale yaliyobakia huwezi ukafika Zanzibar, hapa itategemeana umefanya *testing* hiyo kwa muda gani. Kama lita tano zinatosha ku-*fill* ile au lita nne. Lakini unaweza ukakuta mafuta yaliyobakia yanaweza kukufikisha Zanzibar huna haja ya kujaza mle ndani, lakini kama dharura hiyo imetokea unakuja Zanzibar, ZRB unawaonesha chombo kiliharibika na niliwapa Kampuni hii wakatengeneza na hii ndio gharama na nimenunua mafuta kutoka kwenye Kampuni hii, hii ndio niliyonunua hiyo ni dharura inakubalika.

Kwa hivyo ukisema lita ngapi mimi sijui umetumia ngapi mpaka ukaweza kukivusha chombo chako mpaka Zanzibar kwa sababu kila chombo kina *capacity* yake. Chombo kinapokwenda kwa *speed* zaidi ndio kinakula zaidi mafuta, ile *nautical miles* unayoiona ile ndio mafuta yanaliwa zaidi. Sasa chombo chako kikienda kwa *8 nautical miles* na mwenzako anakwenda *15 nautical miles* yule anatumia mafuta zaidi kuliko wewe. Sasa hiyo siwezi nikajibu lita ngapi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka kumtoa wasiwasi Mhe. Waziri wa Fedha mimi sina meli asije akafikiria natetea maslahi yangu ningekuwa nime-*clare interest* mapema mimi kwa mujibu wa sheria za hapa, nataka kukutoa wasiwasi kabisa Mhe. Waziri lakini wafanyabiashara, mimi si langu, mimi nimetumwa na ninatumikia wananchi wana hiari wananisikia wenyewe ninaowawakilisha hichi chombo, na chombo hichi kipo kwa niaba ya wananchi. Si cha mjomba wangu wala si cha kaka yangu, wanapotoka kule wanafika usiku sheli zimefungwa kupata mafuta ya magari inakuwa usumbufu, tujipange tuwe wazi tunapofanya kazi tuwe wazi, inafika meli hapa usiku anataka kurudi tena hakuna kituo cha kupata mafuta usiku. Tukitunga hizi sheria tuzitambue athari yake mbele kuna nini tusiwe tunavuta kama maandishi ya kiarabu ukakaa unavutia kwako.

Mhe. Mwenyekiti: Makusudio ya kauli yake ile ni kwamba wale ambao wana meli na wamepatwa na dharura hizo ndio makusudio, wale ambao wanamiliki meli na wamepata hiyo dharura, sio kwamba anasema kwamba wewe unayo meli, haidhuru amekuelekeza kwako. Lakini makusudio ni kwamba wale ambao wana meli na wamepata dharura.

Kifungu 2203	Bodi ya Mapato ZRB OfisiKuu	147,207,085,000
Jumla ya Fungu		409,892,465,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 19 - OFISI YA RAIS FEDHA UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	825,075,000
Kifungu 0401		

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa jinsi leo alivyochambua hoja za mtu mmoja mmoja, na kwa kiasi fulani Mhe. Mwenyekiti nataka niseme tumeridhika sana, na ninaomba sana ndugu zetu wa TVZ mimi leo nilikuwa naitaka hii CD ya Mhe. Waziri ili iwe kama kumbukumbu yangu niwe ninajikumbusha hoja zote alizotujibu Mhe. Waziri. Ninakuja katika hoja.

Mhe. Mwenyekiti Mhe. Waziri hoja zangu zote amezijibu vizuri isipokuwa moja tu inaonesha kidogo hakunifahamu vizuri nataka nimfahamishe kidogo ili nipate usahihi wa jawabu yangu. Nilipozungumzia suala la ZIPA katika

wawekezaji ambao nataka niseme kwamba hawatendei vizuri wananchi hasa katika zile haki zao ambazo katika masuala ya malipo aidha ya fidia au kuyatumia maeneo ya wazalendo wakawa wanawekeza wanapata faida wananchi hawapati kitu.

Suala la Maghembe namshukuru sana Mhe. Waziri lakini nilikuwa namuomba hili suala la Maghembe. Maghembe kwa Mkuu wa Wilaya amesaini kwamba anadaiwa milioni 16 na wananchi wa Michamvi, na akasema atazilipa kwa tarehe hakufanya hivyo. Wananchi wamekaa wakaja Baraza la Wawakilishi kuja kushtaki tukamwita Maghembe ni mtu maridhia sana unapomwita, kaja Barazani vile vile tukasaini naye mkataba pamoja na wananchi wa Michamvi, atalipa milioni 16 kwa tarehe, akatoa tarehe 25 mwaka uliopita, hakupita wala hajaja. Kwanza kalidharau Baraza na leo ameshazungumza na Mhe. Waziri anasema kwamba sasa hivi yuko safarini akirudi atamlipa.

Sasa kwanza nilikuwa nataka ajue tabia ya Maghembe kwa kukubali ni maridhia lakini katika utekelezaji kwa kweli anakuwa ni mkorofi, hilo nilikuwa nataka alichukue alifanyie kazi. Lakini hoja yangu inakuja katika muwekezaji hoteli ya Cristal. Mhe. Mwenyekiti suala la hoteli ya Cristal amejenga na mpaka sasa hivi kuna maeneo amejenga ndani ya eneo la muwekezaji mzalendo. Kamati yangu Mhe. Mwenyekiti tumekwenda na wao wenyewe akakiri yule Meneja kweli hizi nyumba karibu nne nimezijenga ndani ya eneo la huyu mzalendo. Sasa kama bado mpaka sasa hivi kuna nyumba ambazo muwekezaji wa hoteli ya Cristal anaendelea kuweka wageni anafaidika na mapato lakini limo ndani ya eneo la mzalendo.

Mhe. Mwenyekiti hapa si suala la fidia. Yeye alifunga mkataba na huyu mwananchi kwamba amuuzie lile eneo lake akakubali akalipa *advance* ya dola elfu moja lakini zilizobakia hajalipa tena mpaka leo bado, na katika ile *advance* wameeleza katika mkataba walitupa kwamba baada ya miezi miwili hajakamilisha yale malipo yaliyobakia fedha zile zitakuwa ni muflisi. Leo sasa hivi zaidi ya mwaka wa nne anaendelea kumzungusha, lakini bado anaendelea kuvuna fedha ndani ya eneo la huyu mzalendo. Hili Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri anipatie maelezo ya kutosha kwa sababu Mkurugenzi wake wa ZIPA analijua vizuri, sasa kama walipokaa hakumueleza vizuri basi hiyo ndio hali halisi. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti nadhani ndugu yangu Mhe. Hamza leo amelifafanua vizuri sana tofauti sana leo amelinyumburua hasa na nimemfahamu. Mimi nataka nimuombe tu kwamba huyu Cristal Hotel hawajakutana na mimi bado wala huyu Maghembe hawajakutana na mimi

bado walikuwa wanazungumza na ZIPA, kwa sababu kesi ikishafika ndani ya Baraza lako tukufu hili ni kesi ya Waziri. Namuomba sana anipe muda na mimi niishughulikie na ninaamini hili suala litakwisha, ninamuomba anipe muda na mimi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi Waziri sahibu wangu sana na ninaamini hili atalishughulikia, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti kwa sababu wananchi wameshaathirika kwa muda mrefu na wanaendelea kuathirika, naomba basi tujitahidi kabla ya kikao kinachokuja angalau haya masuala yawe yamepatiwa majawabu ambayo yataniridhisha na mimi. Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo naomba tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa namsikiliza kwa makini Mheshimiwa Waziri suala la huyu kijana niliyesema, kwa kweli majibu hayakuniridhisha. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti ninaomba unipe muda kidogo nieleze taswira yenyewe ilivyo halafu anambie kwamba kweli tunampa kada na huo muda ambao umeshatumika.

Mhe. Mwenyekiti, sisemi kuwa Waziri hafahamu nakubaliana nalo hafahamu, lakini wahusika wanam-*feed* vibaya sana na hilo ndio tatizo la watendaji wetu. Mheshimiwa kuna barua ya ruhusa ambayo kijana huyu ameomba ruhusa ya tarehe 15/11 kwa kuipelekea wizara husika nayo ikamruhusu tarehe 6/2/2012 hii barua naomba niinukuu kidogo tu Mheshimiwa Mwenyekiti. Ruhusa ya kuendelea kusoma MBA kipindi cha pili cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kwa heshima naomba husika na mada ya hapo juu. Idara ya Ujenzi inakujulisha kuwa umeruhusiwa kuendelea na masomo hayo kwa kipindi cha pili kuanzia tarehe 7/2/2012 hadi tarehe 29/2012. Kwa barua hii Ndugu Saada Ali Ahmed ambaye ndiye Msaidizi Mhasibu atashika dhamana ya uhasibu hadi kurejea kwako.

Mheshimiwa huko kwengine mimi nilikuwa sitaki niguse, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti nikigusa kutakuwa hatari tupu. Kwa mujibu wa sheria sikusoma sheria Mheshimiwa lakini kwa mujibu wa sheria huyu mtu hawezi kumtia hatiani wamemuonea tu Mhe. Mwenyekiti. Alikuwa *vice* wake ndiye aliyekuwa anasaini zile saini ambazo zilizofanywa *forgery*, kwa nini hataki tuwe wazi. Mheshimiwa nina *document* hii hapa *bank* zipo hapa ninazo na *check* hizi hapa zipo, sasa tatizo liko wapi Mheshimiwa, kwa kuwa mnyonge hana haki ya kuwatetea ndio sisi watetezi.

Ninamuomba sana Mheshimiwa hili asilitie mkono yeye alipiga *bismillahi* pale, alianza kwa jina kubwa la Mwenyezi Mungu na leo mwezi mtukufu huu,

huyu kijana hana hatia namwambia Mheshimiwa kwa nini tufanye mdororo mkubwa, kwa nini tumtafute kada wa kuweza kum- *peruse* tena Mheshimiwa *automatical* yuko *open* na sheria halafu leo akija kudai mafungu mengi mtakuwa hamumlipi nyinyi. Naomba nisikie kauli ya kurejeshwa kazini Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti ndugu yangu Mhe. Mshimba yeye ndiye aliyesababisha mimi nitie mkono, angekuwa hajalileta humu ndani mimi nisingelitia mkono. Lakini ile kuniletea humu ndani akataka nimjibu ndio nimelitia mkono. Mimi hii kesi nimeshaletewa ofisini wahusika wenyewe wamekuja wazazi wao wamekuja. Lakini jibu langu niliwaambia kwamba Wizara mama kwanza waache waliangalie wamepatia ufumbuzi wizara mama. Wizara ya Ardhi, Ujenzi ndio waliohusika lakini tukasema kama hili halitoshi, pengine Wizara mama wanaweza wakathubutu kufanya kama vile ambavyo anavyosema Mhe. Mshimba kwamba labda watamuoneaonea, tukasema hebu CAG huyu yupo kwa mujibu wa sheria, yupo kwa mujibu wa Katiba, tumpe afanye hii kazi huyu yeye yuko kati kati ya wote, ataitazama, atamtendea haki yule Mhasibu kama ana haki, ataitendea haki Wizara kama ina haki, lakini kilichofanyika nini Mheshimiwa? Kilichofanyika ni uhalifu mkubwa sana.

Cheque zimebadilishwa herufi badala ya *six* zimeandikwa *sixty*, zimeongezwa na ziro nimeletewa zote. Hizo alizokuwa nazo ndugu yangu Mshimba mimi karibu miezi sita nimeletewa kila kitu lakini nimenyamaza kimya, natazama Wizara mama watamalizana vipi. Sasa yeye Mhe. Mshimba ndiye aliyenisababisha mimi nilitie mkono hapa, kwa sababu amelileta yeye hapa. Sasa ndugu yangu Mhe. Mshimba ushalitia mkono ushalileta hapa mimi nilifanye nini? Nitalitia mkono na mimi ninalitia mkono sasa. Lakini ninachokuomba Mhe. Mshimba tumpe nafasi Mkaguzi na Mdhibiti, na wameshaanza hii kazi na wala haitotiwa mkono ripoti yake, kama sheria zinaniruhusu ripoti yake vile vile itakavyokuwa *raw* akupe na wewe kama sheria zitaruhusu vile vile ilivyo akupe na wewe uione, kama huyu kijana hana kosa hataingia hatiani, tutamlinda kwa sababu na yeye ni Mzanzibari ana haki kama hana kosa hatoingia hatiani, lakini kama ana kosa haya ndio tuliyoyapigia kelele hapa, wizi, ubadhirifu na mengineyo. Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Mshimba avute subra tusubiri ripoti ya Mkaguzi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti mimi si mkaidi sana ninamshukuru sana nilikuwa ninam-*trace* kitu kama wajibu wa sheria wa wanasheria wanavyotafuta njia nyengine na kwa kufanya ueleze ule muelekeo. Nimshukuru Waziri kuwa aliliona hilo suala kuwa kuna kitu kimeongezwa badala ya milioni sita inafanywa moja inakuwa milioni 16. Hilo

mimi nakubaliana naye wala sina pingamizi naye na ndivyo ilivyofanywa humu katika *document* hizi nilizoonesha. Na isitoshe hata benki imefanyiwa *forgery* humu zimo. *Pay slips* za benki ambazo sizo naomba na eneo hilo nalo aliangalie.

Lakini Mhe. Mwenyekiti nimtake sana Waziri tafsiri ya kulitia mkono sikufahamu hapa mkono kautia wapi? Sasa hapa kidogo Mheshimiwa naomba akinipa tafsiri hii tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo tuache hiyo si hoja, kutia mkono ni ile ulivyozungumzia wewe ukalileta hapa na yeye kuingia akatoa majibu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi nyengine, Mhe. Mwenyekiti katika hoja ambayo nimeizungumza sana katika Baraza hili na katika kamati za matumizi ni suala la mradi wa E-*Government*, na bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti unakumbuka tulipokuwa tunajadili hiyo bajeti ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora nimefikisha pahala pa kuomba Kamati Teule ya kwenda kulichunguza suala hili, tukafika pahala pazuri lakini baadae ukaelekeza wewe kiti chako Mhe. Mwenyekiti kwamba tulisubiri katika Wizara ya Fedha.

Ninashukuru niliungwa mkono na Wajumbe wengi sana siku ile, lakini jana katika kuichangia ninashukuru Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Kamati ya Kisekta inayosimamia wizara hii katika mapendekezo yake nayo ikasema kwamba mradi huu umekuwa ukipigwa danadana baina ya wizara nyingi, umefika pahala ukachunguzwe na ripoti yake ije Barazani. Mhe. Hamza na yeye pia jana akaniunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia maelezo kwanza yaliyomo katika kitabu cha bajeti ya Waziri kuanzia ukurasa 70 mpaka 74 na maelezo yake aliyoyatoa leo. Sehemu kubwa ya maelezo yake Mhe. Mwenyekiti yalikuwa yanahusu kutufahamisha juu ya huu mradi, faida zake na kwa nini umekwama, lakini tulichokuwa tukikizungumza cha msingi Mheshimiwa Mwenyekiti hoja yetu ni kwamba matumizi mabaya ya fedha za wananchi maskini wa Zanzibar. Na nilipoibua hoja hii Mhe. Mwenyekiti hoja yangu ilikuwa ni kwamba kwa hali halisi ilivyo, haielekei milioni 19 dola ambayo sasa tunaambiwa milioni 20 dola ni thamani halisi ya ile kazi ambayo imefanyika na jinsi namna ilivyoripuliwa ripuliwa.

Sasa katupa mchanganuo leo baada ya kupigwa danadana muda mrefu Mhe. Mwenyekiti, na kuthitibisha kwamba suala hili kuna kitu kinafichwa, kama nilivyosema mara nyingi Mhe. Mwenyekiti kwamba kama hesabu zilikuwepo na mradi huu umekamilika zamani. Sisi tulikuwa Wajumbe wa Kamati ya

Katiba, Sheria na Utawala wakati ule tulikwenda kuomba. Tuliandika barua Kamati ya Katiba Sheria na Utawala akatia saini Mwenyekiti wangu wakati ule Mhe. Ali Abdalla Ali kutaka mchanganuo hatukupewa.

Kwa hivyo tuna kila sababu ya kuamini kwamba kuna mambo mengi katika matumizi yale ambayo yameelezwa. Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema sitaki kurejea tena zile hoja nyingi nilizozitoa siku zile. Naomba tu sasa kwamba ile hoja kuunda Kamati Teule Mheshimiwa Mwenyekiti kwa mujibu wa kanuni ya 120 ya Baraza iamue ili kwenda kuchunguza thamani halisi ya mradi huu na yale mambo yake mengi niliyoyataja sina haja kurejea tena katika bajeti zilizopita umeshakubali Mhe. Mwenyekiti, lakini ukasema maamuzi yake tuje tuyafanye tukifika bajeti ya Wizara ya Fedha.

Ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha hili alikubali kwa sababu kwanza litamsafisha yeye na hao watendaji kama wako safi tutajua, kasema hapa kwamba tuiachie CAG. Mhe. Mwenyekiti kuna mambo mengine CAG ina nafasi yake na Baraza hili kwa mujibu wa Katiba yetu, kwa mujibu wa kanuni zetu lina nafasi yake. Naomba Baraza lipate nafasi kwa sababu pale kinachohitajika Mhe. Mwenyekiti ni *investigative audit* sio *audit* ya kawaida. Na bila shaka kuna mambo ya kitaalamu nilisema siku ile kama tutaomba hiyo kamati kama utaikubali Mhe. Mwenyekiti na Baraza likaridhia ipewe wataalamu angalau wawili mmoja mambo ya mahesabu, mmoja wa fani hii ya mambo ya ICT ili kuweza kujiridhisha kwamba gharama za pauni milioni ishirini dola ni thamani halisi au fedha za wananchi wa Zanzibar zimepotezwa bure na zikaishia ndani ya mifuko ya watu naomba tuliamue Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti sijui hasa Mhe. Jussa anachokitafuta kwa sababu maelezo anayoyatoa inadhihirisha kwamba *there is no imperical evidence*, hakuna *imperical evidence. Imperical evidence* baada ya CAG kutoa ripoti yake akabaini kwamba kuna ubadhirifu katika mradi huu, hapo kama nyinyi mtaunda kamati teule, kama Mhe. Haji Omar Kheri atawaambia kitengo cha rushwa hapo kuna *imperical evidence*. Lakini leo unaamka tu unaanza kufikiria kwamba hizi milioni ishirini *it's not worth* kwa kazi iliyofanywa mimi na Mhe. Jussa lazima tukubali *technical* hatuna utaalamu wa hata jenereta, lazima tukubali.

Hatuna utaalamu hata ile *fiber optic* ule waya unanunuliwa kiasi gani kwa mita, hatuna utaalamu huo. Mimi niko *more concern* kuliko hata Jussa katika fedha za wananchi lakini nasema *let us follow the proper channel* katika kuchunguza hili huyu *auditor* mdhibiti anao hawa wataalamu anaosema Mhe. Jussa, *investigative auditors* anao na aende akauchunguze huu mradi, aende

atazame hizo bei alizotupa mkandarasi, halafu aende aseme mkandarasi kuna mtu gani aliyekula pesa atazamwe kwenye mifuko yake kama zimo. Lakini *let us follow the procedure* mimi nalinda utawala bora katika suala la kifedha, twende na *procedure* hiyo, tukienda na *procedure* hiyo nakuambia Mhe. Mwenyekiti *you will save your money*, kamati teule utatumia pesa zako ambazo hazina msingi ambao hawajui waanze wapi.

Tunaunda Kamati Teule kwa ripoti ya CAG ambayo somo yangu anaiwasilisha hapa anaisoma hapa, tunasema kwa hili tunataka tuunde Kamati Teule. Mimi nikimuuliza CAG bahati nzuri yuko juu kule lakini haruhusiwi kusema hapa, nikimuuliza keshakwenda kwenye mradi huu hajaenda. *I respect* mawazo ya ndugu yangu Mhe. Jussa, lakini namuomba na yeye tufuate *procedure, otherwise* tutapoteza pesa za wananchi. Mwaka jana hapa kwa Kamati Teule, Kamati Teule Mhe. Mwenyekiti tulipanga kutumia milioni sitini, *at the end* tumetumia milioni mia tatu na Baraza hili Kamati Teule hizo.

Mimi nakuomba sana Mhe. Mwenyekiti, tumtumie CAG kwanza afanye kazi na mimi nataka CAG ripoti yake iwe wazi kabisa juu ya huu mradi, kama hatutakubaliana na ripoti ya CAG *then* ndio mtasema sasa Kamati Teule, ninamuomba sana ndugu yangu Mhe. Jussa kwa hili.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ninamheshimu sana kama anavyoniheshimu yeye Mhe. Waziri, na ninamuonea huruma sana kama alivyoonewa huruma jana na Mhe. Hamza kupewa kazi ya kuja kujibu mambo hata yeye mwenyewe kakiri leo kwamba yeye keshachoka kujibu hoja za watu na hii ninamuonea huruma sana. Mhe. Mwenyekiti zile ndevu nyeupe alizosema zitaendelea kuongezeka mpaka zikafika kichwani kwa sababu kubeba na kutetea mambo haya si kazi nyepesi.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako linaongozwa na msingi wake na msingi wake ni kanuni limepewa uhalali na Katiba, Katiba ikatoa nafasi ya chombo hiki kutunga Kanuni. Kanuni zetu zimetoa ruhusa katika Kanuni ya 120 kuunda Kamati Teule na inasema haikuweka utaratibu huo anaozungumza *procedure*, *procedure* tunatishana tu humu ndani. Haijaweka *procedure* humu kwamba jambo haliwezi kuchunguzwa na Baraza mpaka likachunguzwe na CAG au chombo chengine chochote kama cha Mhe. Haji Omar Kheri alichokitaja cha Mamlaka ya Kuhujumu Uchumi na Rushwa haikusema hivyo, hizo zote ni mamlaka za mhimili wa utawala. Chombo hiki Mheshimiwa ni mhimili wake peke yake na unalindwa na Katiba na msingi wake ni Kanuni. Kanuni inasema:-

'Baraza linaweza kuunda Kamati Teule kwa ajili ya jambo fulani, Kamati Teule itapendekezwa kwa njia ya hoja itakayotolewa na Mjumbe na kuamuliwa na Baraza, taarifa ya hoja hiyo haitajadiliwa'.

Mhe. Mwenyekiti lakini kabla sijakaa kwa sababu kasema kwamba hatuna msingi na nasikitika sana kafanya *reference* kwa Kamati zako zilizopita Teule kwamba tumetumia milioni mia tatu na sitini kwamba haikupatikana tija. Tija imepatikana Mhe. Mwenyekiti, na tija haikupatikana kwa sababu serikali imeamua kuzikana ripoti haitaki kuchukua hatua. Lakini Kamati hakuna hata mtu mmoja anaweza kusema kwamba ripoti zilizowasilishwa humu ndani kama zilikuwa hazina kitu, zimesaidia sana na mimi naamini hata maongezeko wanayopata ya mapato yametokana kwamba sasa watu wanaona kwamba kunaweza kukafichuliwa uovu katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti kasema kwamba sina utaalamu yeye hana utaalamu Mhe. Omar kwa sababu e-*mail* mpaka leo hana, mimi angalau e-*mail* ninayo. Lakini kama inawezekana rahisi kwake zaidi kupewa taarifa zilizokuwa hazielewi na watendaji wake. Lakini Mhe. Mwenyekiti hoja za msingi zipo. Sasa mimi siwezi ukinambia kwamba suala hili nikaliandikie wala sina tatizo mimi Mwenyekiti katika mambo ya msingi sina ukaidi, ukinambia hili nikalitengenezee hoja ya maandishi niilete Kikao cha Oktoba, nitaleta mimi Mhe. Mwenyekiti kuja kuonesha hayo mapungufu yapo wapi, lakini katika hoja yangu niliyosema Mheshimiwa kwamba kwa sababu na leo ikiwa Oktoba nimesema ikiwa hoja itakubalika kwa sababu haya mambo sisi Wawakilishi tunataka wataalamu ndio maana nikapendekeza kwamba aingizwe mtaalamu wa mambo ya ICT na mambo haya na Kanuni zinaturuhusu hilo, aingizwe na mtaalamu wa mambo ya mahesabu kwenda kuchunguza uhalisia wa mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti wala hilo si geni katika Kamati za Baraza hili, Kamati za mabaraza mengine katika mabunge ya Jumuiya ya Madola wala Kamati za mabunge mengine yaliyokuwa nje ya Jumuiya ya Madola. Mhe. Mwenyekiti kuna mambo ya msingi juu ya gharama halisi hakujakuwa na *tendering* kwa kweli ni *procedure* katika masuala yale, majengo yaliyojengwa, yamejengwa bila ya kufuata kuna mambo mengi niliyazungumza nimesema sitaki kuyarejea kwa sababu niliyazungumza siku ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Na siku ile serikali ilikuwepo hapa haikuyakataa haya iliakhirisha tu kwamba maamuzi yaje yafanywe ikifika Wizara ya Fedha, leo serikali inasema kwamba aa ni safi, na nasema tena kama matumizi yalikuwa ni safi kwa nini Mheshimiwa ichukue mwaka mzima kupewa majibu ya barua yetu hii, ambayo kwenye Baraza hili tulikumbusha zaidi ya mara nne katika vikao tofauti.

Mheshimiwa nina kila sababu ya kuamini kwamba *figure* zile za kupika na naweza kusema Mheshimiwa bado kunahitajika kwenda kufanya uchunguzi ili Baraza hili Wawakilishi wako hawa Mheshimiwa ambao wamekuja hapa wametumwa na wananchi, tukisema kwamba Mwakilishi asizungumze jambo ambalo hana utaalamu nalo basi itakuwa kazi kubwa sana Mheshimiwa wataalamu humu wachache sana humu. Lakini kazi yetu ni kufanya utafiti kutokana na hao wataalamu huko nje tukaja tukawakilisha humu ndani kwa niaba ya wananchi waliotuchagua.

Naomba sana serikali imefanya upande wake watuachie *backbenchers* tukafanye kazi yetu kwa mujibu wa kanuni, tuunde kamati teule Mhe. Mwenyekiti, na naomba utuhoji ili tukubaliane kuunda kamati teule ambayo kwa kawaida haijadiliwi, na kama anasema kwamba laa! mimi nitaheshimu kiti chako, kama niitungie maelezo nilete katika kikao cha Oktoba nitaitungia maelezo katika kikao cha Oktoba. Lakini Mhe. Spika, ninaomba tusitengeneze mjadala sababu kanuni inasema inabidi tuamue bila ya kufanya mjadala. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie ndugu yangu Jussa kwamba chombo hichi kina faida ya *hansard*, mimi wala sikusema kwamba kamati teule zilizofanya hazikuwa na tija, nitaitisha *hansard* sasa hivi nisome maelezo yangu, ninamuomba sana aseme yale niliyosema. Nimeseme bajeti tuliyoiweka kwenye kamati teule ilikuwa ni 60,000,000/= *at the end* tumetumia milioni mia tatu na kitu, sikusema kama haikuwa na tija. Ninachokisema mimi na yeye mwenyewe kanuni ameisoma hapa hapa Mhe. Jussa, anasema kwamba Baraza linaweza kuunda kamati teule, linaweza sio lazima, kama hakuna majibu ndio maana yake, kama hakuna majibu, lakini majibu yako na Serikali ilipokuwepo hapa wakati mimi sipo walitoa majibu, lakini wewe ukaeleza kwamba tumsubiri Waziri wa Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza majibu, kama hizi *data* anasema zimepikwa ni muono wake, sasa kathibitisha wapi zimepikwa ripoti ya CAG haipo, sasa ripoti ya CAG ndio tunasema kwamba tuanzie na ripoti ya CAG akachunguze huu mradi, naona ndugu yangu Jussa tunazungushana tu yeye anataka lazima aanze na Kamati Teule, kwa nini unaanza ya juu wakati chini hujakamilisha huku taratibu za chini. Mimi namuomba sana na uamuzi wa kuunda kamati teule unao wewe Mwenyekiti. Mimi ukiona kwamba kuna hoja za msingi anazo Jussa za kuunda Kamati Teule unda, ukiona mimi nina hoja za msingi tuiachie CAG, mimi nasema tumuachie CAG, tusipoteze pesa za umma wakati CAG amepewa majukumu hayo kikatiba, kama Baraza lilivyopewa majukumu kwenye katiba. Sisi tunang'ang'ania upotevu wa fedha za umma halafu tunalazimisha zikapotee tena. Naomba kama tuna matatizo ya mradi

huu CAG akachunguze na mimi nitakuwa tayari kila atakayehusika na ubadhirifu ndani ya mradi huu basi achukuliwe hatua *including my self.*

Mhe. Mwenyekiti, Makamu hapa kasema juzi kama CAG ataidhinisha kwamba Waziri anahusika na mradi huu nichukuliwe hatua, kila atakayehusika achukuliwe hatua. Mradi huu Kamati yake ilivyoundwa wakati huo Mhe.Rais Karume alisema kwamba kamati ya wataalamu na kamati ya *steering committee,* aliunda *steering commitee* Katibu Mkuu wangu ndiye aliyekuwa Mwenyekiti na baadhi ya Makatibu Wakuu walikuwa ni wajumbe ili waweze kufanya kazi kama ni Serikali kwa pamoja, utaratibu wa kutoa pesa kwa Exim Bank na Mkandarasi sioni hizo zitakuwa zimeliwa pahala gani, sioni.

Mhe. Mwenyekiti, niko *genuine* na ninalinda sana heshima yangu, kama CAG atagundua Waziri kahusika na mradi huu basi naomba Rais anichukulie hatua na watakaohusika wengine basi watachukuliwa hatua, kama kuna *element* ya watu wamekula, maana hapa tusiwe na dhana tu, chombo hichi hakipaswi kuwa na dhana, tunatoa *tension* kwa wananchi kwamba Serikali wizi, si kweli Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana tufuate zile *procedure*, kanuni zetu zinasema mnaweza kuunda, si lazima, ukishasema unaweza Mwanasheria huyu hapa, Jussa mwenyewe ni Mwanasheria, Abubakar ni Mwanasheria, mimi *by profession I am not a lawyer*, Mshimba kule Mwanasheria nasikia na yeye.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Jussa, twende na CAG kwanza, tumpe kazi CAG, tuache *process* hizi kwanza ziende tumpe kazi CAG, mimi na yeye tufanye kazi kwa pamoja tumpe CAG, na ripoti tutakuja kuisoma hapa hapa, hapa tutakuja kuisoma.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa, mimi nasema kanuni iko wazi, haina matatizo, inapotokea juu ya hili jambo lichunguzwe, lakini pale unaposema kwamba Baraza linaweza, sasa ile kufikia kiwango cha kuweza mwachieni anayeendesha kikao. Kwa sababu hatimaye yeye ndiye atakayesema haya basi anayeunga mkono hoja, anayekataa hoja. Anayeendesha kikao anasema *position* ya kuunda Kamati Teule kwa hili bado, na kimsingi unapounda Kamati Teule maana yake Serikali imeshindwa kufanya kazi. Kwa hiyo sasa upatikane msaada wa Baraza ili hatimaye Serikali ielekezwe kwamba ifanye nini. Sasa kwa kuwa kazi bado inafanyika juu ya jambo hili hili basi tuache, kama uchunguzi utaonesha bado hakuna ufafanuzi mzuri basi hiyo sasa itakuwa ni *position* ya kusema kwamba OK ile hoja sasa tuiamue. Kwa kipindi hiki siruhusu hoja iamuliwe ya kuunda Kamati Teule, kwa sababu kuna kazi bado inafanyika. Tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	285,297,000/=
Kifungu 0701	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	3,183,570,000/=
Kifungu 0801	Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Naona kama kuna Idara tumeziruka, kuna Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, yeye katupeleka moja kwa moja kwenye ukurasa wa 99, hii iko ukurasa wa 96 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Tumeshakisoma Mhe. Jussa kifungu hicho.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Sawa tuendelee

Kifungu 0801	Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam	326,970,000/=
Kifungu 0901	Idara ya Fedha za Nje	173,868,000/=
Kifungu 1301		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu nilizungumzia suala la Kampuni ya Zantel ambayo Serikali ya Zanzibar ina hisa, na katika kitabu cha Mhe. Waziri, alizungumza hii katika maeneo ambayo yanasimamiwa na Idara hii ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwanza Mhe. Waziri, katika hili kusema kwamba wanalifuatilia na kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitaruhusu Zantel kuuzwa, nashukuru kwanza kwa kuhakikisha hili. Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yake kasema kwamba kuna hatua zinaendelea na kaahidi kwamba tutakaa pamoja, ni matarajio yangu kwamba haitokuwa ahadi ile kwamba tutakaa pamoja ili tupitishe bajeti tu hapa halafu ikasahaulika, lakini kwa sababu kaahidi tutakaa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naelewa kwamba hivi sasa kuna baadhi mnakwenda kusali, sitaki niseme msiende kusali, lakini mkitoka mmoja mmoja namna hiyo maana yake hatimaye itakuwa hatuna *quorum* itabidi tusimamishe shughuli zetu, niombe basi walioko nje warudi ndani tumalize kazi. Endelea Mhe. Jussa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo ninasema kimsingi Waziri alichosema ni kwamba yako mambo mengi ambayo asingependa kuyazungumza hapa katika Baraza. Mimi Mhe.Mwenyekiti, niombe kwa sababu katika Kamati zako kuna Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambapo mimi ni Mjumbe, na Zantel kwa upande mwengine kwa sababu inahusika na mawasiliano inahusika hili. Kwa hivyo mbali ya kwamba Waziri kaniahidi, nadhani kwamba tunapaswa tushirikishwe vizuri kujua hatma yake hii na nadhani hizo taarifa ambazo hapa hawezi kuzisema kwa sababu pia Baraza letu linatangazwa moja kwa moja na kasema kuna

masuala ya kibiashara, ingawa nilisema katika hoja yangu jana kwamba Zantel yenyewe wamefanya maamuzi ambapo Serikali haikushirikishwa, ilishajivua nguo yenyewe ilipotangaza kutaka kujiuza wakatoka kila mtu kampuni inayotaka kununua ikakaribishwa ndani ikaja ikaangalia kila kitu chake, kwa hivyo washindani wake wanajua kila kitu cha Zantel sasa kwa nini hakufanya maamuzi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, sina pingamizi na hoja ya Serikali, ninaiomba tu Serikali kwa sababu si sahihi Mhe. Mwenyekiti, kudhani kwamba tunapenda sisi kuja hapa kila wakati kuisuta Serikali, lakini inapokuwa haitekelezi yale ambayo tunakuwa tunasema ndio tunapokuwa wakali zaidi, naomba hilo walitazame kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, jana nilisema hapa kwamba Kampuni ya *Etisalat* inaonekana ina mipango yake ya kuuza miradi yake, na katika utafiti wangu mdogo Mhe. Mwenyekiti, huyu aliyeletwa hapa kama ni CEO bwana Pratap, huyu huyu alimtumia *etisalat* kuifunga kampuni yao iliyokuwepo India baada ya kuja kampuni inayoitwa *Indian Tuji Telecom*, palitokezea *scandal* kubwa sana na mradi wao uliokuwa na thamani ya 820 milioni dola India, wakamtumia Pratap kuifungisha, sasa Pratap kaletwa Tanzania kaletwa Zanzibar kwenye Zantel, ndie huyu aliyesema Wazanzibari hana haja nao waondoke katika Kampuni, anatumia lugha chafu chafu. Kwa hiyo ninasema tusiingie huko lakini ninamuomba tu kwamba yote yazingatiwe haya, na katika kipindi hiki mpaka tukifanya maamuzi basi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iisimamie kampuni ya Zantel, na jana nilisema kuna mapendekezo mengi ya kuweza kuzingatia ikiwemo Serikali kuweza kutangaza mimi naamini Wazanzibari wakiambiwa Serikali inauza hisa za Zantel wazanzibari wananchi wenyewe wanaweza kuzinunua kuinusuru kampuni yao ikawa na huduma bora zaidi na wao pia wakapata faida na Serikali ikapata faida.

Kwa hivyo nasema sitaki tuamue hapo lakini nasema tu kwamba katika hayo aliyoyasema atayazingatia naomba sana, kwa sababu nina wasi wasi sana Mhe. Mwenyekiti, na Wajumbe wetu wawili waliokuwa katika Bodi ya Zantel kwamba kule wanasimamia maslahi ya Zanzibar nina wasi wasi sana mimi, watu wetu wanakwenda kule tunaangalia zaidi mambo yao mengine kuliko yale ambayo tumewapeleka kule kwenda kulinda maslahi yetu. Kwa hiyo naomba hili Serikali itizame kwa makini na sina wasi wasi na Mhe. Omar hata siku moja, nilimuona alikuwa mkali sana na hata katika suala la *E-Government* sikuwahi kumuhusisha kwa sababu najua hahusiki, na ingelikuwa najua anahusika ningelisema humu ndani, maana yake kawaida yangu huwa sitafuni maneno. Kwa hivyo nasema hii ni Serikali imekubali, imezingatia iishirikishe kamati mbili; kuna kamati ya fedha kwa sababu inahusika na Wizara hii ya Fedha, kuna kamati ya mawasiliano ishirikishwe

ili kwa pamoja tuone vipi kulinusuru hili na tusiruhusu *etisalat* kumtumia Pratap aliyekwenda kuinyonga kampuni ya India akaja akainyonga kampuni yetu ya Zantel hapa Zanzibar. Naomba sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa kuzishirikisha kamati sina matatizo kabisa na hilo ambalo limeelezwa na Mhe. Jussa, lakini nitaziomba tu kamati kwamba watakapokuwa wakiangalia haya kuna masuala mengine ya kibiashara wasije wakaya-*expose* sana kwa sababu kuna *competition* kubwa sana katika sekta hii ya simu, nitaziomba tu kamati zile mbili kamati ya sekta pamoja na hii kamati ya fedha wanaweza wakashiriki, wakaenda wakazungumza na Zantel, wakaja pale ofisini tukazungumza nao sisi kwa sababu Serikali ina hisa asilimia 18, tukawashirikisha hawa wajumbe wetu wawili wa bodi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nisema kwamba wajumbe wetu wa bodi ni Makatibu Wakuu, Katibu Mkuu Wizara inayosimamia masuala ya fedha na Katibu Mkuu Wizara inayosimamia miundombinu. Bodi imechukua Makatibu Wakuu, wakiondoka hawa nafikiri Katibu Mkuu ndiye anayekwenda aka-*replace* sio mtu. Kwa hiyo tutakapokuwa tunaitazama ile tuitizame kama ni Katibu Mkuu tusitizame kama mtu, kwa sababu mimi sina matatizo na hili analolizungumza Mhe. Jussa, acha tushirikiane kwa sababu ninaelewa nia yake ni kutaka kuona Zantel ina-*prosper*, Zantel inafanikiwa, hata na mimi nataka nione Zantel inafanikiwa na tubakishe jina la Zantel, Zantel ni *brand name* ya Zanzibar hatuwezi ikatutoka, hivyo mimi ninakubaliane naye kabisa.

Kifungu 1301 Idara ya Uhakiki Mali

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, nataka nithibitishe kwamba yale aliyoyazungumza Waziri wa Fedha nasema ni sahihi lakini pia sina tatizo kama alivyotaka kamati, lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba juzi nilimwita huyu Pratap, ukimuona kwa ghafla utafikiria mimi, lakini sio mimi, nikamueleza *concern* zinazozungumzwa hapa Zanzibar na kitu kizuri alichonambia kwamba sasa hivi Zantel wanafanya faida na wametuwekea orodha ya watu ambao wanaotaka Wazanzibari, yote haya ni kwa sababu Zantel mahali pake ni Zanzibar si mahali pengine popote. Na mimi nilimwambia kama kutakua na upenyenyo tu wa taarifa kwamba wanataka kuhama basi utaanza kuhama wewe kwanza.

Sasa naomba niwatoe wasi wasi na juzi kanithibithishia kwamba hilo halipo na nichomekee hapa hapa hata lile suala ambalo la walinzi na mambo mengine nimempa muda wa siku 30 atafute ufumbuzi ili tuondokane na matatizo na kuwanyanyasa wazanzibari katika sekta hiyo. Kwa hiyo tukae

mkao wa kuimarisha na kushirikiana na wenzetu hawa lakini Zantel *Zanzibar is their home, thanks*.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sikuwa na nia ya kusimama tena nilikuwa nimesharuhusu tuendelee lakini kwa sababu Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kaligusia jambo jengine ambalo Wajumbe walielezwa na mimi niliwahi kueleza humu nataka likae katika *records* tu kwamba hatumsemi mtu ambaye labda hatumjui Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hata sisi kamati yetu Mhe. Mwenyekiti wa kamati yangu ya mawasilinao na ujenzi, mimi mwenyewe na Mhe. Marina juzi tulipata nafasi ya kukutana naye alikuja na anaonekana hasa kwamba ukimleta hoja hizi anavyobadilika rangi unamuona hasa kwamba ni mtu ambaye anajua makosa yake katika hili, na hata katika maelezo yake alikuwa ameshakutana na Mawaziri hawa lakini bado maelezo yake kwetu sisi anakuwa analaumu kuzorota kwa huduma za Zantel kwa Wazanzibari, wakati Zantel inafanya vizuri walikuwa Wazanzibari hawa hawa waliyoiendesha na ndio walioianzisha. Kwa hivyo imetoka kampuni hii inakula hasara kwa sababu tulikuwa hatujapata wateja wa kutosha mpaka imefika ikawa inapata faida ya kutosha, na tulisema hapa katika mchango wetu kwamba imefika kampuni hii kujilipa *bonus* mwaka 2005 na mwaka 2006 dola 70,000, mwaka 2007 wamejilipa *bonus* dola 200,000 wakubwa wa kampuni hii, kwa hiyo wao ndio waliokuwa wakitumia kuvuruga kampuni hii halafu wakiwasingia Wazanzibari hawafanyi kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru Mhe. Waziri wa Kazi kwamba kaliona hili na sisi tumeliona niseme tu Mhe. Spika, kwamba wajumbe wetu wa bodi nao wasimamiwe na Mawaziri wetu kwa sababu ndio wanaosimamia sera; kwamba kuhakikisha wanalinda maslahi ya Wazanzibari kwa sababu hii kampuni ni yao. Ahsante sana.

Kifungu 1301	Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma	502,750,000/=
Kifungu 1901	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, masuali yangu mengi niliyoyaibua yamepata majibu, yako masuala mawili ambayo hayakupata majibu ninaomba Mhe. Waziri sasa anisaidiea.

La kwanza niliomba maelezo kwamba katika kujibu hoja zetu Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu juzi kuhusiana na suala la ZMA alituambia zile fedha zilitoka katika wakala wake wa *PHILTEX* waliokuwepo Dubai zilikuwa zinakuja Hazina na zilikuwa zinafuata utaratibu wa kifedha. Katika mchango wangu nikamuomba Mhe. Waziri akija aje aniambie ni Benki ipi iliyokuwepo Dubai au pengine nchi nyengine yoyote iliyokuwa ikitumika ku-

transfer fedha hizo kwa *account* ipi na *account* ipi ya Hazina Zanzibar na Benki ipi ikipokea fedha hizo za *PHILTEX* kwa wakala wa ZMA.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Menyekiti, ni kweli Mhe.Jussa aliuliza suali hili lakini nataka nitoe ufafanuzi kidogo inawezekana kwamba yeye na Waziri wa Miundombinu kidogo hapa katikati na pengine labda hawakufahamiana. suala hili ni hivi; Mhe. Spika, kulikuwa kuna *account* iko chini ya Wizara ya Miundombinu, ilikuwa na *signatory* wawili, Fedha na Miundombinu, na fedha zilikuwa zinaingia pale lakini baadaye zinajumuishwa katika mfumo mkuu wa Hazina. Sasa Mhe. Jussa, alivyosikia akafikiria labda zimeingia Hazina *account* kwa Hazina. Kwa sababu jana ilikuwa ni Jumapili nilichoweza ku-*establish* ni kwamba *account* ile ilikuwa chini ya PBZ, lakini nikashindwa ku-*establish* kwamba zilikuwa zinatoka Dubai kwenye *account* gani zimeingia pale kwenye ile *account*. Tukasema hili tutalifanyia kazi tuweze kulitafuta ili tuweze kujua zilikuwa zinakuja kwa utaratibu gani, lakini ni kweli kama alivyosema Waziri wa Miundombinu kwamba zilikuwa zinaingia kwenye ile *account* na kwa utaratibu wa Hazina tulilazimika sisi kuzitumia. Hilo kwa sasa hivi ndio ninaweza nikamjibu.

Mhe. Ismail Jussa ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naweza kuwa na matatizo mengi lakini matatizo yangu ya masikio *alhamdullilah* na ufahamu vile vile. Na tuliangalia *hansard* zitaonesha kwamba Mhe. Waziri wa Mawasiliano alipojibu aliitaja Hazina kwamba zilikuwa zinakuja kwa utaratibu wa kifedha na zilikuwa zinapokelewa na Hazina kwa sababu wakati ule Mamlaka yalikuwa hayajaanzishwa, hakusema kwamba kulikuwa na *account* iliyokuwa imeanzishwa ambayo ilikuwa na *signatory* wawili wa Fedha na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili tusizungushe sana maneno, fedha na Serikali ilikuwa inajua sijui kwa nini inatuficha hapa zilikuwa zinaletwa kupitia kwa wakala mmoja anaitwa Mohammad Bakar Ridhaa, *Forwarding and Clearing Element* aliyekuweko Dubai na zilikuwa zinakuja kwa mfanyakazi binafsi wa kuzipokea hapa Zanzibar kama zile fedha inakuwa mtu ana jamaa yake Uingereza akapeleka kwa wakala kule ukaenda ukazipokea kwa Said Mmaka pale zikawa zinapokelewa na bwana mmoja anaitwa Abdalla Mohammed Abdalla kwa jina binafsi wala si jina la Taasisi. Namuomba tena, hili nimelizungumza sana nataka kumuonesha tu Waziri wa Fedha kwamba tunaposema maneno humu hatusemi kwa kubahatisha, na Mhe. Mwenyekiti Wajumbe wako walipokuwa wakisema kwamba kulikuwa na fedha zilipotea na tunajua zilipotea kwa utaratibu huo, zilikuwa zinatumwa ikawa zinaishia Hazina. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha amesema hapa ana uchungu sana na fedha za wananchi wa Zanzibar, namuomba hili alifuatilie akajue zilikuwa zinatumwa kiasi gani, zimeingia kiasi gani halafu wachukue hatua.

Mhe. Mwenyekiti, masuala yaliyotokea juzi kwamba mtu akikosea tunaambiwa akachukuliwe hatua ya kuteremshwa cheo tu mtu ameshaiba milioni 80 kama ilivyokuwa imetokezea katika viinua mgongo vilivyokuwa havipo, hivi si kuonesha kwamba Serikali inajali kwa sababu kama humchukulii hatua ukampeleka Mahakamani mtu ameshaiba milioni 80 ataendelea tu na mwengine atakuja ataendelea. Hivyo hili nimuombe Mhe. Waziri, kama ana uchungu kama tulivyokuwa na uchungu sisi kuyafuatilia masuala, wazitambue fedha ngapi zimepotea na waliohusika wafikishwe kwenye vyombo vya sheria ili sheria ichukue mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri haina matata na taarifa zaidi ukitaka utachukua kwake Mheshimiwa Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani mimi na Mhe. Jussa, tunazungumza lugha moja, na nilisema kama nime-*establish* kwamba zinaingia kwenye *account* ya PBZ lakini sija-*establish* zinaingiaje, hiyo *account* ipo kila kitu kipo na zipo pale na nilisema kwamba yale ni maongezo ambayo niliyoyapata ya ziada kwamba kule kuna hiyo *account*, nakumbuka hata na mimi Mhe.Rashid Seif hakusema kwamba hiyo *account* ina *signature* mbili, mpaka dakika za mwisho mimi naingia Wizara ya Fedha Zanzibar kulikuwa kuna mzozo baina ya sisi na wao wanaitaka hiyo *account* iwe moja kwa moja kwao wao, nikasema hapana mpaka ZMA isimame vizuri ndio tutakuachieni hiyo *account*, lakini kwa sasa hivi lazima hizi fedha tuzidhibiti. Wazo lake nakubaliana nalo kabisa, mimi nitalifuatilia ili tuweze kuona kiasi gani cha fedha tulitakiwa kukipata na kiasi gani tulichokipata, na baadae tuanzishe utaratibu kama kuna fedha zetu za ziada basi tuzipate kwa utaratibu ambao tumeuanzisha pale ofisini.

Kifungu 1901	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	3,962,349,000/=
Kifungu 2201	Idara ya Bajeti	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nchi yoyote duniani suala la huduma za afya limo ndani ya Katiba kama ilivyo katiba ya Zanzibar. Kwa msingi huo Wizara ya Afya ndio roho ya kila mwananchi na sote ndio kimbilio letu hasa kwa suala la matibabu ndio haki ya kila binaadamu. Yeye Mhe. Waziri wa Fedha, kwanza ilikuwa aombe radhi kwanza kwa jinsi ya wananchi wa Mnazi Mmoja kukosa huduma ya *oxygen* kwa siku tatu au nne ni kitendo cha aibu na cha kutia huruma.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu nimshukuru kwanza hoja aliyoijibu ya milioni 40 kuipatia kitengo cha Hospitali ya Mnazi Mmoja hilo nataka nimuombe ili

hansard zikae sawa aeleze kuwa watazipata kwa wakati Hospitali ya Mnazi Mmoja.

La pili cha kusikitisha ingawa waswahili wanasema *taa unawasha ndani ya nyumba au sadaka inaanza nyumbani*, kitabu chake hiki kajivutia kwake zaidi, Wizara nyeti ambayo Dkt. Ali Mohammed Shein hata katika uteuzi wake alianzia na Wizara ya Afya kwa kuthamini wananchi wake. Hapatoshi hapo Mhe. Mwenyekiti, nilipigia kelele sana suala la wazazi humu nikawa napata jawabu haziridhishi lakini kusikia mwenyewe kaondosha huduma ile.

Mhe. Mwenyekiti, nataka anipe maelezo ya kina na ya msingi kuwa kama alivyochukua 100% yeye katika kitabu chake na Wizara ya Afya aipe 100% vile vile, maelezo yangu yulikuwa ni hayo tu Mhe. Mwenyekiti, hapa nitakuwa mkaidi wala sina sumile, niko tayari kwa lolote kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti: Hee hii mambo ya kuwa tayari kwa lolote hili inawezekana ikawa moja ya kupigana na humu siruhusu. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe.Jaku, asiwe tayari kwa lolote kwa sababu wengine mkiyazungumza hapa watakimbia.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku, ameuliza masuali mawili, la kwanza ametaka nimpatie *assurance* kwamba Hospitali itapata fedha zake *ontime*. Nimeeleza na nimekuwa *very specific* katika maelezo yangu, sikusema *ontime too,* nimesema tarehe 3 ya kila mwezi Hazina; tena haya ni makubaliano kabisa baina ya uongozi wa Wizara ya Afya na Hospitali na uongozi wa Wizara ya Fedha, tarehe 3 ya kila mwezi watapatiwa Wizara ya Afya 30,000,000/= *plus imprest* 10,000,000/= kwa ajili ya hospitali ya Mnazi Mmoja. Na tarehe 5 tumesema *by latest* tarehe 5 Wizara ya Afya wazitoe wawapelekee Hospitali. Kwa sababu mimi nafanya kazi na Wizara, nisije nikazitoa mimi tarehe 3 wenzangu kule wakakaa nazo hawajazipeleka tena ukaja ukanifuata mimi Mhe. Jaku, niko *specific*, tarehe 3 *from the Ministry of Finance to the Ministry of Health* na tarehe *5 from the Ministry of Health to Mnazi Mmoja Hospital*, tumeweka tuko *specific* na hii nataka ikae *very clear* na wala sisi hatutachelewa, sisi tuna utaratibu wetu, tutaweka barua ya *order PBZ*, ikifika tarehe ile zitoke *automatic* tutaweka. Hii itatusaidia sisi zitatoka *automatic*, sasa sijui wale wenzetu wa afya kama na wao wataweka *automatic* hili litakuwa ni baina ya Mhe. Jaku Hashim na Mhe. Juma Duni JJ zitakutana. Hilo la kwanza.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, nimejieleza kwa nini mimi kwangu nina mia mia pale, ile ni *figure* ya kibajeti tu lakini *actually* sijapata mia mimi.

Nimesema kutokana na shughuli za Baraza hili ilikuwa tuwakate *two billions* kwa ajili ya mchango wa meli lakini Baraza hili hatujalikata tumeziacha ili tutekeleze shughuli zenu, lakini pesa zile lazima kuna idara zikatwe ndio baadhi ya idara zikasema aa idara za kwangu kwanza tuanze kuzikata.

Kwa hivyo, kihesabu lazima zikae pale zimepata asilimia mia kwa sababu nimezichukua zote nimepeleka kwenye meli. Kwa hivyo, hili nalo nimelieleza Mhe. Mwenyekiti, sio kama nimepata mia ukienda ukitaka halisi hasa nimetumia ngapi tutakupa vile vile, lakini kibajeti lazima kule kwa sababu nimetoa kwenye *account* zao lazima zionekane, na hii kwa ku- *reflect* shughuli za Baraza, tumeona kwamba ule utaratibu wa mwanzo kila pahala tukate hapa tukaona shughuli zake zita-*paralyze* hilo tu Mhe. Mwenyekiti, ndilo ambalo nimelieleza.

Mhe. Mwenyekiti, na ukitizama historia huu ni mwaka wangu wa tatu *check record* ya Wizara ya Fedha matumizi sina mwaka hata mmoja niliyopata asilimia mia moja na pesa ndio ninazo mimi pale naziona, lakini tunafuata ule utaratibu, wenzetu kinachopatikana tunagawana hivyo hivyo kidogo kidogo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza watendaji wa Wizara ya Afya wapo sijui kazungumza na nani hapa anaweza kutuhadithia nani kazungumza naye ili kuweka rikodi sawa.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja imekuwa kimbilio la wanyonge wengi, Mhe. Waziri tufahamishe watendaji wapo wa Wizara ya Afya, Waziri yupo umezungumza naye au Katibu Mkuu tupate kujua tuweke rikodi sawa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna kikao hapa ndani ya Baraza lako lakini kwenye vyumba vya nje, uongozi wa Wizara ya Afya na uongozi wa Hospitali na Makamu wa Pili wa Rais, wakazungumzia matatizo ya hospitali.

Uongozi wa Wizara ya Afya unaongozwa na Waziri wa Afya. Mimi na Katibu Mkuu wangu tuliitwa kwa masuala ya barabara na uongozi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa sababu niliona mkutano ule mle ndani unachukua muda na sisi tumepewa muda muafaka tuingie mimi nikafungua mlango nikatizama nani hawa walioko ndani, Mhe. Makamu wa Pili akatuita akasema njoo wewe na Katibu Mkuu wako, tukaingia tukasikia malalamiko, Katibu Mkuu wangu akasema sasa hivi tutokeni uongozi wa Wizara ya Afya tumuache Waziri tu, alikuwepo Katibu Mkuu, Mkuu wa Hospitali, alikuwepo Dr, Malik sijui ana cheo gani kule Wizara ya Afya, Mkurugenzi Mkuu, na kwangu mimi kwenye mkutano alikuweko Katibu Mkuu na Mhasibu Mkuu. Hao ndio waliokuwepo ndio wamekubaliana na msingi huo na sisi tunataka

tuutekeleze hivyo walivyokubaliana. Sijui kama Mhe. Jaku nimekupa chochote, katika kikao hicho ninachokijua mimi kama kuna kikao chengine sikijui.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi kabla hujanihamisha katika kamati yako ya Wizara ya Afya uzoefu unanionesha mradi wa kuimarisha huduma za afya wilayani, naomba niseme Mhe. Mwenyekiti. Serikali haiko *serious* ilitakiwa ichangie shilingi milioni 150 haya si maneno yangu, imetoa shilingi milioni 20 tu, haya hapa kwa mujibu wa Ripoti ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Afya katika mwaka Oktoba – Disemba 2012, sasa hapa sisi itakuwa tumekuja kupiga kofi hatujawatendea haki. Hii Mhe. Mwenyekiti, tumechukua dhima sisi kwa wananchi, sasa mwenyewe Waziri awape pesa zao kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ndio hoja yangu ya mwisho tukijaaliwa hii kwa leo. Mheshimiwa nilisema pale kwamba kuna hoja mbili Mhe. Waziri alizisahau, nashukuru ile moja tumeimaliza naomba sasa vile vile anisaidie hoja yangu niliyoitoa ambayo aliisahau katika majibu yake.

Katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nilinukuu katika Idara ya Bajeti ukurasa wa 25 wa hotuba yake ukisema kwamba, "Shilingi 2,520 milioni zilihaulishwa kwenda katika kifungu cha safari za nje za viongozi wakuu".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilimuomba akija anisaidie kwa mwaka huu tunaomalizia fungu la safari za viongozi kwa safari za nje na za ndani liligharimu kiasi gani kwa pamoja na baadae anipe mchanganuo kwa Ofisi ya Rais Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili katika fungu la safari za ndani na nje kwa Viongozi wetu Wakuu hawa zikoje. Hayo masuala Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu; hili ni Baraza la Wananchi na suala hili mara nyingi sijui kwa nini huwa linakwepwa kwepwa. Niliwahi kuandika swali kwa maandishi nikalileta la kuhoji sio mafungu ya viongozi hawa tu, lakini kwa Mawaziri kwa jumla, nimekaa mwaka mzima Mheshimiwa halijatokeza tena katika masuala haya kwa sababu kila mmoja anamtupia mwenzake. Naomba leo tena, nilimuuliza tangu jana nina hakika keshapata muda wa kutosha wa kupitia mafungu anisaidie, fungu la pamoja la safari za ndani na nje ni kwa kiasi gani, halafu kwa kila mmoja kati ya Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili katumia kiasi gani naomba Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ismail Jussa aliuliza suali hilo, lakini namuomba radhi kwamba sikujibu labda niliruka kidogo. Nataka niseme hivi Mhe. Mwenyekiti, viongozi hawa wana taratibu zao, wana safari zao za ndani na za nje. Sisi tumewatengea fedha kwa ajili ya kuhudumia safari zao na

shughuli zao kama serikali, kwetu sisi tumewatengea pamoja na zile tulizohaulisha ilikuwa ni bilioni 8,1. Lakini tumesema hivi, nataka nieleze Mhe. Mwenyekiti, nifahamike. Tumesema hivi, katika fedha hizi za viongozi asilimia 40 zinatumiwa na Mhe. Rais, asilimia 25 na 25 zitatumiwa na Mhe. Makamu wa Kwanza na Mhe. Makamu wa Pili na asilimia 10 zitatumiwa na wastaafu. Sasa ukiniuliza mimi nani katumia ngapi, kiungwana na kiheshima sidhani kama utakuwa ni utaratibu muafaka wa kusema mwaka jana nani katumia ngapi, mwaka huu nani katumia ngapi, haitaleta sura nzuri kwa wakuu wetu.

Lakini ukizitaka Mhe. Jussa hizo taarifa hawa viongozi wote wana wahasibu wao, kwa sababu gharama za safari zao zinategemeana na *needs* za safari zile. Mwaka jana wa bajeti sio huu tunaomalizia, Makamu wa Kwanza alikuwa mgonjwa, safari nyengine sio za kwenda kutembea tu ni safari za matibabu, mwaka huu Makamu wa Pili alikuwa mgonjwa. Sasa utakapokuwa unazungumza ma-*figure* tu bila ya kutazama chimbuko ya zile safari mantiki yake ni nini, utakosea. Mimi namuomba sana Mhe. Jussa tulizotumia ni hizo lakini kwa mpangilio ambao tumeupanga 40, 25, 25, 10, lakini ikitokea dharura basi hata huo mnyumburiko wengine utakuwa uko juu zaidi na wengine utakuwa uko chini zaidi kulingana na hali halisi kama nilivyoelezea, sisi sote ni binadamu na dharura nyengine lazima tutatumia. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo yake, lakini nitofautiane naye kidogo. Mimi nadhani taswira nzuri kwa wananchi itapatikana kama wakijua uwazi wa pesa zao na wala sidhani kama Wazanzibari wana shida ya kuwahudumia viongozi wao hawa. Kwa sababu sote tunatambua kama ni viongozi wakuu na bila shaka madhali wamewekwa wanahitaji kuhudumiwa, na shughuli za safari ni sehemu ya shughuli zao muhimu.

Sasa nadhani kwa misingi ya kulinda uwazi na uwajibikaji wananchi hawa Wawakilishi wao ni sisi na wanapata taarifa kupitia sisi Wawakilishi wao. Kwa hivyo, nadhani *actually* kwa majibu ya Mhe. Waziri kukionekana kwamba kuna kitu hatutaki kukiweka wazi ndio tutawatia wasiwasi wananchi, lakini tukiweka wazi wananchi wataondokana na wasiwasi. Nashukuru kanipa *figure* ya bilioni 8.1 kwa mgao ule aliyosema wa asilimia 40, 25, 25 na asilimia 10. Lakini Mheshimiwa yale yalikuwa ni makadirio mimi ninachoomba ni yale matumizi halisi, ilikuwa nadhani na kwa sababu wanaweka mfumo mzuri, na wametwambia wenyewe katika bajeti zao wana *IFMS* hawa kila kitu kinachotumika kinajirikodi kwenye kompyuta kinajulikana. Kwa hivyo, ilikuwa ni kwenda kubonyeza kwenye kompyuta tu akatuletea leo *figure* halisi kwamba Mhe. Rais katumia kiasi kadhaa sio

makadirio, alichotumia, Mhe. Makamu wa Kwanza katumia kiasi kadhaa, Mhe. Makamu wa Pili katumia kiasi kadhaa.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema wao wanahudumiwa na wananchi kupitia fedha za walipa kodi na ni muhimu wananchi wakajua. Mimi nimestaajabu leo katika maelezo yake kanipa maelezo marefu kuhusu malengo ya safari, mimi sikuhoji wala sijasema kama kuna nia mbaya, nilitaka kujua tu kama matumizi mengine na hilo nimetaka kujua kwamba mchanganuo wa viongozi watatu ukoje. Nadhani kwa kulitendea haki Baraza hili kwa ajili ya kuwatendea haki wananchi wa Zanzibar ambao ndio wanaowahudumia viongozi hawa, ilikuwa ni muhimu serikali kuweka wazi takwimu hizi ili wananchi wa Zanzibar wakazijua. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali kwamba matumizi ya kiongozi tumepanga kwa asilimia, kuna asilimia 40 kwa Rais, asilimia 25 na 25 kwa Makamu wa Kwanza na wa Pili wa Rais na asilimia 10 kwa wastaafu. Sasa akitaka mnyumburuko wa hali halisi hapa sinao, na ndio maana nikasema kwamba anaweza akaenda kwa wahasibu *private office* kwa ofisi hizi wakamuonesha ya mwaka jana, mwaka huu, na mwaka juzi zote anaweza akapewa akaweza kulinganisha. Namuomba kama atazihitajia, kama zitamsaidia basi ofisi za *private* zinaweza zikamsaidia, lakini kwangu mimi nimetakiwa kuangalia huo mgao wa 40, 25, 25, 10.

Kifungu 2201 Idara ya Bajeti	18,171,121,000/-
Kifungu 2202 Chuo cha Uongozi wa Fedha	1,800,000,000/-
Kifungu 2203 Bodi ya Mapato *ZRB* Ofisi Kuu	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hapa kidogo mimi ni mfanyabiashara ionekane kabisa kwamba ni mfanyabiashara na huwezi kudharau dafu kwa embe ya msimu. Dafu siku zote linapatikana juu ya mnazi, embe mwaka hadi mwaka ndio izae. *ZRB* imekuwa ikihangaika sana kutafuta mapato kila chochoro na kila kona, tuko mimi na wenzangu tunafanya biashara ya magari na kwa mwezi tunalipa karibu shilingi milioni 50 au 60 kutoka *TRA* tu. Sasa Mhe. Waziri nilimwambia jana mfanyabiashara upepo unakokwenda ndiko anakoelekea; anieleze je, tuko tayari tuhame hapa tuelekeze nguvu zetu Tanzania Bara kwa ndugu zetu wa Tanganyika tukafanye kazi hiyo ili mapato hayo tuyapeleke kule kutokana na usumbufu? Mpaka jana umetokea magari ya wafanyabiashara yameachwa na biashara ni asubuhi jioni mapato. Mhe. Waziri nataka unieleze wewe ni fundi wa Kiswahili Mungu kakujaalia neema hiyo unajua kupanga, utueleze

wafanyabiashara hao waondoke kama wenzetu walivyoondoka kuelekea Tanzania Bara wakafanye kazi hiyo. Ni hayo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi wafanyabiashara nataka wasiondoke na wale walioko Bara nataka waje zao Zanzibar wawekeze Zanzibar ili mapato niyapate. Lakini kama kuna usumbufu wa Bandari na usafirishaji wa magari nadhani itabidi na hili nikae na Waziri anayehusika na Bandari na Waziri wa tawala za mikoa na Waziri wa Ardhi tuone tunafanyaje.

Sisi tukishindwa kupata suluhisho basi itabidi tumuombe Makamu wa Pili akae na sisi, niachie kidogo nimalize sikukuu hii ili tuone tutafanya nini. Lakini nataka Mhe. Jaku usiondoke, *you can not leave your home.* Mhe. Jaku usiondoke, na wewe *you have to encourage others* kuwekeza Zanzibar, usiondoke kabisa, tunahitaji hizo pesa kuwasaidia wananchi wetu, hizo hizo pesa wanazolipa kodi tunataka kupeleka hospitali, usiondoke ndugu yangu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kama Mawaziri wote wangekuwa kama hivi tungekuwa mbali nchi hii. Naam, "*Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni*". Mhe. Mwenyekiti, kutokana na huu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kusimama kunakuwa kurefu kuna sala ya taraweih, witri, *tahajjoud,* hebu anambie tusimame mpaka lini atupe muda.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nimesema hivi, aniachie kidogo nimalize sikukuu. Kwa sababu wakati wa sikukuu tunahitaji kukaa na familia zetu, ikimaliza sikukuu Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, anayeshughulika na Mji Mkongwe yupo, Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano yupo, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yupo na mimi ninayeshughulika na kodi nipo. Nitawapigia simu hawa tukutane maana yake sikukuu ya pili tumeandaa mkutano na Mhe. Waziri wa Afya, sikukuu ya nne tumeandaa mkutano na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa hivyo, sikukuu hizi mbili nimeziwekea mikutano hawa kidogo tusubiri tumalize sikukuu, wenzangu wawili watatu hao wameshanisikia mimi nitawapigia simu nita-*organize* mkutano, tutafanya mkutano wetu kama vile *concrete solution* halafu tutaona nini tunafanya katika suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima tuendelee.

Kifungu 2203 Bodi ya Mapato *ZRB* Afisi Kuu 8,410,000,000/-
Kifungu 2205 Mfuko wa Barabara

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, baada ya Mwenyezi Mungu kuwa wa mwanzo wa pili Wananchi wa Jimbo la Muyuni kufika hapa ndio sababu, na nitakuwa sijawafanyia haki, kule kuna wawekezaji karibu 10 mpaka 15 waliojenga hoteli tokea sijui tuseme ukoloni mpaka leo wanapigia kelele barabara Mhe. Naibu Waziri ni shahidi lakini jawabu inayopatikana hairidhishi. Mhe. Waziri nimshukuru alipokuwa akijibu suala hili alinisaidia pakubwa tu akanambia atakaa na wahusika wa barabara. Wapo hapa Naibu Waziri, Mhe. Waziri naomba unisaidie wananchi wa Jimbo la Muyuni wapate kusikia kazi ninayoifanya kama ni mtumishi wao.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja ni vipi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja yangu ni barabara haipitiki Jambiani hadi Kibigija; ndani kuna hoteli karibu nane za wawekezaji na wageni na wanachangia kodi zote nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa nafasi hii katika kumsaidia Mhe. Jaku Hashim kupata ufumbuzi wa suala lake. Mhe. Mwenyekiti, inawezekana ikawa labda Kiswahili hatujafahamiana vizuri na Mhe. Jaku, kwa sababu suala hili ni kama alivyoeleza imekuwa kilio cha mara nyingi na sisi kama serikali tumekuwa tuna desturi ya kumpatia majibu. Bahati mbaya kwamba majibu yetu hayamfurahishi lakini ndio majibu sahihi na ndio ukweli ulivyo.

Mhe. Jaku barabara anazozizungumzia ni barabara za ndani, na kama barabara za ndani bila shaka serikali ina usimamizi maalum kwa mujibu wa sheria za nchi, na sisi tumekuwa wazi kabisa kwamba barabara kubwa ndizo ambazo zinajengwa na wizara, barabara za ndani zitasimamiwa na halmashauri. Tulichomuomba Mhe. Jaku yeye kama kiongozi wa Jimbo akae na wenzake wa Halmashauri, sisi kama wizara tuko tayari kutoa msaada; kutoa vifaa, mafundi ili kufanikisha suala hili.

Sasa anachokihitaji Mheshimiwa tumwambie kama wizara tutakwenda kujenga barabara si jambo ambalo tunaweza kulitamka, na kwa kuzingatia mradi huu wa barabara kubwa ya lami serikali imejenga kutoka Paje mpaka Kigaeni Makunduchi, eneo iliyopita ni eneo hilo hilo na Jambiani. Sasa chombo hiki kinahimiza utaratibu mzuri wa matumizi ya fedha za wananchi, tunachokizungumza ni kwamba kwa upande wetu sisi kama wizara hatuna fursa ya fedha kwenda kufanya kazi hiyo, kwa maana kwamba hizo barabara ambazo zingepaswa kujengwa na halmashauri.

Kwa hivyo, mimi niendelee kumuomba Mhe. Jaku akae na wenzetu wa halmashauri, sisi kama wizara tuko tayari kutoa msaada wa vifaa, mafundi kwenda kujenga barabara hiyo anayoilalamikia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba aweke wazi kwamba ni vifaa gani ili wananchi wa Jimbo la Muyuni wakapata kusikia. Mimi anaweza akanambia kwa mdomo lakini wenyewe nao wasikie kuna wawekezaji akavitaja hapa kabisa kuweka *hansard* sawa, ni vifaa gani atasaidia ili na sisi kama Wawakilishi au Wabunge tujivute kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, vifaa tunavyokusudia hapa ni vile vifaa vinavyotumika katika harakati za ujenzi wa barabaraba, kwa maana ya kwamba mashine, kijiko, *wheel loader* la kushindilia, yeye cha msingi atusaidie mafuta na masuala mengine yanayostahiki katika utendaji wa kazi ili tuweze kwenda kupata eneo la kuchimba kifusi na uwekaji katika maeneo husika, sisi tukiwa tuna vifaa vyetu na mashine katika utandazaji na ushindiliaji wa maeneo hayo ili barabara iweze kupitika kwa hali nzuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa tathmini hayo madude yashachoka, tena ningemuomba akaenda akafanya tathmini lita ngapi za mafuta anazohitaji ili tukaliweka sawa suala hili. Ni lini atakwenda kufanya tathmini hiyo ili kuweka rikodi sawa?

Mhe. Mwenyekiti: Sasa kazi hiyo mimi nafikiri yeye ameomba hayo mafuta tathmini fanyianeni huko huko, mfuatilie Mheshimiwa wizarani. Haya tunaendelea.

Kifungu 2205 Mfuko wa Barabara 6,903,000,000/-
Kifungu 2206 Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wangu wa Fedha kwa majibu mazuri, ya ufasaha katika maeneo mengi na kwa kiasi fulani ameweza kujibu masuali mengi sana. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kidogo tu anitoe wasiwasi Mhe. Waziri, kwenye hotuba yangu kwa niaba ya kamati nilizungumzia suala la kumalizika kwa *Mastrer Plan* ya Fumba mwaka huu ambayo imekuwa ni hadithi ya kila mwaka. Suala hili nililizungumza hata wakati wa kamati yako Mhe. Mwenyekiti, tulipopitia bajeti ya wizara hii kwamba wizara itoe fedha kutoka katika eneo jengine ili fedha hizo zilizotengwa za shilingi 150 milioni ziongezeke kufikia karibu 600 ili *Master Plan* hii ya Fumba iweze kumalizika kabisa, mwakani tuzungumzie hadithi nyengine katika maeneo haya ya uwekezaji. Kwa bahati nzuri wizara tulikubaliana hilo, juu ya kutoa fedha

katika maeneo watakayoyafahamu wenyewe ili ziongezeke tumalize *master plan*.

Mhe. Waziri alivyokuwa akijibu alisema kwamba wana mpango wa kumalizia jambo hili, ni mpango gani. Na kwa sababu nilipoangalia kwenye bajeti ya maendeleo fedha zilizotengwa bado ni zile zile shilingi milioni 150 kinyume na makubaliano ya kwenye kamati yetu tuliyokuwa tumekubaliana na wizara yake. Sasa nataka atuhakikishie, aihakikishie Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, alihakikishie na Baraza lako tukufu kwamba *master plan* ile kwa mpango wowote aliokuwanao itamalizika katika kipindi hiki cha fedha. Mhe. Mwenyekiti, naomba atuhakikishie.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tuna utaratibu mzuri tu ndani ya serikali, kwamba taasisi ndani ya wizara fulani inapotengewa pesa kwa kazi fulani na ikiwa pesa zile hazijatosha tuna utaratibu wa kuhaulisha. Tumekubaliana kwamba *master plan* hii tuikamilishe, na wakati wa kamati ilipotembelea imekubali hivyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti wangu asiwe na wasiwasi. Nitalisimamia hili ili tuweze kuona kwamba hata kama hawa hawajapelekewa hizo pesa tutatafuta pesa ndani ya ofisi yetu tuweze kuikamilisha hii *master plan*.

Kuna mambo mawili hapa nataka nimwambie Mwenyekiti wangu awe nayo *in mind*, unaweza ukawa una pesa lakini muda ukawa ni mdogo. Hawa wanaoandaa *master plan* kama watatumia *master plan* kwa kutumia muda wa miezi 12 kukamilisha *fine*, wakisema wanataka miezi 13 maana yake mwaka huo anaouzungumza haitakamilika. Sijajua vipi na hawa wanaoandaa *master plan* wanataka muda gani, lakini wakitaka kutayarisha katika kipindi cha mwaka huu suala la pesa tutahangaika tukatafute, kwa sababu hata na mimi linanikera sana nataka maeneo ya Fumba na Micheweni yawe na *master plan* yawe yameshapimwa. Hilo nataka nimhakikishie kwamba tutalisimamia ili tuweze kuona kwamba linatekelezwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Isipokuwa ninachotaka kumwambia ni kwamba, wakati tulipokuwa tukipitia bajeti yake wenyewe watu wa *ZIPA* walituhakikishia kwenye Kamati kwamba wakizipata fedha mwaka huu wa fedha basi *master plan* hiyo itamalizika. Kwa hivyo, nawaomba wawapatie fedha watu wa *ZIPA* ili *master plan* hiyo iweze kumalizika. Naomba tuendelee Mheshimiwa.

Kifungu 2206 Mamlaka ya Uwekezaji Vitega
Uchumi Zanzibar 250,000,000/-

Jumla ya Fungu **44,794,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 45 – MFUKO MKUU WA SERIKALI

Kifungu 9101 Mfuko Mkuu wa Serikali	66,065,000,000/-
Jumla ya Fungu	**66,065,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 1001 -Idara ya Ukuzaji Uchumi	426,696,000/=
Kifungu 1002 -Idara ya Mipango ya Kitaifa Maendeleo ya Sekta na Kupunguza Umasikini	688,200,000/=
Kifungu 1003 -Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watenda Kazi	149,104,000/=
Kifungu 2001 - Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali	1,300,000,000
Jumla ya Fungu	**2,564,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	34,194,403,000/=
Kifungu 0701 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	40,000,000/=
Kifungu 0901 Idara ya Fedha za Nje	7,500,000,000/=
Kifungu 1301 Idara ya Uhakiki mali na Mitaji ya Umma	7,500,000,000
Jumla ya Fungu	**42,438,403,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu 1001 Idara ya Ukuzaji Uchumi	150,000,000/=
Kifungu 1002 Idara ya Mipango ya Kitaifa Maendeleo ya Sekta na Kupunguza Umasikini	4,419,800,000/=
Kifungu 1003 Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watenda Kazi	342,000,000
Jumla ya Fungu	**4,911,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ilivyokuwa kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha za Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI
Mswada wa Sheria ya Makisio ya mwaka 2013.

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Spika: Naomba sasa nimkaribishe tena Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutimiza wajibu wangu wa kikatiba chini ya kifungu cha 106 kinachomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha mswada wa Sheria ya Matumizi kila mwaka wa fedha unapoanza.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kubwa naomba sasa kwa ruhusa yako niwasilishe mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Shilingi bilioni mia sita na hamsini na nane, milioni mia tano na ishirini na sita laki tano na ishirini na nane elfu kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni mwaka 2014 na kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, tumefikia hatua hii baada ya kazi kubwa na ngumu ya kupitia, kujadili na hatimae kuidhinisha mapendekezo ya bajeti awali ya Serikali na hatimae za wizara zote. Naomba nikiri kuwa kazi hii haikuwa nyepesi, na

Baraza lako Tukufu limefanya kazi kubwa ya kuwakilisha wananchi, na Serikali yao nayo imetoa maelezo yaliyohitajika.

Mhe. Spika, kukamilika uidhinishaji wa bajeti zote hizo kunapelekea mswada huu wa makisio ya matumizi ambayo umedhamiria kutoa uwezo kwa Serikali kutumia kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina jumla ya shilingi bilioni mia sita na hamsini na nane, milioni mia tano na ishirini na sita laki tano na ishirini na nane elfu. Kati ya fedha hizo; shilingi bilioni mia tatu na hamsini na tatu milioni mia moja na saba ni kwa ajili ya kazi za kawaida, na shilingi bilioni mia tatu na tano milioni mia nne na kumi na tisa laki tano na ishirini na nane elfu ni kwa ajili ya kazi ya maendeleo.
Mhe. Spika, kupitishwa kwa mswaada huu kutaiwezesha pia Serikali kukopa ndani na nje kiasi cha fedha zilizotajwa kwenye kifungu cha 5.1 cha Mswaada pamoja na masharti yake kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni mwaka 2014.

Mhe. Spika, mswaada huu una vifungu 9.

Kifungu cha 1 kinazungumzia jina fupi.

Kifungu cha 2 kinatoa tafrisi

Kifungu cha 3 kinazungumzia utoaji wa shilingi bilioni mia sita na hamsini na nane, milioni mia tano na ishirini na sita laki tano na ishirini na nane elfu. Kati ya fedha hizo shilingi milioni mia tatu na hamsini tatu, milioni mia moja na saba kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Kifungu cha 4 kinazungumzia Makadirio ya Fedha zilizokubalika.

Kifungu cha 5 chenye vifungu vidogo vinne kinazungumzia uwezo wa kukopa wa Waziri mwenye dhamana ya fedha.

Kifungu cha 6 Chenye vifungu vidogo vitatu kinazungumzia uwezo wa Waziri katika maombi ya ziada kwa lengo la kukabili matumizi mengine ya dharura pale haja itakapotokezea

Kifungu cha 7 Marejesho ya Mkopo na Riba

Kifungu cha 8 Kukubaliwa kwa mpango wa maendeleo

Kifungu cha 9 Kukubaliwa kwa fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ya mswaada, naomba sasa kwa idhini yako kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kuujadili na hatimae kuupitisha mswada huu ili uwe ni sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kama *formality* kuna hatua moja tumeiruka na ilikuwa ni kusema tu Mhe. Waziri kwamba Mswada huu usomwe kwa mara ya kwanza. Halafu hii ndio hatua ya pili tunafanyaje hii ndio *formality*. Mhe. Waziri ilipaswa kwanza usome ile *statement* ya mswaada huu kwamba umesomwa kwa mara ya kwanza na pili ndio inakuja hii.

Sasa labda nikurejeshe kidogo hebu toa hiyo *statement*.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba Mswada huu kusomwa kwa mara ya kwanza. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mswada umesomwa kwa mara ya kwanza. Sasa naomba tukubali Waheshimiwa Wajumbe usomwaji wa mara ya pili ndio yale maelezo aliyatoa mwanzo mkaunga mkono. Kwa hiyo, sasa hiyo iingie kwamba ni hatua ya pili alikwishaifanya, na mswada ukaungwa mkono kwa maana kwamba sasa uko tayari kuweza kujadiliwa.

Nadhani niseme tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba kazi hiyo mliyoifanya kwa muda wote kimsingi ndio ilikuwa mjadala wa mswaada huu hivi sasa, lakini kama kuna maneno mawili matatu ambayo mnataka kusema basi karibuni. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. Lakini kwa kifunpi sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniwezesha kuwa mchangijai wa mwanzo katika Makisio na Matumizi wa Bajeti. Mimi nilikuwa na jambo moja tu.

Kwanza niwashukuru sana watendaji pamoja na waandaaji wa mambo haya, lakini naona kidogo katika ofisi yangu wametunyika hapa. Katika utafiti niliofanya katika hili jadwedi la Muhtasari wa Makadirio na Matumizi kwa Kazi za Kawaida na Maendeleo 2012/2013 hapa kuna kasoro kidogo nimeiona katika fungu la 16 Baraza la Wawakilishi. Tuna mahesabu hapa ya kumi na nne bilioni, milioni mia nane na hamsini na mbili elfu katika matumizi ya kawaida.

Lakini tukija katika matumizi ya maendeleo kuna milioni mia sita tisini na saba laki tano na thalathini na sita. Tukijumlisha maeneo yote haya mawili *total* ilioko hapa ni bilioni kumi na mbili, usahihi ni bilioni kumi na tano milioni mia tano na arubaini na tisa laki tano na thalathini na sita elfu.

Mimi mchango wangu ilikuwa ni kuchangia hilo lakini mengine yote nakubaliana nayo. Naunga mkono hoja, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kama ulivyosema kwamba huu mswaada kwa kweli haupaswi kujadiliwa sana kwa sababu ni mswaada wa kupitisha. Kwa sababu haya tunayoyapitisha kwenye bajeti yote. Ila mimi nina tatizo moja Mhe. Spika, kwamba hapa tunaruhusu bilioni mia sita na hamsini na nane, mia tano na ishirini na sita milioni, mia tano na ishirini na nane elfu ndizo ambazo tunazoziruhusu hapa Serikali ikazitumie kwa maslahi ya watu.

Lakini tunapokuwa tuna *review* hii bajeti utekelezaji wake au hata wakati wa kupitisha bajeti mwaka ukimaliza kinachoripotiwa na Mawaziri hapa sio hiki tulichokipitisha kinakuwa na mapungufu mengi, hakuna hata wizara moja inayotumia bajeti hii asilimia mia kwa mia ambayo tumeiruhusu.

Sasa wasiwasi wangu isijekuwa tunawadanganya Wazanzibari kwamba tunatumia *figure* hii lakini si kweli. Kama kuna maelezo kidogo naomba sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa waliochangia mswada huu. Lakini vile vile nataka kuwashukuru wale ambao hawakuchangia ni kwa sababu tu wanaona mambo yamekaa vizuri nawashukuru sana.

Hoja ambayo ameeleza Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa tutaangalia hiyo *total* kama ina makosa basi tutairekebisha ili iendane na hiyo *total* ya Baraza la Wawakilishi.

Lakini vile vile Mhe. Abdalla Juma Abdalla nataka niseme tu kwamba haya tunayoyaleta hapa ni makisio. Tunakisia kwamba Serikali yetu katika mwaka huu wa Bajeti itatumia kiasi fulani.

Mwenyezi Mungu anapotujaalia mapato yetu yakawa kama tulivyotarajia tutatumia hii asilimia mia ambayo tumeipendekeza hapa na tumeipitisha. Mwenyezi Mungu akitujaalia kwamba tumepata mapato mengi zaidi na

tunahitajia kutumia zaidi tutalazimika Serikali kuja kuomba *supplementary* hapa.

Kwa hivyo, haya ni makisio na ndio maana utaona katika maelezo yangu nimeeleza kwamba *ZRB* katika makusanyo ambayo walitarajia hawakufikia asilimia mia moja. Kwa hivyo, na kule kwenye mawizara nako hakuna mafungu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nataka niwashukuru sana Waheshimiwa wa Baraza lako Tukufu. Nataka nikushukuru wewe mwenyewe kuongoza hivi vikao, naomba vile vile nitoe hoja ili tufunge huu mjadala.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja imeamuliwa na Kuafikia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya kutunga sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Mwaka 2013

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi
Kifungu 2 Tafsiri
Kifungu 3

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa anatoa maekezo kuhusiana na hoja yangu alisema kwamba ataiangalia. Tayari katika jadweli ambalo liko huku linaonesha kwamba kuna mapungufu, huku kuna idadi ya bilioni kumi na nne na milioni mia sita na ushee, lakini katika jumla kuu kana bilioni kumi na mbili.

Sasa akisema kama tutaangalia ina maana kwamba idadi kamili ya fedha zilizoombwa haijatimia. Naomba maelezo ya ziada katika hili ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani nilisema katika maelezo kwamba hii tutaijumlisha tuone usahihi huo wa takwimu halafu tutairekebisha na itakuwa ni jumla tu alivyojumlisha ile kumi na nne katika Baraza la Wawakilishi.

Kifungu cha Baraza la Wawakilishi ukijumlisha kumi na nne na hii inayosema laki sita hiyo ni *printing error*. Kwa hivyo, tutaijumlisha hii tutapata usahihi wake tutaiweka hapa asiwe na matatizo, mimi nimeshajumlisha ni *printing error* tu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri hoja ya Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa tumeipata. Kwamba kwenye kawaida pale kuna bilioni kumi na nne na wakati kuna sehemu ya maendeleo kuna kama milioni mia sita na sitini na saba. Sasa jumla yake imeandikwa bilioni 12 *of course* hayo ni makoseo.

Sasa kumbe ilikuwa tuchukue bilioni kumi na nne na ile milioni mia sita tisini na saba uzijumlishe ndio inakuja usahihi sasa. Nafikiri tumeona hiyo hoja yenyewe. Kwa hiyo, nadhani ni suala la kujumlisha hapa limekuja vibaya ambalo Mhe. Waziri amekiri.

Kifungu 3 Utoaji wa shilingi bilioni mia sita hamisni na nane miliojni mia tano ishirini na sita, laki tano ishirini na nane elfu kutoka Mfumo Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Kifungu 4 Makiso ya Fedha zilizokubalika

Kifungu 5 Uwezo wa Waziri Kukopa

Kifungu 6 Uwezo wa Waziri wa Maombi ya Wizara

Kifungu 7 Marejesho wa Mkopo na Riba

Kifungu 8 Kukubaliwa kwa Mipango ya Maendeleo

Kifungu 9 Kukubaliwa kwa Fedha zilizopitishwa kwa Matumizi ya Maendeleo.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya marekebisho, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja imeamuliwa na Kuafikia)

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa mswada wa Sheria ya Makisio ya Mwaka 2013 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja imeamuliwa na Kuafikia)

KAULI ZA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na hali ya uzima ambayo imetuwezesha kukutana leo hii katika mkutano huu.

Mhe. Spika, Aidha nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kunipa fursa ya kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, shukurani za pekee zimuendee Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuniagiza kuwasilisha rasmi ripoti hii ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu katika Baraza lako tukufu mara tu baada ya kuipitia ripoti hiyo. Jambo ambalo linazidisha ari, nguvu na kasi ya kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora kutokana na maelekezo yake anayonipa ya mara kwa mara.

Mhe. Spika, vile vile napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa utekelezaji wa majukumu yake katika kudhibiti rasilimali za umma na kuhakikisha kuwa udhaifu, dosari na kasoro zote zinazojitokeza katika uwekaji wa hesabu na utumiaji wa fedha na mali za serikali zinaonekana. Bila ya kuwasahau watendaji wote wa taasisi hiyo, kwani ushirikiano wao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ndio chanzo cha mafanikio haya.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kukubali kuipokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, aidha, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, ndugu yangu Mhe. Omar Ali Shehe na ni Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chake Chake, pamoja na Wajumbe wake wote kwa umahiri, na umakini mkubwa wanaofanya katika kuhakikisha kuwa ripoti zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinakuwa katika mstari ulionyooka, pamoja na mashirikiano yao ya hali ya juu katika kufanikisha hilo.

Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mhe. Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anawajibika kikatiba na sheria nyengine za Zanzibar, kukagua hesabu za taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mashirika ya Umma, na baadae kutoa taarifa za ukaguzi kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi ya mapato na matumizi ya fedha na kuonesha udhaifu au dosari na kasoro zote katika uwekaji wa hesabu, pamoja na kasoro zilizojitokeza katika udhibiti na utumiaji wa fedha na mali za serikali. Lengo ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwajibikaji na uwazi katika mapato na matumizi ya fedha na mali za umma, pamoja na kuhakikisha kwamba ufanisi na tija zinapatikana kwa kila rasilimali inayotumika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wake.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 112(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo.

a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa, na iwapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanayotokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo.

c) Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hesabu za Mahakama zote za Zanzibar na Hesabu za Tume au vyombo vyengine vinavyohusika na Baraza la Wawakilishi.

Mikakati ya Kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mhe. Spika, suala la mafunzo kwa wafanyakazi limeendelea kupewa kipaumbele ili kupata ufanisi katika udhibiti wa matumizi ya rasilimali za umma. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, ofisi imeendelea kutumia miongozo mbali mbali ya kiukaguzi, yaani *Regulatory Audit Manual Performance Audit, guidelines IPS, ISSAI* kwa lengo la kufanikisha ukaguzi wa hesabu ambao unakwenda sambamba na miongozo ya ukaguzi inayokubalika na Jumuiya za Ukaguzi Kitaifa na Kimataifa. Yaani INTOSAI na NBAA.

Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na sheria nyengine za nchi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeendelea kutoa huduma zake za ukaguzi wa hesabu kwa taasisi za serikali, yakiwemo mashirika mbali mbali pamoja na hesabu za Halmashauri za

Wilaya katika Mikoa kwa Unguja na Pemba, pamoja na baadhi ya miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo mbali mbali pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa upande wa kazi ya ukaguzi wa hesabu za viinua mgongo pamoja na fidia. Ofisi imepokea majalada 1846 ya wastafu na wafanyakazi walioumia kazini, ambapo majalada 980 yamekaguliwa kwa ajili ya mafao yanayolipwa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na majalada 866 ya wastaafu yamekaguliwa kwa ajili ya mafao yanayolipwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yaani *ZSSF*.

Tathmini ya utekelezaji wa ripoti iliyopita ya mwaka 2010/2011. Mhe. Spika, katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba serikali imetekeleza mapandekezo na ushauri uliotolewa katika ripoti ya mwaka 2010/2011. Serikali kupitia taasisi zake imeendelea kufuatila hoja na mapendekezo yaliyotolewa. Hata hivyo, kuna haja kubwa ya kuongezwa juhudi za ufuatiliaji na uwajibikaji ili kupunguza au kuondoa kabisa mapungufu ya kihesabu, kisheria na kiutendaji yaliyobainika katika taasisi zilizokaguliwa.
Katika uwasilishaji wa hesabu ya mwaka ya mwaka wa fedha 2011/2012, ofisi imebaini kuna mafanikio makubwa ya uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa wakati kwa kasma za mawizara na taasisi zinazojitegemea. Kwa upande wa mashirika ya serikali pamoja na Halmashauri za Wilaya, bado kuna tatizo kubwa la kutowasilishwa kabisa au kwa wakati hesabu za mwisho wa mwaka, ambapo ni kinyume na sheria za fedha. Aidha, hali hii inapelekea mashirika mengi na Halmashauri za Wilaya kutojulikana mwenendo wao mzima wa utendaji pamoja na rasilimali zinazomilikiwa na mashirika hayo na halmashauri hizo za wilaya.

Upeo na Madhumuni ya Ripoti ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetoa aina mbili za ripoti, ripoti hizo zimekusanya taarifa za ukaguzi wa hesabu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, yakiwemo mawizara na taasisi mbali mbali za serikali inayojumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuzingatia taratibu zilizopangwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na utekelezaji wa miradi ya wahisani, ikiwemo miradi ya kilimo, ujenzi, maji na miradi mingine ya maendeleo.

Kiwango cha Uwekaji wa Hesabu za Serikali

Mhe. Spika, kumekuwa na mabadiliko makubwa katika uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, pamoja na udhibiti mzuri wa rasilimali za umma

kwa baadhi ya taasisi za serikali. Hata hivyo, bado jitihada zaidi zinahitajika kwa baadhi ya taasisi za serikali katika kuimarisha uwekaji mzuri wa kumbukumbu za hesabu, pamoja na utunzaji wa rasilimali za umma.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inaendelea kutoa ushauri na miongozo kwa taasisi mbali mbali za serikali; juu ya kuimarisha viwango vya uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, pamoja na uhifadhi wa udhibiti wa rasilimali za umma.

Mambo Yaliyobainika katika Ukaguzi wa mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 hali ya uwekaji wa kumbukumbu za hesabu katika taasisi mbali mbali za serikali imeimarika. Hata hivyo, kumejitokeza baadhi ya dosari za kiutendaji ambapo hoja mbali mbali za ukaguzi zilizotolewa kuhusiana na dosari hizo ziligundulika, baadhi ya hoja hizo zilipatiwa ufumbuzi kwa kurekebishwa na kutolewa ufafanuzi pamoja na maelezo yaliyokosekana wakati wa ukaguzi.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa kuna udhaifu na matatizo katika masuala ya ufungaji wa uwasilishaji wa hesabu kwa baadhi ya mashirika, halmashauri za wilaya na kuendelea kuwepo kwa malimbikizo ya madeni wanayodai au kudaiwa baadhi ya taasisi za serikali, vikosi maalum na kutofuata kikamilifu sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2005 na kanuni zake. Vile vile kumebainika kukosekana kwa baadhi ya vielelezo muhimu katika ukusanyaji mapato na matumizi ya serikali ikiwemo mikataba ya ujenzi, mikataba ya ukodishwaji wa ardhi na mikataba ya utoaji huduma mbali mbali kwa taasisi za serikali.

Vile vile baadhi ya miradi ya ujenzi wa majengo ya ofisi za serikali haikuweza kukamilika kutokana na sababu mbali mbali zilizotolewa na watendaji ikiwemo upatikanaji wa fedha kwa wakati. Kutowepo kwa usimamizi mzuri pamoja na ukiukwaji wa sheria na taratibu za manunuzi. Hali hii inasababisha hasara kubwa kwa serikali kwa vile fedha nyingi zimetumika kugharamia miradi hiyo ambapo malengo na tija havikupatikana kikamilifu.

Ukaguzi Yakinifu

Mhe. Spika, ukaguzi yakinifu ulifanywa kupitia miradi mbali mbali ya serikali, ikiwemo miradi ya ujenzi wa barabara, miundombinu ya maji safi na salama, vituo vya afya, ujenzi wa madarasa na huduma mbali mbali za elimu, pamoja na miradi ya ujenzi wa ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ukaguzi umebaini kuwa miradi mingi haikuweza kufikia lengo lililokusudiwa

kulingana na fedha zilizoingizwa na kutumika. Aidha, baadhi ya miradi ya ujenzi wa majengo ya ofisi za serikali haikuweza kukamilika kabisa. Hali hii inasababisha hasara kubwa kwa serikali, kwa vile fedha nyingi zimetumika kugharamia miradi hiyo ambapo malengo na tija havikupatikana.

Ukusanyaji wa Mapato ya Kawaida

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, kumekuwa na ukusanyaji mzuri wa mapato na kukusanya jumla ya Tsh. bilioni 262,824,308,000, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 43,739,308,000 sawa na asilimia 16.7, ukilinganisha na mwaka uliopita wa 2010/2011, ambapo zilikusanywa jumla ya shilingi bilioni 219,085,000,000. Aidha, imeonekana bado kuna fursa nzuri ya kukusanya mapato zaidi iwapo jitihada ya makusudi itachukuliwa katika kuibua na kuimarisha vianzio mbali mbali vya mapato ya ndani.

Ukaguzi umebaini kwamba katika maeneo mengi ya taasisi za serikali kama vile vikosi vya SMZ, Halmashauri za Wilaya, mabaraza ya miji, sehemu za maliasili, vyombo vya habari mbali mbali na utalii bado kuna udhaifu wa udhibiti na ukusanyaji wa mapato, ukiimarishwa, utachangia kuongezeka kwa kiasi kikubwa kiwango cha mapato ya ndani.

Matumizi ya Kazi za Kawaida

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, serikali ilijipangia kiasi cha Tsh. bilioni 233,743,399,000 kwa matumizi ya kawaida kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, ambapo shilingi bilioni 233,883,458,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi mbali mbali za kawaida, ambayo hiyo ni zaidi ya asilimia 100 ya makadirio.

Matumizi ya Maendeleo;

Mchango wa Serikali

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, serikali ilijipangia kutumia kiasi cha shilingi bilioni 38,127,642,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, ambapo shilingi bilioni 34,171,302,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi mbali mbali za maendeleo, sawa na asilimia 89.7 ya makadirio.

Mchango Kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo

Kwa mwaka 2011/2012 serikali ilijipangia kupata kiasi cha shilingi bilioni 342,256,329,000 kutoka kwa wahisani wa maendeleo, kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo, ambapo shilingi bilioni 150,150,313,000 zimeingizwa

na kutumika kwa kazi mbali mbali za maendeleo, sawa na asilimia 56.2 ya makadirio.

Malengo ya Baadae

Mhe. Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tayari inaendelea kutekeleza mpango mkakati yaani *strategic plan* wa miaka mitatu, ulioanza mwaka 2011 na utakaomalizika mwaka 2014. Mpango mkakati huo umejikita katika maeneo ya kuimarisha ofisi kiutendaji pamoja na kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye taaluma mbali mbali zitakazosaidia kuimarisha kazi za ukaguzi.

Katika mpango mkakati huu ofisi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo.

1. Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.
2. Kushajihisha usimamizi, uwezo na uwajibikaji wa masuala ya fedha na mali za umma.
3. Kushirikiana na kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa taasisi zinazosimamia uwajibikaji, pamoja na kuimarisha mawasiliano na wahusika wengine wa ofisi.

Changamoto Ziliopo

Mhe. Spika, kazi za ukaguzi ni kazi ambazo zinahitaji utaalamu katika fani mbali mbali na watendaji wenye uaminifu na uadilifu wa hali ya juu. Ili kuongeza ufanisi katika kazi za ukaguzi na hatimaye kuwa na utawala bora katika matumizi ya rasilimali za umma, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imejipanga kupambana na changamoto hizo, kwa kuongeza viwango vya taaluma kwa wafanyakazi wake ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika kada za uhasibu, ukaguzi na nyenginezo, taaluma ambazo zitasaidia sana kuleta mafanikio na maendeleo katika ofisi na nchi kwa jumla.

Kwa upande wa Pemba ofisi bado inaendelea kuwa na ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi. Hali hii inasababisha wakaguzi kuendelea kutegemea kufanya kazi zao katika ofisi za wakaguliwa na kupelekea kutokuwa na uhuru wa kufanya kazi na hatimaye athari katika kazi za ukaguzi huenda zikatokea. Kutokana na hilo ofisi itaendelea kuimarisha ofisi yake iliopo Wete Pemba kadiri ya hali itakavyoruhusu. Aidha, ofisi inamiliki kiwanja eneo la Tibirinzi Chake Chake Pemba na ujenzi wa ofisi katika kiwanja hicho bado unasubiri maamuzi ya serikali.

Hitimisho

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, kwa umakini na umahiri wake wa kuiongoza nchi yetu ya Zanzibar.

Vile vile niwashukuru Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu Waheshimiwa Wawakilishi kwa umakini wao wa kufuatilia shughuli za serikali kwa ujumla.

Mhe. Spika, baada ya muhtasari huo, sasa kwa heshima na taadhima kubwa naomba kuwasilisha.

Mhe. Omar Ali Shehe: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*)): Mhe. Spika, kuanza hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu ni jambo linalostahiki kipaumbele cha awali kutokana na neema yake ya kutujaalia afya njema na uwezo wa kuendelea kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi na nchi yetu.

Aidha, kipaumbele cha pili katika hotuba yangu hii, kabla ya kuzungumzia maudhui niliyoyakusudia ni kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, juu ya uwasilishwaji wa ripoti mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mbele ya Baraza lako hili tukufu. Tatu, nampongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa namna alivyoisimamia na kuiongoza Wizara hii muhimu sana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa aina ya pekee, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali, kutokana na mashirikiano makubwa wanayotupatia wakati wote wa kazi za Kamati.

Mhe. Spika, ripoti zilizowasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu muda mfupi uliopita na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni “Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2011/2012” pamoja na “Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012”.

Nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati ya *PAC* kumpongeza kwa dhati kabisa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hatua kubwa ya

kimaendeleo iliyoifikia hadi kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza hili tukufu ripoti mbili za ukaguzi ambazo nimezitaja hapo awali. Hatua hii ya kupigiwa mfano ya maendeleo ya ukaguzi wa hesabu za Serikali nchini ni kielelezo cha ukomavu wa Serikali yetu katika utekelezaji wa mikakati ya Utawala Bora, kwani ni ukweli usiopingika kuwa matumizi sahihi ya fedha na rasilimali za umma ndiyo yatakayolisaidia taifa hili katika kijikwamua na umasikini na kupiga hatua za kujiletea maendeleo endelevu.

Mhe. Spika, pamoja na Ripoti hizo kukabidhiwa Baraza hili, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) inayoundwa na Kanuni ya 106(g) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012 na inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Uwezo na Majukumu ya Kamati hii ambayo yameelezwa na Kanuni ya 118(2) kama ifuatavyo:

a) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
b) Kuchambua na kutafakari ripoti yoyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale ambapo Rais aliagiza ukaguzi huo ufanywe.
c) Kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali na asasi zake.
d) Itatoa taarifa yake baada ya kufanya uchunguzi kuhusiana na matumizi ya ziada ya fedha iliyotolewa kwa mwaka wa fedha unaohusika.
e) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

Ni wazi kwamba, kwa msisitizo wa kanuni ya hapo juu (ya 118(2)(a), Kamati ya *PAC* ina dhima ya kuzifanyia kazi ripoti hizo na kuwasilisha taarifa yake mbele ya chombo hichi cha wananchi kwa niaba ya wananchi.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kwa kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika. Na napenda shukurani hizo ziwafikie moja kwa moja kwa kuwatambua kama ifuatavyo:

1. Mhe. Omar Ali Shehe - Mwenyekiti.
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Mjumbe
4. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Mjumbe
5. Mhe. Rufai Said Rufai - Mjumbe

6. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Mjumbe

Aidha, shukurani zangu pia ziwe kwa Makatibu wa Kamati yetu, nao ni vyema nikawatambulisha kwako Mhe. Spika kama ifuatavyo:

1. Ndg. Asma Ali Kassim; na
2. Ndg. Othman Ali Haji.

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar, imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na majukumu yake yameelezwa katika kijifungu cha (3) cha kifungu hicho kama haya yafuatayo:

a) Kuhakikisha kwamba, fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria, na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe;

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo, na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoelezwa hapo juu, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeanza zoezi maalum la uhakiki wa mishahara kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kufuatia zoezi hilo, Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Afisi ya Mdhibiti kwa kuanza zoezi hilo kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa hakika huo ni mwanzo bora hasa tukitilia maanani kuwa elimu ndiyo msingi na nguzo imara ya maendeleo ya jamii na Taifa lolote.

Ni imani yetu kuwa, mwanzo huo mzuri ulioanzwa na Afisi hii utaendelezwa kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali, na mimi kwa niaba ya Kamati, naomba nimuombe Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwamba akimaliza ukaguzi wa Mishahara katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya pili iwe ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi msisitizo tukiweka katika Vikosi vyote vya SMZ.

Ripoti za ukaguzi za mwaka 2011/2012 bado zinaonesha ukiukwaji mkubwa wa sheria katika matumizi ya fedha za Umma

Mhe. Spika, sasa naomba nianze na muhtasari wa uchambuzi wangu wa Ripoti hizo mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za mwaka 2011/2012, kwa kuzungumzia suala zima la ukiukwaji wa sheria za fedha katika matumizi ya fedha za umma, Kamati yetu inasikitishwa kuona kwamba bado watendaji wa taasisi za umma, wanaendelea kukiuka taratibu za matumizi ya fedha za umma zinazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi na taratibu zilizowekwa ndani ya sheria zilizopitishwa na chombo hichi.

Mhe. Spika, suala la kutofuatwa kwa sheria ya fedha na sheria ya manunuzi katika ripoti hizi, limegusa takriban katika maeneo mengi ndani ya taasisi za umma na sekta binafsi hasa katika maeneo ya uwekezaji.

Mhe. Spika, Uwasilishaji wa Ripoti hizi umekuja sambamba na kufikia ukingoni kwa kazi ya Baraza hili ya kuiruhusu Serikali kukusanya na kutumia fedha ambazo z itatokana na kodi za wananchi wanyonge wa nchi yetu. Baraza lina wajibu wa kuiidhinishia serikali kukusanya na kutumia, lakini pia lina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba fedha tunazoziidhinisha zinatumika kama tulivyoziidhinisha, kwa malengo na kwa kiwango kama kilivyokubalika ndani ya chombo hichi. Tutakapokwenda kinyume na hayo Mhe. Spika, tutakuwa tunafanya kosa kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya wananchi waliotuleta humu kwa lengo la kuwasemea, kuwatetea na kulinda rasilimali zao katika nchi yao.

Mhe. Spika, mimi binafsi na wanakamati wenzangu tulidhani kuwa vitendo vya ukiukwaji wa sheria na taratibu vitakuwa vikipungua kwa kasi kadiri siku zinavyokwenda, lakini kupitia ripoti hizi Waheshimiwa Wajumbe mtakuwa ni mashahidi kuwa, tumekuwa na maendeleo ya ukaguzi, lakini hakuna mabadiliko katika kupungua kwa kasi ya ukiukwaji wa taratibu za matumizi ya fedha za umma. Waheshimiwa Wajumbe, kwa maslahi ya kulinda kodi za wananchi, tunapaswa tujiulize na tupate jibu, ni kitu gani kinachosababisha hali hii? Tunapaswa pia tujiulize tatizo liko upande wetu Wawakilishi

kwamba tumeshindwa kusimamia ipasavyo serikali au tatizo liko kwa serikali kuwa haitaki kusikiliza ushauri na mapendekezo ya Wawakilishi? *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba tukumbushane majukumu ya vyombo vyetu vilivyopo kwa mujibu wa Katiba na Sheria zetu. Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mbali ya kazi ya kudhibiti matumizi, kazi yake kubwa ni kufanya ukaguzi na kuwasilisha Barazani matokeo ya kazi yake ya ukaguzi kama anavyofanya leo.

Mamlaka ya Baraza kupitia Kamati yake ya *PAC* ni kuchunguza yatokanayo na ripoti ya Mdhibiti na hatimaye kuwasilisha Barazani maoni na mapendekezo yake. Kwa mantiki hiyo, mamlaka ya Baraza kama chombo cha kusimamia utendaji wa shughuli za umma hatimaye ni kuagiza serikali kama chombo cha utendaji kwa hatua na utekelezaji.

Mhe. Spika, kwa mtiririko huu wa kimamlaka tutaona kwamba kila mmoja kati yetu, yaani Mdhibiti, Baraza kupitia *PAC* tunaendelea kufanya kazi kwa mujibu wa mamlaka tulizonazo, lakini tatizo liko kwa upande wenye mamlaka ya uchukuaji wa hatua na utekelezaji. Iwapo serikali itashindwa kuwajibika kwa kuwakemea, kuwachukulia hatua za kinidhamu na kijinai, kuwafilisi mali zao watendaji wanaofuja fedha za kudangadanga za wananchi wetu masikini, kazi yote ya Mdhibiti na Kamati ya *PAC* itakuwa haina maana yoyote na itakuwa ni eneo jengine la kufisidi fedha za wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni wazi kwamba serikali yetu kama ingelikuwa makini, ilitosha kuwapa nafuu kubwa wananchi wake dhidi ya gharama za maisha, kutokana na ukweli kwamba, ina vianzio vingi vya kujipatia mapato. Lakini kwa uzembe na kutowajibika kwa watendaji wake walio wengi, ndio maana hata Wawekezaji mbali mbali wa Mahoteli hapa Zanzibar, wanaendelea kuitafuna nchi hii kiuchumi, huku faida inayobakia ya utalii huu, kupita Miradi hii ya Mahoteli, huwanufaisha wageni hao na wengine, na wazanzibari hubakishwa kuimbishwa nyimbo wasiyoijua, ya "*Utalii kwa wote*!" *(Makofi)*

Serikali Kuiwezesha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu:

Mhe. Spika, Baraza lako litakubaliana na mimi kwamba, ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi mbali mbali hususan miradi inayohusu ukodishwaji wa ardhi kwa wawekezaji, unahitaji ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Na ni wazi kwamba, katika sehemu yenye migogoro mikubwa katika nchi hii ni suala zima la ardhi, lakini zaidi ardhi inayohusika na miradi mbali mbali ya kitalii.

Mhe. Spika, kwa Maofisa wa kawaida wanaomsaidia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kufanya kazi ya ukaguzi katika mahoteli mbali mbali na

kuonesha udhaifu mbali mbali unaojitokeza katika miradi hiyo ya Mahoteli pamoja na kuwa jasiri katika kuionesha serikali wapi inakosea katika ukusanyaji mzima wa mapato. Kwa kweli, bila ya shaka ni suala sio tu linalohitaji uzalendo na mapenzi ya nchi na serikali yao, lakini serikali hii inapaswa izingatie kwa makini suala la kuongeza maslahi ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la ukaguzi na zaidi wa thamani halisi ya fedha (*value for money*), linahitaji utalaamu wa fani mbali mbali. Jambo hili linapaswa litizamwe kwa makini, kwa kuongeza wataalamu katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, lakini pia kwa kuongeza mafunzo kwa Kamati yetu ya *PAC*, ili Wajumbe wake waweze kufuatilia na kuichunguza ipasavyo miradi yote iliyohusika na ripoti hii.

Mhe. Spika, kamati yetu katika kufanya kazi hizi, kwa namna yoyote ile, inahitaji kupatiwa mafunzo na utaalamu wa sheria zinazohusiana na ardhi, ili tuweze kuifuatialia kwa karibu miradi ya mahoteli, kwani takriban yote imehusishwa na masuala ya ardhi na Mikataba inayohusiana na masuala hayo. Aidha, kamati yetu haiwezi kufanya kazi zake kwa ufanisi hususan kufuatilia ripoti hizi, bila ya ufahamu mkubwa wa namna ya thamani halisi ya fedha inavyoweza kukaguliwa na kuthibitishwa kwa mnasaba wa miradi mbali mbali iliyoainishwa na ripoti hizi.

Mhe. Spika, sambamba na hilo, kamati yetu inaendelea kuhitaji mafunzo juu ya ukaguzi wa fedha na sheria zinazohusiana na suala hili, ikiwa ni pamoja na Sheria za Manunuzi na zinazohusiana na ukaguzi mzima wa Hesabu za Serikali. Haya yote Mhe. Spika, hayawezi kupatikana wala tija kamili ya Kamati yetu haiwezi kufikiwa, bila ya Wajumbe na Makatibu Kamati wa Kamati ya *PAC*, kupatiwa mafunzo mbali mbali, ndani na nje ya nchi.
Kutokana na hali hiyo, naendelea kwa niaba ya Kamati, kusisitiza haja ya Kamati hii kupatiwa mafunzo na Serikali, ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Taasisi yoyote ya Serikali; Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hata na Afisi ya Baraza lako hili la Wawakilishi.

Mhe. Spika, napenda kukumbusha tu kwamba, kamati yetu sasa kwa kuzingatia ratiba ya kawaida ya kamati ndani ya mwaka hufanya kazi kwa wiki 8, basi kwa kamati hii sasa imebakia wiki 6, kwani wiki mbili za mwanzo za kikao cha mwezi wa sita tulikwishazitumia mwezi Mei mwaka huu kwa kufuatilia mambo mbali mbali yaliyojitokeza katika ripoti 5 za Mdhibiti tulizoziwasilisha katika Kikao cha Aprili.

Kwa hivyo, leo hii tunakabidhiwa Ripoti hizi mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ambazo zote zina hoja zinazohitaji uchambuzi na ufuatiliaji mkubwa na wa undani, ili tuweze kutoa ripoti yetu katika kiwango kinachotarajiwa katika kikao cha Aprili, 2014 ni lazima kamati yetu iongezewe muda wa kufanya kazi kinyume na kupewa wiki 6 (sawa na siku 30 tu za kazi), ambazo hata ripoti moja kati ya hizo haiwezi kukamilika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaishukuru serikali sasa kwa kukubali maelekezo ya Wajumbe wa Baraza hili, juu ya kuwepo kwa baadhi ya watendaji wanaoitia hasara Serikali, na ni sawa na kuwaingiza wananchi wa nchi hii katika hasara kubwa zaidi na umasikini usioweza kutokomezeka.

Mifano hii inapotolewa kwa mfano wa Ujenzi wa Jengo la Afisi ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Ujenzi wa *Terminal* mpya ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume; Unguja na matendo mengi maovu ya baadhi ya Watendaji hao, sio tu serikali kubakia kukiri, lakini hivi sasa imeshafika wakati wa watendaji hao waliohusika, sio tu kuchukuliwa hatua za kufukuzwa kazi kutokana na kuiingiza serikali na wananchi wake katika hasara, lakini pia wachukuliwe hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufilisiwa kwa mali zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunasikitika sana kwa serikali hii inayokiri kuwepo kwa matatizo mengi na udhaifu mkubwa wa baadhi ya viongozi na watendaji wake ambao sisi kamati pamoja na Kamati nyengine za Baraza hili, tumeeleza sana kupitia ripoti zetu mbali mbali. Kwa kweli, bado serikali hii hii inayopata uhalali wake kutokana na ridhaa za wananchi wake, bado inaendelea kupuuzia kuyatekeleza kwa kina mapendekezo ya kamati.

Hali hii sio tu kwamba inadhoofisha imani ya wananchi wetu dhidi ya serikali yao, lakini kwa kiongozi mwenye busara atazingatia sana tanbihi ya juzi ya Mhe. Asha Bakari Makame kwamba, Baraza hili likifikia wakati wa *backbenchers* kusema kwamba nao wanaweza, hali ya ushuari haitakuwepo tena! Na nahofia Mhe. Spika, Wajumbe wako tukaja kufika pahala tukaamua kutovitumia visu vyetu kwa mnyama asiyeliwa! *(Makofi)*

Mhe. Spika, na mimi niungane na tanbihi hiyo kwamba, serikali hii iyatekeleze mapendekezo ya Kamati ya *PAC* na Kamati nyengine za Baraza hili, kabla ya kufikia wakati huo wa Wajumbe hawa wa Kamati kwa ujumla wao, ambao ndio *backbenchers* kusema na sisi tunaweza kuiwajibisha serikali hii, ambayo hadi leo imeendelea kutia pamba za masikio, vizibo vya macho, na kuziba uwezo wa pua, kwa kutoona haja ya kuyatekeleza mapendekezo yetu ya Kamati kwa vitendo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sina dubi kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na kunivumulia kuimaliza hotuba yangu ambayo nimeisoma kwa hisia kali kama kawaida ya usomaji wangu wa hotuba zinazohitaji uwajibikaji wa serikali, lakini pia shukurani zangu ziwe kwa Wajumbe wote wa Baraza hili, ambao kama si ustahamilivu wao, basi ujumbe wangu nilioutoa kwa serikali, Wajumbe wa Baraza wote kwa ujumla wao kupitia hotuba yangu hii wasingeliweza kusikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda tena kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na kumtaka aendelee kutoa ripoti mbali mbali kwa wakati na ufanisi mkubwa. Aidha, nizishukuru taasisi zote za serikali na niziombe taasisi zote zile zilizohusika na Ripoti mbili hizi kwa mwaka 2011/2012, ambazo kamati yetu itazifikia kwa lengo la kupata ufafanuzi husika, zisichoke kuipokea kamati yetu na kuipa mashirikiano mema kwetu, kwani hatutekelezi majukumu yetu kwa utashi, bali ni kwa kuzingatia maelekezo ya Katiba na Sheria zetu za Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kwa uwasilishaji wa maoni haya ya kamati. Taratibu zinatutaka tukiona inafaa tuweze kupokea maswali mawili au matatu.

Lakini Waheshimiwa Wajumbe, kama mnavyojua kwamba ripoti hizi kimsingi hapa zimeletwa ili zipokelewe na hatimaye ziweze kufanyiwa kazi na kamati inayohusika kama Mhe. Mwenyekiti alivyosema. Kwa hivyo, sifikirii kama kuna maswali yoyote.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwa sababu tunafikia ukingoni kabla sijauliza swali langu naomba uniruhusu kutumia fursa hii, naamini niseme mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wenzangu, kwamba tukushukuru na kukupongeza kwa dhati kwa kazi kubwa unayoifanya kukiongoza kikao hichi kizito. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kila mtu ameona umakini, umahiri wako, hekima na busara zako na hatimaye tukaweza kumaliza salama kikao hichi kwa mafanikio makubwa mimi naamini.

Baada ya pongezi na sifa hizo Mhe. Spika, kama ulivyonitabiria nina swali moja tu kwa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba; kwa sababu ripoti hizi za ukaguzi wa Hesabu za Serikali zinazofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

zimekuwa zikitolewa mwaka hadi mwaka, na mengi yanabainishwa na baadaye kufanyiwa kazi na kamati za Baraza hili na pia ndani ya ukumbi huu kwa pamoja.

Lakini serikali haionekani kuchukua hatua zozote za kisheria na sio za kinidhamu kwa waliohusika na upotevu au matumizi mabaya ya fedha za umma. Je, Mhe. Waziri anadhani ipo haja ya kuendelea na kazi ya kufanya Ukaguzi huu. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Machamo Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, na mimi naomba nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kukiongoza kikao chetu hichi tangu mwezi wa Juni mpaka leo tarehe 5 Agosti, 2013 na Mwenyezi Mungu akipenda labda kesho tutafunga Baraza hili, yaani wewe pamoja na timu yako mumetuongoza vizuri.

Mhe. Spika, naomba kuuliza pamoja na kutoa ushauri. Tukiangalia kwa haraka nimechukua mfano wa Shirika la Magari kwenye kiambatanisho Nam. 6 inaelezwa wadaiwa sugu ingawa shirika hili linaelekea kwenye ufu, lakini hawa wanaodaiwa na Shirika la Magari baadhi yao wengi ni Waheshimiwa, lakini pili baadhi yao tayari wameshatangulia mbele ya haki; na tatu najua wapo wawili watatu wamelipa karibuni baada ya mtikisiko mkubwa.

Mhe. Spika, nashauri labda iwe kuna utaratibu wa kuwakumbusha kila mwaka, ili waweze kulipa maana yake kama Waheshimiwa na wao wanaonekana kwenye vitabu kwenye mwaka inakuwa haileti picha nzuri.

Vile vile kwa sababu Shirika hili tumeambiwa na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwamba linakwenda zake na haya madeni yatakwenda zake au yatarithiwa na Wizara yake ya Biashara, Viwanda na Masoko au Hazina katika kuona haki inapatikana? Mhe. Spika, ni hayo tu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri tumemaliza na nakushukuruni, muda wetu ni dakika 10 sijui kama unamtosha Mhe. Waziri au tuongeze muda kabisa, lakini nadhani unamtosha.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa mara nyengine tena kunikaribisha hapa kwa ajili ya kuja kutoa baadhi ya ufafanuzi wa maswali ambayo yameulizwa.

Kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza na hatimaye kumsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, vile vile kwa kukubali kuvipokea vitabu kabla ya kuipokea ripoti. Kwa kweli

ni imani yangu kwamba kwa sababu vitabu wamevipokea basi utakapowahoji pia wataipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza na kumshukuru ndugu yangu Mhe. Omar Ali Shehe ambaye ni (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika; *PAC*), kwa uwasilishaji wake wa Maoni ya Kamati ya *PAC*. *(Makofi)*

Kwa kweli nataka nimthibitishie kwamba Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa, itaendelea kuwajali wananchi wake kwa kuona kwamba rasilimali za nchi zinatumika vile ilivyokusudiwa na haitawaruhusu wajanja wachache kuzivuruga na kuzitumia visivyo rasilimali hizo, pale itakapobaini kwamba wapo watu wa namna hiyo, basi serikali imejidhatiti kuwachukulia hatua.

Mhe. Spika, maoni yake Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi nimeyapokea na serikali kwa jumla na mengi yalikuwa ni ushauri na mengine yalikuwa ni maonyo kwa serikali hasa lile alilolisema kwamba tusisubiri mpaka Wawakilishi wa wananchi na wao wakaja wakaamua. Nadhani serikali sikivu haiwezi kusubiri hapo, na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wake mahiri Dkt. Ali Mohammed Shein nafikiri ni sikivu sana. *(Makofi)*

Suala hili limekuwa likisemwa sana na Waheshimiwa Wajumbe, kwamba serikali sikivu. Vile vile na mimi nataka niseme kwa mara nyengine naendelea kuwa mpiga debe wa Kamati ya *PAC* na Baraza la Wawakilishi liwe sikivu, kwamba wiki 8 kwa Kamati ya *PAC* haziwatoshi, kwa hiyo na Baraza nalo liwe sikivu. *(Makofi)*

Jengine ambalo ninalotaka kusema ni kwamba kama nilivyoeleza na Mdhibiti amesema kwenye ripoti yake, kwamba kumekuwa na mabadiliko makubwa ya ripoti zilizokuwa zikiwasilishwa nyuma na ripoti ambazo zinazowasilishwa sasa, Mdhibiti na mimi mwenyewe nimesema kumekuwa na tofauti.

Kwa hiyo, yale ambayo yalikuwa yakifanyika huko nyuma ni tofauti kabisa na hivi sasa, ijapokuwa yapo machache ambayo tunahisi bado hayajafanyika vizuri na mimi pia nimekiri kama serikali kwamba bado na Mdhibiti ameyabainisha, kuwa yapo baadhi ya maeneo hatujafanya vizuri na hivyo hayo tutahakikisha kwamba tunayafanya vizuri. *(Makofi)*

Vile vile nilisema kwamba serikali hii tokea tumeingia madarakani tumekuwa na utaratibu wa kuwasilisha ripoti Barazani, ili Kamati ya *PAC* nayo ije

ituoneshe yale mapungufu ambayo yatakuwa bado serikali haijayafanyia kazi na ndio madhumuni yake *PAC* inachukua nafasi hiyo.

Mhe. Spika, narejea tena kusema kwamba sisi serikali tumekuwa na utamaduni sasa wa kupitia Ripoti hii ya *PAC* ndani ya Baraza la Mapinduzi, na kuanzia pale Mawaziri wote pamoja na watendaji wanatakiwa warekebishe yale mapungufu ambayo yameelezwa katika ripoti hii na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* nakubaliana naye kwamba yale mapungufu lazima serikali itayachukulia hatua, kwa sababu serikali hii ni ya watu, iliyochaguliwa na watu, kwa hiyo lazima tuwatumikie watu na wala hatuwezi kufanya vyenginevyo.

Mhe. Spika, kama mnavyosema katika michango yenu mbali mbali kwamba hatutosubiriwa hasa serikali ya Chama cha Mapinduzi kuja kuhukumiwa kwa kukoseshwa kura kwa sababu ya uovu ambao wanaulea, kwa hiyo hilo hatutalifanya hata siku moja. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nikushukuru Mhe. Mwenyekiti na ushauri wangu mwengine tunaupokea na mengi ameyaeleza lakini muda hautoshi. Kwa mfano, ameeleza masuala ya maslahi ya wafanyakazi na hilo nafikiri tuko katika hatua za mwisho katika kulifanyia kazi.

Pia ameelezea kuwa na wataalamu Taasisi hii ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, hivyo katika mwaka huu wa bajeti tutahakikisha kwamba tunaajiri wataalamu wenye sifa katika yale maeneo ambayo tunahisi katika Ofisi ya Mdhibiti hakuna wataalamu wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu naye alizungumzia kuhusu serikali haionekani kuchukua hatua, na je kuna haja ya kufanya kazi hii. Mhe. Spika, ipo haja ya kufanya kazi hizi, kwani tusipofanya kazi hii tutakuwa tunavunja Katiba kwanza; kwa hiyo hatuwezi sisi serikali tukathubutu kuvunja Katiba, lakini kama nilivyosema mwanzo kwamba mabadiliko yapo, isipokuwa na kasoro bado zipo.

Sasa madhumuni ya serikali au Mdhibiti ni kukagua na hatimaye ripoti kuwasilishwa hapa Baraza la Wawakilishi ni kwamba Kamati ya *PAC* nayo iende ikayaangalie yale ambayo yamebainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, je bado yapo au hayapo? Na hatimaye katika Kikao cha mwezi wa Aprili, basi Kamati ya *PAC* itatuletea taarifa.

Kwa hivyo, mimi naona haja ya kufanya kazi hiyo Mhe. Mjumbe naona bado ipo, kwa sababu kwanza tusipoifanya tutakuwa tunavunja Katiba, Sheria zetu za Fedha pamoja na sheria nyengine za Manunuzi kama tulivyozikubali wakati tulipozileta hapa Barazani na zikapitishwa rasmi.

Vile vile Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) na yeye ameulizia juu ya masuala la madeni ya Shirika la Magari ambalo linataka kuvunjwa.

Mhe. Spika, kwanza bado Shirika halijavunjwa na ijapokuwa hiyo azma ipo. Kwa hiyo, shirika lenyewe linahitajika kufuatilia madeni yao na wadaiwa wenyewe ikiwa ni Waheshimiwa Viongozi au wananchi wa kawaida wanapaswa kujua kwamba wanadaiwa na shirika hili na wanapaswa kulipa madeni yao. *(Makofi)*

Kwa hivyo, pale ambapo serikali italivunja shirika hili basi serikali ina taratibu zake; madeni haya yatarithiwa na Hazina kwa maana Idara ya Mitaji ya Umma na Uhakiki Mali itarithi madeni haya na serikali itaamua madeni haya ifanye nini, lakini kwa sasa bado madeni haya yanapaswa kulipwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo, naomba kwa heshima kwa mara nyengine tena Baraza lako tukufu liipokee ripoti hii na tuwaruhusu Wajumbe wa Kamati ya *PAC* kwenda kuifanyia kazi ripoti hii. Sambamba na hilo, naendelea kuwa mpiga debe wa Kamati ya *PAC*, na kwamba Baraza liwe sikivu liwaongezee muda wa kufanya kazi Kamati ya *PAC*. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nione wale wanaopokea ripoti hii ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika wanyanyue mikono, ili hatimaye ifanyiwe kazi, wanaokataa kuipokea, waliopokea na kusema ifanyiwe kazi na Kamati ya *PAC* wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niendelee kuwashukuru tena kwa kutupa mashirikiano makubwa juu ya shughuli zetu ambazo tunaelekea kufika ukingoni pengine panapo majaaliwa kesho.

Kuna matangazo mawili madogo sana. Tangazo moja ni la Mhe. Waziri wa Afya ameomba nikuarifuni kwamba jana tulikuwa na ujio wa Rais Mstaafu

wa Marekani Bill Clinton na amekuja maalum kuhusu masuala yanayohusu Wizara ya Afya kwa ajili ya wananchi wetu.

Kwa hivyo, ameniambia nikuelezeni Waheshimiwa Wajumbe, kwamba ziara hiyo ya Mhe. Rais Mstaafu Bill Clinton imefanikiwa na mazungumzo yaliyofanyika yamekwenda vizuri pale uwanjani Amaan, na shughuli zote ambazo zilikuwa zimepangwa zimefanikiwa sana. *(Makofi)*

Pili kuna tangazo la Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi; yeye anaomba aanze kufanya kazi kwa karibu sana na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hivyo, anasema kwamba wale wote ambao wanahitaji Mhe. Naibu Waziri awatembelee katika majimbo yao, basi wamuarifu tu na wajiorodheshe kwake, ili apange ratiba ya kutembelea maeneo ya majimbo yote kwa wale wanaohitaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo, nichukue nafasi hii kukushukuruni tena kwa kazi nzuri ambayo mnafanya ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya wananchi wetu.

Sasa nichukue nafasi hii niakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 06/08/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 9:00 jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 06/08/2013 saa 3:00 asubuhi)